ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe	- Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	- Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	- Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	- Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	- Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	- Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	- Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	- Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	- Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	- Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	- Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	- Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	- Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	- Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	- Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	- Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	- Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	- Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	- Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Kwanza – Tarehe 15 Juni, 2011

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:
Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 5 April, 2011.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:
Taarifa kuhusu tetemeko la Ardhi lililotokea tarehe 10 Juni, 2011.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kimataifa kuhusu tetemeko la Ardhi lilililotokea tarehe 10 Juni, 2011.

Mhe. Waziri wa Afisi ya Rais Fedha na Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Hotuba ya Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 76
Mchango wa SMZ kwa Jeshi la Polisi

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman – Aliuliza:-

Jeshi la Polisi Tanzania linajitahidi kupambana na uhalifu kwa juhudi kubwa na ndio maana nchi yetu ikawa na amani na utulivu. Hatua hiyo imetoa mchango mkubwa katika kukuza utalii na pato la taifa.

Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa nchi mbili zinaounda Jamhuri ya Muungano wa Tanziania imejipanga vipi katika kulisaidia Jeshi la Polisi ili kuendelea kulinda hali ya amani na utulivu tunayojivunia na pia kudhibiti vitendo vyengine vya uhalifu kama vile ujambazi, matumizi ya madawa ya kulevya na ajali za barabarani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake Nam. 76 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni miongoni mwa Nchi mbili huru zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kulithibitishia Baraza hili tukufu na wananchi wote kwa jumla kuwa Serikali yetu imejipanga vyema katika kulisaidia Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Vikosi vyetu vya SMZ kudhibiti vitendo vya uhalifu kama vile ujambazi, matumizi ya Madawa ya Kulevya na ajali za Barabarani.

Mhe. Spika, hivi sasa Jeshi la Polisi limeunda Kamati ya Ulinzi na Usalama katika kila Shehia (Polisi Jamii) inayoongozwa na Sheha ambapo Katibu wa Kamati hiyo atakuwa askari Polisi. Kazi za Kamati hiyo ni pamoja na kukaa vikao vya kujadili matatizo na kuyapatia ufumbuzi ndani ya Shehia zao, pia kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi juu ya hali ilivyo katika Shehia.

Mhe. Spika, Serikali yetu ipo karibu sana na Jeshi la Polisi na inatoa ushirikiano na misaada kila inapohitajika, mfano wa misaada hiyo ni vyombo vya usafiri na kusaidia upatikanaji wa mafuta wakati wa *operations* mbali mbali. Nawaomba wananchi nao wazidishe ushirikiano ili kufanikisha usalama wa Taifa letu.

Mhe. Makame Mashimba Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na kuona kuunda hizo polisi jamii . Lakini je, Mhe. Waziri Wizara yako imejipanga vipi kuweza kuzisaidia vitendea kazi hizo polisi jamii kwenye hizo shehia.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Sio Wizara yangu tu lakini serikali nzima kama nili vyoeleza inaunga mkono jitihada hizi za polisi na tutaendelea kushirikiana na polisi, kadiri ya uwezo wa serikali utakavyojitokeza ndio tutakavyoweza kusaidia shehia mbali mbali kwa ajili ya usalama wetu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Mhe. Spika, amani inajengeka vizuri zaidi pia kwa kuhakikisha kuwa usalama wa nchi unalindwa katika mipaka yake. Katika uchunguzi wangu wa taarifa kadhaa za matokeo mbali mbali ya kutumia silaha hapa Zanzibar, wanaotuhumiwa na siku nyengine kukamatwa ni watu ambao hawatoki katika visiwa hivi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuona kuwa watu wanaoingia hapa kiholela kutoka sehemu nyengine wanachunguzwa rasmi ili wasiweze kuingia na silaha.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Siku zote serikali kwa kushirikiana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama inachukua hatua mbali mbali kuhakikisha kwamba inadhibiti uingiaji kiholela katika nchi yetu, napenda nichukue mawazo ya Mhe. Salim Abdalla Hamad kama ushauri ili tuzidishe jitihada za kuhakikisha kwamba wale wote wanaoingia kinyume na taratibu basi hatua zinachukuliwa na milango yetu yote tunaidhibiti, ili watu wanaoingia nchini hapa wafuate taratibu zilizowekwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika kulinda hali ya amani na utulivu na mambo mengine nyenzo ya usafiri ni kitu muhimu, kwa kuwa jeshi la Polisi Wilaya ya Magharibi wanayo gari moja tu kwa ajili ya huduma Wilaya nzima. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kunapatikana nyenzo moja ya usafiri ili kuona kwamba jeshi la Polisi linafanya kazi yake ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Makamo wa Pili wa Rais: Naomba niuchukulie ushauri wake na niwasiliane na Wizara husika ya mambo ya Ndani tulipeleke tatizo hili. *(Makofi).*

Nam. 90
Kurejea Vitendo Viovu kwa Wanafunzi Chuo cha Mafunzo

Mhe. Ashura Sharif Ali – Aliuliza:-

Lengo la kuanzishwa kwa Chuo cha Mafunzo ni kutoa taaluma na urekebishaji wa tabia kwa wanafunzi. Aidha, chuo hubuni mbinu mbalimbali za uzalishaji mali ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea wanafunzi hao na kuachana na vitendo vya uhalifu.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea kwa sasa wanafunzi wengi wanaomaliza kukitumikia chuo cha mafunzo kurejea katika vitendo viovu vya uhalifu na kuhatarisha usalama wa watu pamoja na mali zao.

(b) Serikali haioni kwamba ipo haja ya kufuatilia ipasavyo mwenendo mzima wa uendeshaji wa chuo cha mfunzo ili kubaini matatizo yaliyopo na kuweza kukiimarisha kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa.

(c) Je, Waziri anaweza kulieleza Baraza ni mafunzo yepi hasa wanayopatiwa wanafunzi pindi wanapokuwa Chuo cha Mafunzo.

(d) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mradi maalum wa mafunzo ya urekebishaji tabia kwa wanafunzi utakaosaidia kuendesha chuo na kuweza kuwa kama vyuo vyengine vya aina hiyo ulimwenguni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 90 lenye kifungu (a),(b),(c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe Spika,

(a) Nakiri lengo kuu la kuanzishwa Vyuo vya Mafunzo ni kurekebisha tabia kwa watu wanaohalifu Sheria. Pia tumeelewa kuwa kuna baadhi ya wanafunzi wanaomaliza kutumikia Vyuo vya Mafunzo hurejea tena katika vitendo viovu vya uhalifu. Naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mwakilishi kuwa hali hii haitokani na kutopatikana kwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo hivyo bali inategemea sana na tabia ya baadhi ya wanafunzi hao ambao wamejenga tabia ya kukifanya Chuo cha Mafunzo ni nyumbani kwao.

(b) Imebainika kuwa wengi wanaorejea katika uhalifu ni wale wanaotumikia Vyuo vya mafunzo katika vipindi vifupi. Hata hivyo Vyuo vya Mafunzo vimekuwa vikipitia mara kwa mara mafunzo yanayotolewa ili lengo la kurekebisha tabia iweze kupatikana.

(c) Mafunzo yanayotolewa kwa Vyuo vyetu vya Mafunzo ni pamoja na:-

- Mafunzo ya Dini kulingana na Madhehebi ya mwanafunzi
- Kazi za mikono
- Ufundi Seremala
- Ufundi Uwashi na Ujenzi
- Ushoni
- Utengenezaji Sabuni
- Elimu ya Kilimo na ufugaji.

(d) Nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuhusu umuhimu wa kuimarisha mafunzo kupitia mradi maalum na muhakikishia kuwa hatua zinachukuliwa ya kutayarisha mpango mkakati wa kuimarisha Vyuo vya Mafunzo *(Strategic Plan)* ikiwa ni mafunzo Psychology na mafunzo mengine ya kurekebisha tabia. Pia katika mwaka wa fedha 2011-2012 tunatarajia kuanza matayarisho Sera ya Vyuo vya Mafunzo ambayo pia itasaidia huduma bora kwa wanafunzi kwa lengo la kurekebisha tabia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suali moja la nyongeza.

1) Kwanza Mhe. Waziri ni lini ametembelea Chuo hicho cha Mafunzo tokea kukaa uwaziri?

2) Atakubaliana na mimi kuwa hali ya Chuo cha Mafunzo hairidhishi hata kidogo kwa muda huu ikiwemo watoto wadogo hawan sehemu ya kulala wanopelekwa chuo hicho.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Tayari nimeshatembelea Makao Makuu ya Chuo cha Mafunzo tarehe siikumbuki hapa Unguja, lakini mbali ya Unguja nimeshatembelea vituo vyote vya Chuo cha Mafunzo Unguja na Pemba na leo ukiniuliza ramani hata kwa rafiki yangu Kangagani kwa Mhe. Hamad Masoud nitakuelezea. Kweli nakiri matatizo yapo na tumekusudia kufanya marekebisho makubwa pamoja na kujenga Chuo Kikubwa cha mafunzo huko Hanyegwamchana.

Pili nakiri kwamba kweli hali ya Chuo cha Mafunzo si nzuri na hili suala la watoto tayari tumeshalishughulikia kwa ile sehemu ambayo ya kina mama kuwapa wanafunzi watoto kwa muda huu kwanza, waende huko wakati tunajitayarisha hayo makubwa ya kuwajengea sehemu yao maalum.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri amejitahidi kuepuka chuo kikuu isije ikakubalika kuwa ni *University. (Kicheko)*

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa miaka ya nyuma kulikuwa na Chuo cha Manunda Tunguu chuo kile kilikuwa kikitoa mafunzo kwa watoto manunda. Lakini baada ya kutoa watoto wale kuwa wazuri tena wenye heshima na hupelekea pia wengine kuwa mashehe. Sijui Mhe. Waziri atatueleza nini katika Baraza lako

hili tukufu chuo kile kilikuwa kinatumia mbinu gani hata kikawa kinatoa mafunzo mazuri na watoto wakawa wazuri kiasi hicho.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nakubaliana nae kwamba ni kweli Chuo kile kwa miaka ile kilifanya kazi nzuri sana ya kutoa mafunzo kwa wale watoto wa manunda, sasa wale ukati ule taratibu za kuwafunga au chini ya sheria iliyokuwepo wakati ule haikumkinika kuwafunga, ndio tukahisi kwamba ni vyema wakapelekwa mahala maalum kupata mafunzo maalum kwa kipindi fulani, baadaye wakiwachiwa wanaweza kurekebishika. Lakini umefika wakati sasa hivi kwa hali tuliyokuwa nayo wengine wamekuwa sio ununda wanakwenda kwa uhalifu hasa, kwa hivyo tumehisi kwa mujibu wa sheria zilizopo kwanza wafuate mkondo wa sheria.

Lakini pili nafikiri tulipitisha sheria hapa ya Mhe. Waziri ya kuwapa nafuu watoto kama wale, sasa nakubaliana na wewe kwamba hali ile ilikuwa nzuri na sisi tunaosimamia vyuo vya Mafunzo tutajitahidi kuona kwamba baadhi ya mafunzo au mwelekeo ule tunauchukua. Lakini ukweli kutokana na hali ya vijana wetu siku hizi niseme wamekithiri ada wengine hata ungewatengea kule kwa mafunzo yale basi usingewasadia, ukweli wanafanya makosa makubwa mno sasa ningeomba sana kama wazee na wawakilishi kuwanasihi watoto wetu na tuwasaidie wazee kuwalea vijana wetu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suali moja la nyongeza lenye vifungu a, b na c.

Mhe. Spika, kuna uvumi kwamba wale walimu wa wanafunzi kule chuoni wao ndio wanaotoa miwanya au kuwasaidia wanafunzi kuendelea kutumia madawa ya kulevya kama bangi wakiwa kule jela. Sasa naomba kuuliza kwanza je uvumi huo ni wa kweli na kama ni kweli haoni Mhe. Waziri kwamba sababu hii pengine ndio inayofanya wanafunzi wakitoka kule ndio hawakurejesheka kitabia.

Mwisho Mhe. Waziri atachukua juhudi gani kuhakikisha kuwa askari kule wanakuwa waadilifu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Naomba nijibu kwa pamoja, uvumi kweli upo na nchi kama yetu na nchi nyengine siku zote uvumi unakuwepo, lakini suala la msingi ukishasikia uvumi basi ufanyie kazi. Na sisi tuliupata uvumi huo na tumekuwa tukiufanyia kazi lakini bado hatujabaini ushahidi, kwa hivyo nakushukuru kwa kutueleza hilo kwa hivyo tutazidi kuimarisha hatua zetu za kuanya upelelezi ndani ya vyuo vya Mafunzo, lakipi pia hata kwa hawa askari uliosema

tumeweka hatua kali kabisa tukimbaini askari yeyote anashiriki katika vitendo kama hivyo ni *summary dismisal* moja kwa moja hilo hakuna masihara.

Nam. 10

Makusanyo ya Taasisi za Muungano Ziliopo Zanzibar

Mhe. Abdalla Juma Abdalla - Aliuliza:-

Pamoja na ukweli kwamba Suala la Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na Mashirika ni suala la Muungano, kama ilivyotajwa na Kifungu cha 4, Nyongeza ya Kwanza 10 ya Katiba ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini kwa kuzingatia haja ya kuufanya Muungano huu unufaishe pande zote mbili, imekubalika kuwa makusanyo yote yanayokusanywa na Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar yanatakiwa kutumika hapa hapa Zanzibar kwa maslahi ya walipa kodi wa Zanzibar.

(a) Kwa nini makusanyo na matumizi hayo yasiidhinishwe na Baraza la Wawakilishi.

(b) Kwa kuzingatia kuwa matumizi ya mapato hayo yanatumika Zanzibar, Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Zanzibar kukagua matumizi ya Taasisi hizo.

(c) Kwa nini Baraza la Wawakilishi kupitia Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *(P.A.C)* haina nafasi ya mapato na matumizi ya makusanyo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo -Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi Nam. 10 lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kila ifikapo mwezi Juni serikali huwa inawasilisha bajeti yake ya mwaka Serikali inapowasilisha Bajeti yake ya mwaka katika Baraza lako tukufu huwa inawasilisha pia mapato na matumizi ili yaridhiwe na Baraza lako tukufu.

Katika uwasilishaji wake huo wa bajeti msingi mkubwa ni kuwasilisha mapato na matumizi ya Serikali ili yaridhiwe na Baraza lako tukufu. Mapato yanayowasilishwa huwa ni mapitio ya makusanyo yanayotarajiwa kukusanywa na taasisi za Zanzibar pamoja na taasisi za Muungano zinazokusanya mapato zilizoko Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, Mapato yanayokusanywa na taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hutumiwa na Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa maana hiyo, taasisi zinazotumia mapato hayo kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Zanzibar.

Kwa taasisi za Muungano ambazo hazitumii mapato yanayoingia SMZ taasisi hizo hukaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu wa SMT.

Mhe. Spika, kama nilivyoanza kutoa ufafanuzi katika kifungu (a) na (b). Baraza lako tukufu kupitia Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika inayo nafasi ya kujua namna gani mapato hayo yaliyokusanywa pamoja na matumizi yake. Baraza hilo ndilo lililopewa dhamana ya kupitisha kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar makadirio ya makusanyo hayo na matumizi yake kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Ismal Jussa Radhu: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa sababu mbali ya masuala ya mapato na kodi za watu binafsi na mashirika kwa suala la muangano yapo mambo mengi ambayo yanahusika na uchumi katika orodha hii iliyopo katika nyongeza ya kwanza katiba ya Jamhuri ya Muungano, kwa sababu uchumi sio suala la muungano lakini kama tulivyosema mara nyingi nyezo kuu wa kuendesha uchumi yakiwemo masuala haya ya kodi na mabenki, sarafu na fedha za kigeni yamewekwa katika orodha ya Muungano.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba wakati sasa umefika katika mchakato unaokusudiwa kuanzishwa katika katiba mpya, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikachukua hatua ya kuona mambo haya ya kuhusu uchumi yakarejeshwa katika udhibiti wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili katika kazi yake kubwa ya kusimamia uchumi Waziri wetu wa Fedha awe na udhibiti kamili na kuweza kurejesha uchumi wetu vile ambavyo Zanzibar itaona inafaa kwa maslahi ya watu wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Kwanza nataka nikubaliane nao asilimia mia moja *(Makofi)* Masuala ya uchumi sio masuala ya muungano, lakini baadhi ya mambo haya yamo katika orodho ya Muungano. Kwa sababu Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameshasema mchakato wa kuandaa katiba mpya utaanza hivi karibuni nitawaomba sana Wazanzibar wasisitize hilo, kuyaondoa katika orodha ya

Muungano kutampa nafasi Waziri wa Zanzibar anayesimamia masuala ya uchumi kuyasimamia vyema katika katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Salim Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa *TRA* ni taasisi ya Muungano inayofanya kazi katika sehemu zote mbili za Muungano, kwa kuwa bidhaa za Zanzibar kama vile magari yanayotoka ughaibuni kama vile Japan yakifika pale Dar es Salaam bandarini huwa hayaruhusiwi kuwa ni *transit* kama vile yanavyopita ya Zambia pamoja na Ruwanda, badala yake hutakiwa kufanyiwa *clearence* na kulipa kodi na matokeo yake ikija tena hapa Zanzibar vile vile tunatakiwa kufanywa *clearence* nyengine jambo ambalo ni *double taxatation.*

a) Kwa hivyo, je Wazanzibari tumefaidika na nini katika Muungano huu kwamba bidhaa za Rwanda zinapita pale kama *transit goods*, lakini bidhaa za Zanzibar ni lazima zifanyiwe *clearence* na gari ikifika huku ifanyiwe tena *clearence*, hiyo si ndio *double taxation.*

b) Mhe. Spika, kama Muungano unawanufaisha wa Zambia, Rwanda na Burundi lakini sisi tunafanyiwa *double taxation*. Je, Muungano wa namna hii una faida kwetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nitoe ufafanuzi kidogo kuna magari yanayotoka Zanzibar ikiwa hayapelekwi kubakia Dar es Salaam yanakwenda Zambia, Uganda, Burundi, Rwanda hayo yanatakiwa kwa mujibu wa sheria yapite kama ni *transit good*, hayatakiwi tena kutozwa ushuru. Hivyo, yanatakiwa kuangaliwa tu kwamba haya magari ni halali yanapita na *destination* sio Tanzania yanatakiwa kwenda.

Mhe. Spika, suala la pili ni lile ambalo walilosema kwamba kuna magari ambayo yanaingia Tanzania Bara. Mimi nataka nithubutu kusema kwamba suala hili limejadiliwa kwa kipindi kirefu katika Kamati ya Kero za Muungano na uamuzi umetoka, lakini nashangaa kama wenzetu bado wanatoza ushuru wa ziada kwa magari ambayo tayari yameshatozwa ushuru, nadhani tutalipigia tena kelele na nafikiri wakati huu nitakuwa mkali zaidi, na nitaiomba kamati watendaji ambao wanafanya hivyo wa *TRA* wachukuliwe hatua.

Mhe. Spika, la mwisho walisema faida tunayoipata kwenye Muungano mimi nataka niseme kwamba faida ziko nyingi tunazipata kwenye Muungano, lakini kasoro hizi zinazojitokeza zisituvunje moyo ni kwamba muda tunao, uwezo tunao na tutazirekebisha.

Nam. 47

Uvamizi wa Eneo Liliopo Idara ya Nyaraka

Mhe. Amina Iddi Mabrouk – Aliuliza:-

Suala la utunzaji wa nyaraka ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi pamoja na kulinda historia. Zanzibar ni miongoni mwa nchi inayosifika kwa utunzaji mzuri wa nyaraka zake. Lakini inasikitisha kwamba eneo la Idara ya Nyaraka limevamiwa na raia na hivi sasa Idara hiyo imo katika uzio (*fence*) pamoja na nyumba ya wananchi wa kawaida. Jambo hilo hutoa tafsiri mbali mbali kwa wageni wanaokwenda idarani hapo kufanya utafiti. Kwa kuwa idara hiyo hutunza nyaraka mbali mbali muhimu na kwa kuwa usalama ndani ya jengo hilo ni mdogo.

(a) Je, Mhe. Waziri unatueleza nini kuhusiana na kadhia hiyo nzito.

(b) Kwa kuwa kila mmiliki wa eneo hutakiwa kupewa eneo kutokana na mipaka maalum, Je, ni ipi mipaka ya jengo la Idara ya Nyaraka.

(c) Kutokana na kadhia hiyo Serikali haioni kuwa kuna haja ya kununua nyumba iliyomo ndani ya jengo la Idara na ile nyumba iliyopo pembezoni mwa Idara hiyo ili kulinda usalama wa nyaraka na hadhi ya Idara ya Nyaraka.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu swali hilo naomba kutoa maelezo ya msingi yanayohusiana na suala lake.

Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa nyaraka ni hazina muhimu kwa maendeleo ya Taifa na Historia ya Nchi yetu. Aidha, Zanzibar ina hadhi kubwa duniani kwa utunzaji bora wa nyaraka. Kwa kufahamu uzito wa suala hili, Serikali kupitia Baraza lako tukufu iliandaa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2008 ili kusimamia vyema hifadhi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa. Kutokana na uzito huo Mhe. Rais wa Zanzibar wa awamu ya saba inayoongozwa na Dk. Ali Moh'd Shein ameifanya kuwa ni idara kamili badala ya kuwa sehemu ya Idara ya Makumbusho na Nyaraka za Taifa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya msingi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, wizara inalifahamu tatizo liliopo la uvamizi wa eneo ambapo nyumba ya mwananchi imejengwa hadi kwenye uzio wa jengo la Nyaraka na tayari tunalifanyia kazi na njia moja wapo ni kuinunua nyumba hiyo.

(b) Napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kuwa idara inayo michoro inayoonesha mipaka ya eneo hilo kutoka Idara ya Upimaji na kupewa hati na Idara ya Ardhi na Usajili Zanzibar.

(c) Kama nilivyotangulia kusema, wizara imeanza kuchukua hatua za awali za kuinunua nyumba hiyo kwa lengo la kuongeza usalama wa jengo la nyaraka pia tumeanza kufikia kutatua eneo jengine la kujenga jengo jipya la kutunzia nyaraka na kumbukumbu za Taifa, kutokana na jengo la Nyaraka la hivi sasa kutokidhi mahitaji ya sasa na siku za baadaye.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba idara ilifanya uzembe kumuachia mtu binafsi akajenga katika eneo lake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kwamba sikubaliani nae Mhe. Mwakilishi kama idara ilifanya uzembe.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali pamoja na Mhe. Waziri wote wamekiri umuhimu wa nyaraka na kwa kuwa nchi yetu ina watu wengi na vyuo vingi. Je, wizara imechukua hatua gani ya kuwaelimisha wataalamu wetu au vyuo vyengine vilivyopo nchini nyaraka zilizoko huko ili isiwe kwamba ni sehemu tu ya kuweka lakini iwe ni sehemu pia ya kutumika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, wizara yangu imechukua hatua na inaendelea kuchukua hatua ya kuwaelimisha wafanyakazi wetu katika ngazi mbali mbali ili kuhakikisha kusudio la serikali lilokusudiwa la kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu za taifa linafikiwa. Kwa kulitambua hilo wizara yangu kupitia

watumishi walioko Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa imetoa nafasi mbali mbali kwa nyakati tofauti miaka ya nyuma na hivi sasa kuwaelimisha wafanyakazi hao.

Pia serikali katika jitihada hiyo imeanzisha Chuo cha Utawala wa Umma, miongoni mwa mambo yanayofundishwa hapo ni suala zima la *Record Management* ambalo linatolewa kuanzia ngazi ya Certificate na hivi sasa mpaka kwenye ngazi ya Diploma.

Mhe. Spika, siku hadi siku namna ya shughuli zetu zinavyoendelea basi na chuo nacho kitaendelea kuongeza viwango vya taaluma ili kuhakikisha tunakidhi mahitaji ya watumishi wa Ofisi ya Nyaraka na Ofisi nyengine za umma katika vitengo vya *Record Center*. Ahsante sana.

Nam. 73

Kutumika kwa Jina la Serikali ya Umoja wa Kitaifa

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali lakini kwa sababu suala lilofanana kama hili liliulizwa katika mkutano wa Baraza uliopita na nashukuru ulinipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza ambalo jibu lake halitafautiani sana na suala nililileta pia nashukuru pia ilikuwa hakuna haja ya kuuliza tena swali kwa jibu ambalo nimelipata kwa hivyo kwa heshima yako na ruhusa yako naomba suala langu kuliondoa.

Nam. 16

Kubomoka Daraja la Tinga Tinga

Mhe. Omar Ali Shehe - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa, wananchi wanaoishi Wesha, Kisiwani, Ndagoni, Tondooni, Birikau na kwengineko, wanapata usubufu mkubwa katika kivuko cha Tingatinga kufuatia kubomoka kwa daraja la Tingatinga. Usumbufu huo ni pamoja na wananchi wengi kupoteza maisha yao wanapojaribu kuvuka sehemu hiyo hasa wakati wa kujaa kwa maji.

Kwa kuwa sehemu hiyo ni kiunganishi kati ya vijiji na mji wa Chake-Chake, Serikali ina mpango gani wa kulijenga upya daraja hilo na hivyo kuondosha usumbufu na kuokoa maisha ya wananchi wa sehemu hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Kivuko cha Tinga Tinga kilikuwepo katika barabara ya Chake Chake hadi Wesha na kilikuwa ni kiunganishi muhimu kwa vijiji vya Tibirinzi, Chake Chake na Kijiji cha Kisiwani.

Serikali iliona tatizo la Daraja hilo na hivyo kuamua kujenga barabara mpya ya Wesha hadi Chake Chake kama mbadala wa daraja hilo baada ya kuvunjika kwake ili kuwaondoshea usumbufu wananchi wetu wanaoishi katika vijiji hivyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, naomba ieleweke kuwa Serikali imejenga barabara mpya ya Chake Chake hadi Wesha kwa kiwango cha lami kwa madhumuni ya kuwarahisishia wananchi wa maeneo hayo harakati zao za usafiri na kuwaondolea usumbufu waliokuwa wakiupata.

b) Kuhusu suala la watu, kupoteza maisha katika kivuko hicho hatujawahi kupata taarifa zozote za kifo tangu kukamilika barabara hiyo. Hata hivyo, tusingependa kuona jambo hilo likitokea na tunaomba tuwahamasishe wananchi wetu kuitumia barabara yetu mpya na yenye uhakika kwa ajili ya kuepuka matatizo watakayoyapata.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba tangu kuvunjika kwa daraja hili, watu wapatao 16 tayari wameshapoteza maisha yao.

Lakini pamoja na kujengwa kwa barabara katika kipindi hiki ambacho tayari barabara imeshajengwa wananchi wawili miongoni mwa 16 tayari wameshapoteza maisha yao. Kwa kuwa wananchi hasa wengi waliokuwa hawana fedha kuendelea kutumia njia hii kama ni sehemu rahisi kupitia katika maeneo yote yale sio Kisiwani tu na Ndagoni, Birikau na sehemu nyengine.

Kwa hivyo, kwanza serikali inatambua hivyo kwamba watu wengi wameshapoteza maisha yao, vile vile serikali katika hali kama hiyo ina mpango gani wa kufanya angalau marekebisho kidogo katika kipindi hiki cha bajeti tuliyonayo ya 2011-2012.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama nilivyotoa maelezo yangu katika jibu la msingi tumeeleza kwamba sisi wizara tokea kumalizika kwa ujenzi wa barabara hiyo hatuna takwimu wala taarifa ya mtu yeyote kupoteza maisha. Pia naendelea kutoa msisitizo wa kwamba sisi wananchi na viongozi tuendelee kushajiishana ili tutumie barabara hii mpya itakayoweza kuwaondolea usumbufu na kupoteza maisha kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, serikali kwa upande wetu kwa muda huu hatuna mpango wa kujenga kivuko wala daraja katika eneo hilo kwani tayari serikali imeshafanya maendeleo makubwa ya ujenzi wa barabara ya kudumu ya lami.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa hapo zamani daraja la Tinga Tinga lilokuwa likitumika kwa asili pamoja na kwamba njia iliyojengwa mpya ya kutoka Chake Chake mpaka Wesha. Je, haoni kama kuna umuhimu wa daraja hili kurejea tena kujengwa la Tinga Tinga, tunaishauri serikali bado iendelee kuangalia daraja hili la Tinga Tinga, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, umuhimu wa pekee wa kivuko na daraja hilo ilikuwa ni kiunganishi kwa watu wanaokaa upande mmoja hadi upande wa pili umuhimu huo umeshachukuliwa na ujenzi mpya wa barabara, hivyo umuhimu ule umeshaondoka na haupo tena.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Spika, daraja la Tinga Tinga ni miongoni mwa daraja za kihistoria katika kisiwa kile cha Pemba, na kwa kuwa barabara ile ilijengwa na Mwasisi wa Mapinduzi Mzee Abeid Amani Karume akiwa ndiye mhandisi wa ile barabara na *engineer* akiwa Mhe. Rashid Abdalla Mamba wote hao ni marehemu.

Mhe. Spika, wananchi wamelazimika kupita katika barabara ile yenye daraja bovu katika kuyaenzi na kuyaheshimu Mapinduzi ya mwaka 1964. Je, kuendelea kuliachia daraja lile kuwa bovu kwanza ni kupoteza historia ya Zanzibar na pili ni kuyadharau Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 yaliyoongozwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, madhumuni makubwa na malengo ya mapinduzi matukufu ya Zanzibar ni kuwaendeleza wananchi wake, ni imani yangu kwamba ujenzi wa barabara hii unaendana sawia na malengo ya Mapinduzi Matukufu.

Mhe. Spika, kuhusiana na dhana ya historia nakubaliana naye kulikuwa kuna umuhimu huo wa daraja hili kulibakisha katika historia. Lakini ni bahati mbaya kwamba daraja hili ni daraja la mbao na hivi tunavyozungumza ni kwamba halipo. Hivyo, tukitaka historia maana yake ni kutunza na tukitaka kutunza hilo daraja ni kuwa halipo. Mhe. Spika, kwa msingi huo historia tutaiandika kama lilikuwepo lakini kwa muda huu halipo na serikali hatuna mpango wa kujenga upya.

Nam. 84

Michango Maskulini

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Tangu mwaka 1964 baada ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, Serikali ilitangaza kuwapatia elimu bila ya malipo wananchi wote wa Zanzibar. Hata hivyo kutokana na hali halisi ya uchumi wa taifa, katika miaka ya hivi karibuni serikali kupitia wizara ya elimu iliamua wanafunzi wawe wanachangia kiasi kidogo cha fedha ili zisaidie kuimarisha huduma katika skuli zao.

(a) Je, ni kiwango gani cha fedha ambacho skuli zinatakiwa kuwachangisha wanafunzi wa msingi na wale wa sekondari kwa mwaka.

(b) Je, Mhe waziri anaelewa kwamba baadhi ya skuli zinawarejesha nyumbani wanafunzi wanaoshidwa kulipa mchango huo.

(c) Je, ni hatua gani ambazo zimechukuliwa katika kuwadhibiti walimu ambao huwanyanyasa wanafunzi ambao wazazi wao wameshindwa kuchangia fedha hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe, Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 ambalo lina sehemu (a), (b), na (c) kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza Sera ya Elimu Bila ya Malipo tokea mwaka 1964 kwa lengo la kuwapatia wanachi wote elimu bila

ya vikwazo na ubaguzi wowote ule. Katika utekelezaji wa sera hiyo, wazazi wanachangia kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kusaidia gharama za baadhi ya huduma za upatikanaji wa elimu. Kama vile ujenzi wa madarasa, gharama za vifaa vya kuandikia, michezo na sare za wanafunzi. Pamoja na kuwa wananchi wanatakiwa kuchangia kulingana na uwezo wao, wananchi ambao hawana uwezo wa kuchangia watoto wao hawazuiliwi kuendelea na masomo yao kutokana na kutoa michango hiyo. Baada ya maelezo hayo, napenda kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Kiwango cha fedha ambacho wananchi wanatakiwa kuchangia kwa kila mwanafunzi ni kama hivi ifuatavyo:

   i. Elimu ya Msingi sh. 3,000/= kwa mwaka
   ii. Elimu ya Sekondari ya Awali (Kidato cha I na II) sh. 5,000/- kwa mwaka.
   iii. Elimu ya Sekondari ya Pili (Kidato cha 3-4) Sh. 7,500/- kwa mwaka.
   iv. Elimu ya Sekondari ya Juu (Kidato cha 5 – 6) sh. 10,000/- kwa mwaka.
   v. Mafunzo ya Ualimu: Ngazi ya Cheti sh. 15,000/- kwa mwaka.
   vi. Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada sh. 20,000/- kwa mwaka.

b) Ni kosa kumrejeshwa nyumbani kwa wanafunzi ambao wazazi wao wameshindwa kutoa michango. Wizara imetoa miongozo juu ya ukusanyaji michango na kuwataka Walimu Wakuu, Wajumbe wa Kamati za skuli kutowarejesha nyumbani wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuchangia.

   Napenda kutoa wito kwa Walimu Wakuu na Wajumbe wa Kamati za Skuli kuhakikisha kuwa wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuchangia hawarejeshwi majumbani. Pia, napenda kuwashauri wazazi watimize wajibu wao wa kuchangia maendeleo ya skuli zao kwani michango yao inasaidia sana katika kufanikisha maendeleo ya watoto wao.

c) Wizara haijapokea malalamiko rasmi kutoka kwa wazazi ya kufukuzwa skuli kwa watoto wao kwa kushindwa kuchangia na hivyo hakujakuwa na haja ya kuchukua hatua ya kinidhamu kwa viongozi wa skuli zetu. Wizara itawachukulia hatua za kinidhamu vingozi au walimu watakaothibitika kuwa wamewafukuza wanafunzi au wamenyanyaswa kutokana na wazazi wao

kushindwa kuchangia fedha. Wizara itaendelea na juhudi zake za kuwaelimisha walimu na wazazi ili watambue wajibu wao katika kuleta maendeleo ya skuli zao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii naomba nimuulize swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri lenye kifungu (a), (b) na (c).

a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba wizara ndio iliyotoa muongozo wa michango hii kwa wanafunzi wetu, naomba kujua wizara ilitoa muongozo huo kwa sheria gani ya fedha ambayo iliwataka wananchi kuchangia michango mbali mbali.

b) Michango hiyo ya kuanzia msingi hadi vyuo zipo taarifa kwamba kuna fedha zinaingia moja kwa moja Wizara ya Elimu naomba kujua ni shilingi ngapi kwa mwaka na kwa nini hazionekani kwenye bajeti ya serikali.

c) Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba hana taarifa ya malalamiko, malalamiko yeye angekusudia kuyapata wapi kama si katika Baraza la Wawakilishi ambao ni wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama ambavyo nilijibu kwenye swali mama ni kweli wizara ilitoa muongozo wa wanafunzi wetu kuchangia kiasi kidogo cha fedha, lakini kama nilivyosema ni muongozo sikusema kama hii ni sheria, muongozo ni suala jengine na sheria ni suala jengine. Pia kuhusu shilingi ngapi kwa mwaka ambazo tunakusanya hizi tunazo kwa sababu tuna wakaguzi ambao tunawapeleka maskulini kukagua hesabu hizo hivyo nitamletea kwa maandishi.

Mhe. Spika, pia kuhusu fedha amesema kwamba hazionekani katika bajeti, ni kwamba fedha hizi hazionekani kwa sababu ni michango ambayo inamalizia maskulini mwao. Ni kwamba wao wenyewe walimu na kamati za skuli ndio wanaosimamia michango hii na hutumika kwa shughuli za skuli hivyo hakuna hata asilimia moja ambayo inaingia katika shughuli za wizara. Mhe. Spika, michango hii hutumika kwa ajili ya majenzi ambayo tunayaona katika maskuli yetu, wazee wameshajihika pamoja na walimu kujenga haya madarasa ya kusomea na baadae wizara humalizia kwa kuezeka.

Mhe. Spika, kuhusu swali lake la mwisho ni kwamba nilisema katika jibu mama kama wizara hatujapata malalamiko rasmi kutoka kwa mzee kuja kwa Katibu Mkuu wetu kumwambia kama kuna moja, mbili au tatu. Hivyo, ndio

tunasikia kutoka kwenu nyinyi Waheshimiwa, hivyo kama kuna mzazi yeyote ambaye mtoto wake amerudishwa skuli basi atuone kwani wizara ipo na sisi tutahakikisha kwamba tunadhibiti vitendo hivyo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Je, wizara haioni haja ya kutoa tamko la kufuta michango hiyo midogo kuwaondolea kadhia hii wananchi na watoto wa wakulima hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wizara haioni haja ya kutoa tamko la kufuta michango hii. Kwa sababu kama nilivyozungumza kuwa michango hii inatusaidia sana katika kuhakikisha elimu ya watoto wetu wa Kizanzibari inakwenda mbele, tunaiona bajeti tuliyokuwanayo, tuna mahitaji mengi ya skuli ambayo tunahitaji kujenga ili watoto wetu wasome. Sasa ni michango hii ambayo inasaidia.

Mimi nilidhani Mhe. Mwakilishi angesema kwamba wizara ihamasishe michango hii ili wazee watoe.

Kwa sababu Mhe. Spika, tumetoka ule utamaduni wetu wa zamani wa kuchangia na ni mzuri kama viongozi basi turudi huko kwenye utamaduni wetu wa zamani ambao ulitupa maendeleo ya haraka baada ya mapinduzi kwa kujitolea. Kwa hivyo, nawaomba waheshimiwa wahamasishe kwenye majimbo yao ili wananchi wetu wachangie elimu kwa manufaa ya watoto wetu. Ahsante.

Nam. 51

Kukosekana Maji Safi kwa Wananchi wa Kengeja

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza:-

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kushughulikia tatizo sugu la kukosekana kwa maji safi nchini, bado wananchi wa Kengeja hawapati maji safi na salama.

Na kwa sasa wanategemea kisima kimoja tu ambacho hakikidhi mahitaji ya wananchi hao na wananchi wa maeneo mengine yakiwemo Chole, Likoni na Mahuduthi, hawapati kabisa huduma ya maji kupitia kisima hicho.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kuchimba kisima chengine ili kusogeza huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, maeneo ya Chole na Likoni yote ya Kengeja yanapata maji kutoka tangi la chini la kuhifadhi maji la Kengeja. Tangi hili linapata maji katika kisima kimoja tu, kilichopo karibu na Skuli ya Ufundi ya Kengeja. Katika hali ya kawaida maeneo haya yanapata maji kwa mgao wa kila baada ya siku nne, mgao huu unatokana na uchache wa visima na ukubwa wa mtandao wa maji na mgao.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na tatizo hilo, Mamlaka ya Maji inadhamiria kuchimba visima vya maji katika maeneo ya karibu na tangi la maji la Kengeja ili kuweza kukabiliana na upungufu wa maji katika maeneo yanayohudumiwa na mtandao huo.

Mhe. Spika, wizara yangu katika kukabiliana na tatizo hilo inadhamiria kuchimba visima vya maji katika maeneo ya mtandao wa maji ili kukabiliana na tatizo hilo la maji.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu a na b.

(a) Kwa kuwa vijiji vya Chole, Likoni na Makhuduthi havipati maji salama kama vilivyo vijiji vya Mwange, Potoa, Kibeni Migombani. Mhe. Waziri ananiambia ni lini vijiji hivi vya Kibeni Migombani Potoa na Mwange vitapata maji yaliyo salama.

(b) Kuna kisima cha Kiashange ambacho kinapeleka maji Matemwe kimeharibika kwa muda mrefu sana pale, ni lini kisima hiki kitakuwa tayari ili wananchi wa Matemwe nao wafaidike kwa maji hayo, kwa sababu sasa hivi wanapata maji kutoka Kiashange ambayo yanakuwa ni kidogo hayawezi kutosheleza baina ya wananchi wa Mkwajuni na Matemwe ni lini kitakuwa tayari.

Mhe. Spika: Hebu subiri Mheshimiwa, hivi kisima hicho ndicho kinachohusu vijiji hivyo? Kwa sababu usivuke nje ya hivyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Sijakufahamu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kisima hicho ulichokitaja ndicho kinachohusu vijiji hivyo kwa sababu usizunguke nje ya vijiji hivyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Hapana Mhe. Spika, kisima hiki hakihusiani na vijiji hivi, lakini linafanana na vijiji hivyo vya Chole kwa sababu havipati maji salama kama vilivyo vijiji vya Mwange, Potoa na Kibeni Migombani ambavyo havipati maji kama hivyo vilivyotajwa.

Mhe. Spika: kama vile wakati mwengine Makunduchi, vijiji vya Kajengwa na kwengine vikakosekana. Tengeneza swali jengine la msingi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa muongozo wako, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Takwimu ni suala muhimu sana katika uendeshaji wa serikali. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu amesema kwamba Mamlaka ya Maji ina mpango wa kuchimba kisima kipya ili kuongeza kisima katika tangi la Kengeja. Je, anafahamu kwamba maeneo ya Sipwese karibu na kwa Mwakilishi aliyeuliza swali, viko visima viwili vimechimbwa na havitumiki na bado leo kunataka kuchimbwa visima vyengine. Anakusudia kusema kwamba hawana takwimu halisi ya visima vyao?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, tuna matatizo na matatizo makubwa yanatokana na upungufu wa nidhamu ya maji yaliyoko ardhini ambayo ukichimba unapata maji yanayokuja juu na matumizi. Upungufu huo ni mkubwa sana. tumefanya utafiti kiasi cha miezi mitatu iliyopita kuthibitisha ule utafiti uliofanywa kabla. Tumegundua hata hivyo visima vya zamani vilivyochimbwa bado havitoi maji ya kutosha.

Tumezungumza na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China tutachimba visima 52 Unguja na Pemba, vyengine vitaingia katika hayo maeneo ambayo tumeshachimba visima lakini havitoki maji, tumeshafanya utafiti huo, tumeshakubaliana na hivi karibuni tutavichimba hivyo visima 52 Unguja na Pemba. Visima hivyo vitakuwa vinajitegemea kwa maana kila kisika kitakuwa na pampu yake, mitandao ya mabomba, halkadhalika kitakuwa na umeme wa jua.

Kwa hivyo, visima hivi tunategemea vitakuwa endelevu na hili tatizo lililozungumzwa katika suala mama tunategemea katika ziara aliyofanya rais juzi ambayo mimi nilishiriki tumegundua kwamba kweli kuna visima viwili lakini havitoi maji ya kutosha. Kwa hivyo, tatizo hili tumeshalifanyia utafiti na *Inshaallah* tutalimaliza punde si punde. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tunashukuru kwa kauli ya Mhe. Waziri kwa kusema kwamba, kutokana na matatizo ya maji yaliyopo katika nchi yetu ya Zanzibar mijini na vijijini kwamba serikali kupitia wizara

yake imefanya utafiti na kuweza kugundua kwamba visima vilivyokuwepo bado havitoshelezi kwa ajili ya maji. Sasa hivi serikali ina mpango wa kuchimba visima vyengine 52 kwa ajili ya kuondoa tatizo hilo. Swali langu liko hapa.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri suala lake amelielekeza kwa Zanzibar nzima na hivi karibuni Serikali ya Japani iliweza kuchimba visima katika Mkoa wa Mjini na Magharibi katika kuondoa tatizo la maji, lakini bado mpaka sasa hivi visima vimechimbwa, Wajapani wameshaondoka lakini bado tatizo la maji lipo kubwa katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi.

Sasa Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri atuthibitishie, kwa kuwa wananchi wameshazowea kuchimbiwa visima lakini maji hayapatikani. Je, hivi vyengine 52 serikali inategemea kutumia fedha nyingi, kuna uwezekano gani wa kuweza kupatikana maji wakati ambapo tayari kuna wataalamu wakubwa hawa Wajapani wamechimba visima katika Mkoa wa Mjini Magharibi na maji hayajapatikana mpaka sasa hivi naomba jawabu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri majibu yako ndio yaliyoleta maswali ya Mhe. Hamza Hassan aulize swali hili la jumla akiacha lile swali la msingi. Saidia Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nashukuru sana. Mhe. Spika, Wajapani wamefanya kazi nzuri wala sivizuri kusema kwamba wamefanya kazi labda tija hatujaiona hapana, wamegundua maeneo yenye maji, wamechimba visima, mahozi manne makubwa sana tatizo ni mtandao.

Kuna mradi wa kuchimba visima vyengine tisa Mjini Magharibi pamoja na kulaza mitandao ambayo yote imeharibika na kuweka mitandao mipya. Ametaka nimhakikishie, sidhani kwamba ni sahihi kumhakikishia mana mambo haya nayo yana mkono wa Mwenyezi Mungu, lakini Mwenyezi Mungu akitaka basi namhakikishia juhudi itakayochukuliwa na hawa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ya kuchimba visima 52 pamoja na visima hivi tisa vya Mjini Magharibi, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda mambo haya ya kusikitika kwa maji yatakuwa ni mwisho. Na tunasema ifikapo mwaka 2013 tatizo la maji Zanzibar, yaani Unguja na Pemba litakuwa limeshamalizika. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mheshimiwa wangu Ali Salum nakuomba radhi sana, umenyanyuka mara nyingi lakini tutakupa nafasi katika masuala mengine. Tunaendelea.

Nam. 41

Uimarishaji wa Vyombo vya Habari vya Serikali

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Historia inaonesha wazi kwamba, Zanzibar ni nchi ya mwanzo kumiliki Televisheni ya rangi Afrika ya Mashariki. Hata hivyo, redio ya Sauti ya Tanzania Zanzibar inawafikia wananchi wengi kwa urahisi zaidi ndani na nje ya nchi.

(a) Je, ni mwaka gani Televisheni ya Zanzibar (TVZ) na Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) zilianzishwa hapa Zanzibar.

(b) Kwa nini hadi leo TVZ haionekani ndani ya mfumo wa *Satellite* na kuna masharti gani ya kuiwezesha kurusha matangazo yake kupitia *Satellite*.

(c) Kutokana na udhaifu wa TVZ, wananchi walio wengi wa Zanzibar wameamua kujiunga na Televisheni ya Kebo *(Cable Television)*. Je, serikali inatoa kauli gani kuhusiana na suala hili.

(d) Kwa kuwa Zanzibar ni nchi ya pili inayounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vya habari vina mchango mkubwa wa kuitangaza nchi, kwa nini hadi leo redio yetu iitwe "Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) na isiitwe Sauti ya nchi ya Zanzibar (SYZ) au jina jengine la utambulisho wa nchi yetu."

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 41 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Televisheni Zanzibar (TVZ) ilianzishwa mwaka 1973 na kufunguliwa rasmi tarehe 12/01/1974 katika kuadhimisha sherehe za kutimiza miaka kumi ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na Matangazo ya Mwanzo ya Redio yalianza kurushwa Machi, 15 mwaka 1951 na yalitolewa na Sauti ya Unguja ambayo kwa sasa inaitwa Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ).

(b) Sababu kuu ya msingi iliyopelekea hadi hii leo TVZ kuwa haionekani ndani ya mfumo wa *Satellite* ni maamuzi. Bado hatujaamua na tukiamua basi hakuna cha kutuzuia. Sharti kuu la kuiwezesha TVZ kurusha matangazo yake kwa njia ya *satellite* ni kukodi '*transponder'*

ukishafanya hivyo pamoja na kufunga *Uplink* (dishi la kurushia matangazo kuyapeleka kwenye *satellite)*, kazi huwa imekwisha. Gharama za kukodi ya '*transponder'* ni jumla ya USD 81900 kwa miezi mitatu (3).

(c) Wananchi wamejiunga na *'Cable Television'* si kwa sababu ya udhaifu wa TVZ bali ni kwa sababu ya mahitaji mbali mbali yanayoambatana na utashi wao wa kuona michezo (*Sport*), dini, michezo ya kuigiza, *TVZ*, *TBC*, *ITV* na kadhalika, wananchi wanachokifuatia katika *Cable TV* ni wingi wa vipindi. Ni wananchi wa Wilaya ya Mjini tu, wanaomudu malipo ya Tshs. 16,000/= kwa mwezi ndio wanaopata huduma hii ya *Cable*, lakini wananchi walio wengi bado wanaangalia Televisheni Zanzibar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu ambayo sikuyapenda ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifugu a na b.

(a) Amesema suala la kujiunga na *satellite dish* ni suala la kuamua na kwamba serikali hadi hii leo haijaamua. Katika hali ya utandawazi wa dunia ya leo ni suala la kuamua au ni suala ambalo linakwenda na wakati katika uso wa dunia.

(b) Mhe. Spika, naomba kujua mwezi wa Machi – April katika kika cha Baraza la Wawakilishi Mhe. Waziri aliahidi kwamba ndani ya mwezi wa Aprili wataingia katika mfumo wa *digital* na pia televisheni Pemba itaonekana. Naomba kujua hadi leo lipi limefanyika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kuhusiana na suala la *digital* kwa taarifa tu labda niseme kwamba tayari mitambo imeshawasili hapa na tunayo, tunachosubiri ni vile ambavyo vinatakiwa kwenda Pemba basi wakati wowote tutavipeleka Pemba na tunatarajia kuifunga mwishoni mwa mwezi wa Julai au mwanzoni mwa Agosti.

Kuhusiana na suala la *sattellite* ni kweli lakini inategemea na uwezo vile vile, kwa sababu kukodi inakuwa ni pesa nyingi sana. kwa hivyo, tutaangalia bajeti yetu itakavyoturuhusu basi tutalifanya hilo suala. Ahsante sana.

Mhe. Subeti Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. kwa kuwa Mhe. Waziri anasema mitambo imeshafika na wanategemea kuifunga mwishoni mwa mwezi wa Julai au Agosti, na kwa kuwa sasa hivi tuko katika kipindi cha bajeti na wananchi wa Pemba wanataka na wao wafaidike na kusikia pamoja na kuona michango

inayoendelea ya wawakilishi wao katika kipindi hiki cha bajeti. Ni lini hasa ataharakisha kuifungu mitambo hiyo ili wananchi wa Pemba nao wafaidike.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli, lakini ninachoomba tuwe na subira kidogo kwa sababu hili suala lilikuwa ni la muda mrefu na tumeweza kustahamili. Kwa hivyo, tumesema mwishoni mwa mwezi wa Julai au mwanzoni mwa Agosti basi mitambo yetu tutaifunga na itakuwa tayari. Kwa hivyo, naomba tustahamiliane, tuwe na subira na *Inshaallah* tutakuja kusahau yote hayo.

Nam. 62

Kuwatunza Wazee wa Zanzibar

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-

Kwa kuwa nyumba za wazee Sebleni ni chakavu kutokana na kujengwa zamani bila kufanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu.

Na kwa kuwa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu 2010 Rais wa Zanzibar Dkt. ALI MOHAMMED SHEIN alipokuwa katika mkutano wa Donge aliahidi kuwatunza wazee wa Zanzibar.

Je, serikali haioni kuwa ipo haja kutimiza ahadi ya Mhe. Rais kwa kuwajengea nyumba mpya na za kisasa wazee hao.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 linalozungumzia kufanyiwa matengenezo nyumba za wazee kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba Nyumba za Wazee Sebleni zimejengwa zamani, ni chakavu na hazijafanyiwa matengenezo tokea zilipojengwa. Ni kweli pia Mhe. Rais wa Zanzizbar ametoa ahadi ya kuwatunza wazee wa Zanzibar.

Napenda kumhakikishia Mjumbe wa Baraza lako tukufu kwamba, ahadi aliyotoa Mhe. Rais wa Zanzibar imeanza kutekelezwa hatua kwa hatua.

Mhe. Spika, ninapenda kumuarifu Mhe. Mjumbe na Baraza lako tukufu kwamba, Wizara yangu ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake

na Watoto kwa mashirikiano na Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeeleo tayari imeanza kazi ya ukarabati wa nyumba iliyoungua moto ambayo imefanyiwa matengenezo makubwa ikiwemo ujenzi wa paa jipya, utiaji wa milango na madirisha mapya, uwekaji wa plasta na utiaji rangi. Kazi hizo zinafanywa na mafundi wetu kutoka Kikosi cha KMKM.

Aidha, tumeanza kazi ya ujenzi wa uzio (ukuta) utakaozunguka eneo lote la nyumba ya wazee kwa madhumuni ya kuwahifadhi na kuwaweka wawe salama. Kazi hiyo ambayo imepangwa kugharimu shilingi 107,000,000/= inayotekelezwa na mafundi wetu wa KMKM inaendelea vizuri.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 wizara imetenga shilingi 100,000,000/= (milioni mia moja) kwa madhumuni ya kuendeleza matengeenezo ya nyumba hizo kama tulivyokusudia.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ujenzi wa nyumba mpya kwa ajili ya wazee wasiojieweza, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalichukua suala hilo na uwezo ukiruhusu litashughulikiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yameonesha kuwa serikali ina hitihada ya kutaka kuwatengenezea mazingira mazuri wazee wetu wa Sebleni. Lakini moja katika suala la kuwatunza watu basi sio jengo tu, hata kuwawezesha hali zao kuwa nzuri. Inavyosemekana kuwa kasma ya wazee wale sio nzuri na inapelekea wazee wale kwenda kwenye mitaa na kuomba omba. Je, katika hili la kuwatunza kwa kuwawezesha serikali ina mpango gani.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nadhani tunakwenda hatua kwa hatua, kidogo tulichonacho tugawane kidogo kidogo, kwanza tunawashughulikia watu waishi katika mazingira mazuri na naamini baadae posho yao huenda ikabadilika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa kuna uvumi wa kuwa nyumba zile wanaishi vijana kuliko wazee wenyewe kama lengo lililokusudiwa na serikali.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, haya mambo ya uvumi yanakuwa sio ya ukweli. Mimi mwenyewe siondoki kwa wazee wakati wowote, saa yoyote mchana usiku nipo. Sijawaona vijana pale na nikiwaona tu basi serikali itachukua hatua zinazofaa. Naomba Waheshimiwa Wajumbe msichukulie mambo ya uvumi piteni kwa wazee mkague na muone hali zao.

Nam. 7

Mswada wa Kuanzisha Ghala ya Chakula

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

KAULI ZA MAWAZIRI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kukutana hapa leo katika Baraza lako hili tukufu. Aidha, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoa kauli juu ya janga la tetemeko. Aidha, nitoe shukurani maalum kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Viongozi wa Kitaifa kwa namna wanavyoshirikiana na wizara yetu na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu vizuri.

Pia Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa namna wanavyoshirikiana na serikali yao na hivyo kuipa nafasi serikali kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi.

Mhe. Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kijiolojia Tanzania imethibitisha kuwa siku ya tarehe 10 Juni, 2011 muda wa saa 5:28 asubuhi limetokea tetemeko katika bahari ya hindi umbali wa kilomita 52 Kusini Mashariki ya Jiji la Dar es Salaam na kilomita 105 Kusini Mashariki mwa Zanzibar. Tetemeko hilo lilikuwa na ukubwa wa kipimo cha *rishta scale* 4.4 na lilitokea katika kina cha kilomita 10 chini ya maji ya bahari.

Mhe. Spika, taarifa hiyo imeelezwa kwamba, chimbuko la matetemeko katika pwani ya Tanzania ni kuteleza kwa mapande ya miamba kwenye mipasuko ya ardhi. Hii hutokea kwa sababu ya mwambao wa Tanzania kuna mipasuko mikubwa ya ardhi kama vile Bonde la Ruvu, Bonde la Mto Mzinga unaotenganisha Mbagala na Temeke na mpasuko unaotenganisha miinuko ya wazo Chuo Kikuu hadi vilima vya Pugu na ukanda wa chini wa kuelekea baharini.

Mhe. Spika, kwa kawaida matetemeko ya ardhi yanatokea mengi kwa mfululizo yanaanza yenye nguvu ndogo ndogo na kuongezeka nguvu hadi kufikia tetemeko kuu na kisha kupungua nguvu *after shocks* hadi kusimama kabisa. Wakati mwengine mwenendo huu hautokei bali panaweza kutokea tetemeko moja kuu bila ya kutokea mengine.

Mhe. Spika, kutokana na tukio hilo jiji la Dar es Salaam hususan kati kati ya jiji kuliripotiwa kutokea kwa mtikisiko uliosababisha taharuki kwa wananchi na wakaazi wa jiji hilo.

Mhe. Spika, hayo yamejitokeza Zanzibar. Baada ya kupokea taarifa ya tukio hilo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Kukabiliana na Maafa, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Kukabiliana na Maafa ilifanya mawasiliano na Kamati za Maafa za Wilaya zote Unguja na Pemba na kubaini kwamba baadhi ya sehemu za mji wa Zanzibar zilipata mtikisiko kidogo kutokana na tetemeko hilo.

Mhe. Spika, maeneo hayo ni Mji Mkongwe katika eneo la Forodhani ambapo hali ya mtikisiko ilijitokeza na kusababisha majengo ambayo yako katika hali mbaya kudata, kupasuka na kupukutika udongo. Mfano wa jengo lililoathirika ni Ofisi ya Idara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili. Athari nyengine ni pamoja na kuongezeka kwa kasi ya mawimbi ya bahari yasiyo ya kawaida. Hata hivyo, hakuna athari kubwa zilizojitokeza.

Mhe. Spika, hatua zilizochukuliwa na Idara ya Kukabiliana na Maafa. Mhe. Spika, katika kushughulikia suala hilo Idara ilichukua hatua zifuatazo:

(a) Kufanya mawasiliano na Mamlaka ya Hali ya Hewa Kanda ya Zanzibar ili kuendelea kuratibu kwa pamoja taarifa hizi na kupata mwelekeo wa tukio hilo.
(b) Kuendelea kufuatilia taarifa za mwenendo wa matetemeko hayo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Jiolojia Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa Dar es Salaam.
(c) Kuendelea kufuatilia mwenendo wa tukio hilo hapa Zanzibar.
(d) Kuandaa na kutoa taarifa ya hali ya matetemeko hayo kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Spika, ushauri na tahadhari. Mhe. Spika, katika kushughulikia suala hili serikali inachukua hatua zifuatazo:

(a) Kuendelea kuimarisha mawasiliano ya moja kwa moja na Taasisi za Kitaifa, Kanda na Kimataifa zinazoshughulikia masuala ya matetemeko ya ardhi ili kupata taarifa sahihi na kwa wakati unaostahiki.
(b) Kuendelea kutafuta eneo maalum la kuhamishia watu wakati wa matukio kama haya ikiwa ni hatua za tahadhari.
(c) Kwa kushirikiana na taasisi husika kuendelea kuyafanyia ukaguzi wa kina majengo ya Mji Mkongwe ambayo ni mabovu na

yanahatarisha usalama ili kunusuru maisha ya wakaazi wake wakati wa majanga.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Kukabiliana na Maafa inaendelea kufuatilia mwenendo wa matukio haya kupitia taasisi na vyombo vinavyohusika na kuwasiliana na Taasisi ya Utafiti wa Jiolojia Tanzania ili kuwaelezea hali iliyojitokeza Zanzibar kwa lengo la kupata ushauri juu ya hatua zinazostahiki.

Mhe. Spika, ofisi hii inaendelea kusisitiza kwamba wananchi waendelee kusikiliza na kufuatilia utabiri wa hali ya hewa pamoja na taarifa za maelekezo yanayotolewa juu ya suala hili hususan watumiaji wa bahari na kuchukua hatua zinazostahiki. Pia wananchi wanasisitizwa kutoa taarifa kwa masheha, vyombo vya ulinzi na usalama, Kamati za Maafa za Wilaya na Mikoa au Idara ya Kukabiliana na Maafa juu ya kujitokeza kwa tukio lolote lisilo la kawaida katika maeneo yao. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hiyo ndio taarifa kuhusu tetemeko ambalo limetokea katika nchi yetu. Taratibu za kanuni zinatutaka kwamba jambo hili la taarifa kama hii lisijadiliwe, isipokuwa kama kuna mambo hayajafahamika vizuri basi maswali yanaweza yakaulizwa kwa mujibu wa kifungu cha 43 (3) kama yapo. Lakini kabla ya hapo tunamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ili atoe maoni ya kamati yake.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusimama hapa kuweza kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kupitia ripoti iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambayo imeelezea tukio la tetemeko la ardhi lilitokezea hivi karibuni.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kutoa maoni ya kamati naomba kwa niaba ya Kamati na Wajumbe wote kuweza kukupa shukrani zetu za dhati kwa kuweza kutuondolea tatizo la *echo* katika ukumbi wetu huu wa Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, umetuonesha mfano mzuri sana kwamba wewe ni mtekelezaji mkubwa wa maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi kwani ni kikao tu kilichopita kutokana na malalamiko ya Waheshimiwa kutosikilizana katika kikao hiki, kwa hiyo umechukua jitihada za makusudi ndani ya miezi sita umeweza kutatua tatizo hili. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Mawaziri kuweza kuiga mfano wa Mhe. Spika. (Kicheko/Makofi)

Mhe. Spika, baada ya hayo, kwanza hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena katika kikao cha mwanzo cha Bajeti ya Kwanza ya Serikali hii ya Awamu ya Saba. Mhe. Spika, pili nakushukuru wewe binafsi kwa kusimamia Baraza letu tukufu kwa hekima na uadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, tatu nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura kwa kunichagua kwa kura nyingi ili kuweza kuja kuwawakilisha katika chombo hiki adhimu cha kutunga sheria hapa Zanzibar. Ninawaahidi kwamba nitajitahidi kuwatumikia kwa kadri ya uwezo wangu wote ili kushirikiana na serikali kuweza kuwaondolea matatizo na kuondoa umaskini hapa Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Spika, nne napenda kuwashukuru wajumbe wangu wote wa kamati kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu yetu ya kamati. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano tunayopeana katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Mhe. Spika, kwanza tunaishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuletea ripoti hii ya tetemeko la ardhi lililotokezea siku ya tarehe 10 Juni, 2011 kiasi cha umbali wa kilomita 52 kusini mashariki mwa jiji la Dar es Salaam na kilomita 105 kusini mashariki mwa Zanzibar. Tetemeko lililokuwa na ukubwa wa *rishta scale* ya 4.8 lililotokezea kilomita 10 chini ya bahari.

Mhe. Spika, kunapotokea majanga kama haya au yanayofanana na haya basi ni vyema serikali yetu kutoa taarifa kwa wananchi na pia kutoa elimu kwa wananchi ili wafanye nini pindipo yanapotokezea majanga kama haya. Lakini pia ni vyema serikali yetu kupitia Idara yetu ya Maafa kuwa na utaratibu wa kutoa tahadhari pale inapotokezea hata dalili ya majanga kama haya.

Mhe. Spika, taarifa ya serikali inasema kwamba tetemeko hili limetokana na kuteleza kwa mapande ya miamba kwenye mpasuko wa chini ya ardhi ambapo inasemekana Tanzania ina mpasuko mkubwa kuelekea baharini ambapo visiwa vyetu vya Zanzibar tuko kati kati ya bahari. Kwa hiyo, Mhe. Spika, kutokana na mazingira haya Zanzibar na sisi hatuko salama sana.

Mhe. Spika, hili ni fundisho kubwa kwa wananchi wetu kwani wengi wao wanadhani nchi yetu kuwa ni pande tu la jiwe ambalo haliwezi kukatika au kupata msukosuko mkubwa kama ilivyotokea. Ndio maana wananchi wetu wengi wanapoelekezwa kuhifadhi mazingira na kufuata ushauri wa kitaalam

hasa katika ukataji wa mawe ya miamba iliyoko ardhini basi wao huwa wakaidi na huendelea kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kamati yangu inaiomba sana serikali yetu kuzuia ukataji wa mawe katika eneo la Muwambe kule Pemba hadi hapo wananchi watakapopewa maelekezo ya kitaalam ili kukata mawe hayo kitaalam, kwani maeneo hayo yana uharibifu mkubwa sana wa mazingira yanayotokana na ukataji mkubwa wa mawe ambapo inaweza kuja kusababisha athari kubwa sana iwapo litatokezea janga kama hili la tetemeko la ardhi katika ukanda ule.

Mhe. Spika, hivi sasa Idara yetu ya Maafa ina kazi kubwa sana kutokana na dunia yetu kukumbwa na hali ya mabadiliko ya tabia nchi. Ongezeko la joto duniani na ongezeko la kina cha maji ya bahari yanayotokana na kuyeyuka kwa milima ya barafu kutokana na joto linaloongezeka duniani.

Mhe. Spika, kazi kubwa ya Idara yetu hii ya Maafa ni kutoa elimu kwa wananchi ili kuhifadhi mazingira na kufuata maelekezo ya kitaalam. Mhe. Spika, tunaiomba sana serikali yetu kuanzisha Mfuko wa Maafa ili kuweza kusaidia huduma za haraka pale panapotokezea maafa kwani hivi sasa hakuna utaratibu mzuri wa matumizi ya fedha za umma wakati yanapotokezea maafa.

Mhe. Spika, hakuna fungu lililotengwa katika shughuli hiyo na hapa wananchi wanaweza kudhania kwamba serikali yao haiwajali pale watakapotokezewa na dharura kama hiyo. Hii pia hupelekea Mkurugenzi wa Idara ya Kukabiliana na Maafa kuwa na wakati mgumu wa kuwahudumia waathirika pale tatizo linapotokea kwani hajui ni wapi ataweza kupata fedha au nyenzo za kuweza kuwahudumia wahanga kwa haraka. Kwa sababu majanga hayachagui siku wala saa ndio maana kila wakati tunatakiwa tuwe tumejiandaa katika kukabiliana na hali ya maafa.

Mhe. Spika, leo ni aibu kubwa sana kwetu sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunasoma hotuba ya bajeti lakini tumeshindwa kutenga fungu la dharura pale yanapotokezea maafa. Hii inaonesha bado tuna mapungufu katika kuwajali wananchi wetu na ndio hao waliotuleta hapa na hii inaonesha kwamba tunawajali tu kwa raha lakini kwenye shida hatuna habari nao. Kamati yangu inayaona haya ni mapungufu makubwa kwenye bajeti yetu na tunaomba waziri anayehusika kukamilisha taratibu za kisheria ili kuleta Sheria ya Mfuko wa Maafa ili tuwe na kinga ya uhakika pale yanapotokezea majanga.

Mhe. Spika, Waswahili wanasema ‘Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki’. Kwa hiyo, wananchi wametuleta hapa basi na sisi tuwaandalie mazingira mazuri pale wanapokutwa na dhiki na tuweze kuwafariji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hakuna serikali yoyote duniani inayoweza kukabiliana na maafa bila ya kusaidiwa na ndio maana huanzishwa mifuko ya maafa ili yeyote aweze kuchangia mfuko huo pale maafa yanapotokezea. Mhe. Spika, kama nchi haina mfuko huo basi hakuna njia sahihi ya kuweza kupata msaada hasa wa kifedha na haya tunayashuhudia katika nchi mbali mbali za mataifa makubwa duniani wakati maafa yanapotokezea.

Mhe. Spika, kuna maafa makubwa yametokezea duniani mfano kama Marekani, Japan, hata Haiti. Kwa hiyo, sisi Zanzibar tumejiwekea kikwazo cha makusudi ili wananchi wetu wasichangiwe wakati yanapotokezea maafa. Ili kuondoa hili ni kuanzisha mfuko huo tu wa maafa ndio maana tunahimiza serikali yetu kukamilisha hilo kwa faida ya wananchi wetu na serikali kwa jumla.

Mhe. Spika, tukio hili la tetemeko la ardhi liwe funzo kwa wale watekelezaji wa sheria tunazozitunga kwani hivi karibuni tu tulipitisha Sheria ya Majengo hasa majengo ya ghorofa kuwatumia mainjinia waliosajiliwa ili kulinda ubora wa majengo hayo yawe imara na panapotokezea maafa kama haya basi athari isiwe kubwa.

Mhe. Spika, kutokana na tukio hili tunaiomba Mamlaka ya Mji Mkongwe kuzifanyia tathmini nyumba zilizo katika Mji Mkongwe na kutoa ushauri unaofaa kwa wakaazi na wamiliki wa majengo hayo na kuyaboresha kwani majengo hayo ni ya muda mrefu na yanahitaji ukarabati ili yaendelee kuwa imara na ya kudumu kwa muda mrefu ujao. Lakini pia yaweze kuhimili athari zinazoweza kutokezea wakati wa majanga kama haya.

Mhe. Spika, pia tunaiomba serikali kuendeleza utaratibu wa serikali iliyopita wa awamu ya sita kujenga majengo mapya ya wizara zake ili kuhama katika majengo ya kurithi yaliyochakaa na ambayo hayakukusudiwa kwa ajili ya matumizi hayo. Kutokana na mahitaji ya kisasa basi ni vyema kuwa na majengo yaliyo salama zaidi na ya kisasa zaidi.

Mhe. Spika, majanga yapo ya aina nyingi ukiacha tetemeko la ardhi lakini pia kuna vimbunga, mafuriko, moto, baridi kali, joto kali, ukame, maradhi ya miripuko mfano kipindupindu na kadhalika. Lakini sisi tunapaswa tujihadhari sana na yale yanayolingana na mazingira yetu.

Mhe. Spika, ili tuweze kujiepusha nayo itabidi tuwatake wananchi wetu kuepuka kujenga kwenye vianzio vya maji ili kuepuka maradhi ya kipindupindu na majanga mengine, pia kuepuka kujenga katika mabonde yanayopita na kujaa maji wakati wa mvua. Kujiepusha na matumizi mabaya ya ardhi hasa yale yanayofaa kwa kilimo ili kujikinga na njaa na tujitahidi tusikate

miti ovyo na tupande miti mingi ili tupate vianzio vya maji vya kutosha ili kujiepusha na ukame. Mhe. Spika, tunawashauri wananchi wetu tusitupe taka ovyo ili kuepuka maradhi ya matumbo pamoja na kipindupindu. Mhe. Spika, haya yote serikali haitaweza peke yao bila ya sisi waheshimiwa kushirikiana na wananchi wetu kutoa elimu ya kinga ya maafa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa tunawaomba wananchi kusikiliza sana vyombo vya habari hasa taarifa za habari na utabiri wa hali ya hewa ili kuweza kujua taarifa za kidunia na kujua namna ya kuchukua tahadhari ya matukio namna kama haya yanapotokezea. Pia tunatoa pole kwa wananchi wote waliopata athari ya namna yoyote kutokana na kadhia ya tetemeko hilo na tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subira wote waliopatwa na maafa.

Mhe. Spika, tunakushukuru wewe na Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa taarifa hiyo ya kamati. Sasa ni zamu ya Waheshimiwa Wajumbe. Kifungu cha 43 (3) cha kanuni kinatuelekeza kwamba mjadala kwa taarifa kama hii haupo isipokuwa kama kuna jambo linahitaji ufafanuzi tunaweza tukauliza maswali. Kwa hiyo, kama maswali yapo naomba tuyaulize lakini yasiwe marefu ikaonesha kama tunajadili.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri maswali machache kuhusiana na kauli hii ya serikali. La kwanza Mhe. Spika, ametwambia kwamba kumetolewa tahadhari ya matukio kama haya kuweza kuendelea. Lakini katika hilo amesema idara inayohusika Zanzibar imekuwa ikiwasiliana na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kujua uwezekano wa matukio kama haya kuweza kuendelea. Ningeomba atusaidie je, baada ya kuwasiliana na taasisi hizi kuna taarifa zozote kwamba matukio haya yanaweza kuendelea ili wananchi wetu waweze kujua wanajiandaa vipi.

Mhe. Spika, swali langu la pili ni kwamba kwa nchi za wenzetu kwa masuala kama haya yanayohusu matetemeko ya ardhi wamekuwa na utaratibu wa kuweka vifaa ambavyo huwa vinatoa tahadhari mara vinapohisi kuna mabadiliko yasiyo ya kawaida katika bahari au ardhi. Je, kwa hapa kwetu Zanzibar vifaa kama hivyo vipo na kama havipo serikali inachukua hatua gani kuviweka ili angalau wananchi waweze kujua hata kwa muda mfupi kwamba kuna mwelekeo wa kutokea tukio kama hilo.

Mhe. Spika, la mwisho naishukuru serikali kwamba tayari imeandaa rasimu ile ya sera inayohusika na maafa lakini sijui Mhe. Waziri atatueleza kwamba kuna

hatua gani zitakazofuata baada ya kupitishwa kwa sera ile katika kuyawekea msingi wa kisheria masuala mazima yanayohusika na kukabiliana na maafa kama haya hasa kwa nchi yetu ambayo ni visiwa. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi naomba kuuliza maswali matatu kuhusiana na hoja ya Mhe. Waziri. Mhe. Spika, la kwanza Taasisi ya Utafiti wa Jiolojia Tanzania hapa Zanzibar haipo. Sasa naomba kujua je, serikali ina mpango gani wa kuitaka taasisi hii kufungua tawi hapa Zanzibar au kuanzisha chombo kama hichi ambacho kitafanya tafiti kama hizo ili kuwa rahisi kwa Wazanzibari kupata taarifa za mabadiliko ya hali ya hewa.

Mhe. Spika, la pili suala la kuanguka kwa majumba ya Mji Mkongwe ni suala ambalo tumelizoea, huanguka mara kwa mara bila hata ya kuwepo kwa upepo. Je, tukio la juzi la kutikisika kwa jumba hilo lilihusishwa vipi na tetemeko la ardhi kwa sababu masuala ya majumba ya Mji Mkongwe kuanguka ni mambo tuliyoyazoea.

Mhe. Spika, la tatu sasa hivi inakadiriwa kwamba takriban hapa Zanzibar nyumba zote zina visima vya maji binafsi na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alitwambia karibuni watachimba vyengine 50 na kidogo. Je, kwa kuwa Zanzibar ni visiwa vinavyoelea kwenye bahari ya Hindi taasisi hii inaweza kutusaidia kufanya utafiti kujua kwamba machimbo ya visima hivi na vile vya serikali na yale ya Muwambe ambayo serikali wanachimba yanaathiri vipi visiwa vya Zanzibar katika hali ya hewa na athari ambazo zinaweza kusababisha kuzama kwa visiwa hivi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kumuuliza Mhe. Waziri kuhusiana na kadhia hii. Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwamba mara nyingi matatizo haya hutokea sehemu za baharini na huathiri sana ama walioko ndani ya bahari kwa shughuli zao au walioko kando kando ya bahari. Sasa kutokana na tatizo hili kwa kipindi ambacho tunakiita kwamba ni wakati wa kusubiri lolote linaloweza kutokea Mwenyezi Mungu atuepushe. Je, serikali inachukua hatua gani kuwatahadharisha wale wanaotumia bahari kwa kipindi hichi na wale walioko kando kando ya bahari licha ya taarifa hii kutolewa ndani ya Baraza hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo kwa ufupi sana kuhusu maswali ya Waheshimiwa Wawakilishi. Aidha, naomba na mimi nijumuike na Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kutoa pole kwa wale wote walioathirika na matatizo haya.

Mhe. Spika, niendelee kumshukuru sana Mwenyekiti wangu Mhe. Hamza Hassan Juma na kamati yake kwa namna ambavyo wamekuwa mstari wa mbele kutusaidia kutupa ushauri. Katika maelezo yake aliyoyatoa hapa ilikuwa ni ushauri wa namna ya kutekeleza kazi zetu vizuri. Nataka nimhakikishie kwamba ushauri ule tumeupokea na tutaufanyia kazi kwenye masuala yote, suala la elimu kwa umma, suala la kutunza mazingira yetu, suala la kuhakikisha kwamba serikali inaangalia fungu maalum huko mbele ya safari kwenye bajeti yetu ili kuona namna gani tunaweza kushughulikia matatizo haya ya maafa.

Lakini pia jambo kubwa ambalo Mhe. Hamza Hassan Juma alilizungumzia ni kuanzisha mfuko. Nataka nimhakikishie kwamba harakati zimeanza za kuanzisha mfuko wa maafa na muda sio mrefu Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe tutakuwa na mfuko huu.

Mhe. Spika, ni kweli alichosema kwamba mfuko huu hautokuwa tu ni mchango wa serikali bali pia na wananchi, wahisani, wafadhili na wale wote watakaoona wana hamu na nia ya kusaidia watu wetu wanapotokewa na mambo haya. Kwa sababu Mhe. Spika, jambo hili ni jambo letu sote na kwa msingi huo kuwa na mfuko huu utatusaidia sana. Hivi sasa mtazamo wa ulimwengu ni ushirikishaji kwa wote kwa maana wadau wote. Kwa hiyo, tunauchukua ushauri huu na kuufanyia kazi vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu suala la majengo ya serikali tayari serikali imeshatoa uamuzi kuhusu kuwa na majengo mapya na hivi sasa utaratibu unafanywa kupitia wizara yetu kwa kutengeneza warka ili kutafuta maeneo yatakayojengwa wizara zetu mpya na kwa utaratibu ulio mzuri ili tuwe na utekelezaji wa uhakika. Pia napokea ushauri wake kuhusu vyombo vya habari ambavyo wananchi wetu wanatakiwa kuvisikiliza sana ili kuhakikisha kwamba taarifa hizi wanazipata za kutosha kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu alikuwa na maswali matatu na yaliyohusu sana hasa ni je, kuna taarifa zozote zinazoashiria kutokea matetemeko mengine. Kwa mujibu wa taarifa tulizozipata awali kwamba mwelekeo wa kutokea matatizo haya ya matetemeko madogo madogo bado upo na yanaweza yakatokea.

Kuhusu vifaa vya tahadhari ya tetemeko. Mhe. Spika, vifaa hivi niseme ukweli kabisa katika Baraza lako tukufu kwamba hatuna vifaa vinavyoweza kujua tetemeko la ardhi litatokea. Tunategemea sana wakubwa huko hususan Serikali ya Marekani katika kuwasiliana kwetu ndio ambao wanaweza kutupa kidogo mwanga wa kujua hali inakuwaje. Lakini jambo hili linashughulikiwa kikanda na kilimwengu kwa sababu ni maafa ya watu wote.

Mhe. Spika, sisi kama tulivyosema tumo kwenye utaratibu wa kupitisha sera. Katika sera yetu hiyo naamini mambo mbali mbali yatajitokeza ambayo kwa njia moja au nyengine kutokana na hali yetu ya uchumi wa nchi tutaweza kuyashughulikia. Kwa hiyo, Mhe. Spika, kwa kuwa suala la sera limeshafikia hatua ya mwisho na muda si mrefu tutalileta katika Baraza letu tukufu hili tutazidi kupata michango ya wajumbe ili kuwa na sera nzuri lakini kuwa na chombo kizuri kitakachoweza kushughulikia mambo haya ambayo ni matatizo makubwa kwa wananchi wetu.

Kwa sababu nchi masikini huathirika mara 200 zaidi ukilinganisha na nchi zile zenye uwezo. Maana masikini anakuwa masikini zaidi, kile kidogo alichonacho kinapotea ndio matatizo yanakuwa magumu zaidi. Kwa hiyo, Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba tutashirikiana vizuri ili tuwe na chombo kizuri kitakachosaidia katika matatizo haya.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kukaribisha Taasisi ya Utafiti wa Jiolojia Tanzania kuleta tawi lake hapa Zanzibar. Huko liliko tunashirikiana vizuri lakini tutazidi kupata ushauri wa kitaalam kama umuhimu huo upo kwa kushauriana basi tuweze kuwakaribisha hapa Zanzibar.

Kuhusu suala la uchimbaji wa visima na mashimo yake ambayo yanasababishwa na matofali yale ya kukata. Mhe. Spika, ukweli mashimo haya yana athari kubwa katika nchi yetu na ni uharibifu mkuwa wa mazingira.

Hivi karibuni Rais alikuwa akitembelea maeneo mbali mbali kule Pemba, tuliona mahandaki makubwa ambayo kwa kweli yana athari kubwa ya kimazingira na ndio maana wananchi wetu wameombwa kuacha kuchimba mashimo ya aina ile na serikali inachukua hatua ya kushauriana na wananchi ili kutafuta mpango mbadala wa kuendesha maisha yao badala ya kuchimba matofali yale ambayo yanaleta athari kubwa.

Vile vile wizara inayosimamia ardhi, makaazi, maji na nishati imeweka utaratibu maalum wa kutoa vibali kwa ajili ya visima ili kuepuka kuwa na mashimo bila mpango ambayo pia yanaathiri. Kwa hivyo, ningewaomba sana wananchi wale ambao wanataka kuchimba visima, wapitie wizara husika na taasisi husika ili kupata ruhusa hizi kabla ya kujichimbia ovyo ovyo visima kwa sababu vinaweza kuleta taathira kubwa kwa nchi yetu kama kisiwa na tukapata matatizo makubwa zaidi.

Kuhusu Mhe. Omar Ali Shehe, kuwa serikali inachukua hatua gani sasa za kuwajulisha wananchi ili kuwa katika hali ya kujilinda zaidi na kuweza kuchukua taadhari. Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye ripoti yangu,

nimeeleza mengi lakini jambo kubwa hapa tunalolisema ni kwamba wananchi wetu wasikilize sana taarifa za hali ya hewa na wasikilize sana maelezo mbali mbali yanayotolewa na serikali. Vile vile tusidharau elimu yetu ile ya asili, kwa sababu Mhe. Spika, kuna elimu hizi za asili ambazo zinasaidia sana katika kujua miongo hii na kutuepusha katika matatizo mbali mbali.

Mhe. Spika, hapa kuna msemo tunasema kule nyumbani kwamba "wakati wa panzi wengi unajua kuwa huku kunakuja ukame mkubwa". Kwa hivyo, vile vile wakati wa mabadiliko ya hali ya hewa wazee wetu na wananchi mbali mbali wanao uzoefu huo. Kwa hivyo, wananchi wanapoambiwa juu ya masuala haya basi wachukuwe tahadhari na wasikilize ushauri huo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana wewe pamoja na wajumbe wote kwa namna ambavyo tunashirikiana katika utekelezaji huu, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa majibu na ufafanuzi huo mbali mbali. Sasa tuone kama Waheshimiwa Wajumbe wameipokea taarifa hii. Wale walioipokea taarifa hii wanyanyuwe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Taarifa imepokelewa rasmi na Baraza.

Waheshimiwa Wajumbe, kama mnavyoelewa kwamba leo ni siku ya bajeti na tunakawaida ya kuja mapema kidogo kuliko taratibu za kawaida, lakini kwa sababu muda umewakwa kwa mujibu wa kanuni na tunataka tutenguwe hiyo kanuni. Basi nichukue nafasi hii kumuomba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kutoa hoja hiyo ya kutenga kanuni kando ili tuweze kufika mapema kuliko wakati wa kawaida wa saa 11:00. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kanuni ya 23(1) ya Baraza hili la Wawakilishi toleo la mwaka 2011, limeweka utaratibu wa nyakati za kuanza vikao vya Baraza kwa kipindi cha asubuhi saa 3:00 kamili na kipindi cha jioni saa 11:00 kamili.

Mhe. Spika, kwa kuwa leo hii jioni tunatarajia kwamba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo atawasilisha Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012, na kwa kuwa tunakusudia kumpa nafasi ya kutosha Mhe. Waziri kwa ajili ya uwasilishaji wa bajeti hiyo, pia tuweze kumaliza shughuli zote za siku ya leo

mapema zaidi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba tutenge kando kanuni hiyo ya Baraza, ili tukutane leo jioni kuanzia saa 10:00 kamili badala ya saa 11:00 jioni kama ilivyo kawaida. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya sijaahirisha kikao hiki kuna matangazo mawili au matatu. Kwanza kabisa leo ni siku ya bajeti, utamaduni wetu Waziri anayehusika na masuala ya fedha, uchumi na mipango ya maendeleo, ambaye ni Waziri wa Nchi Afisi ya Rais huwa tunamficha pahala na mkoba wake ule, ili mkoba ule usije ukafunguliwa na mtu yeyote isipokuwa mwenyewe humu ndani.

Kwa hivyo, mheshimiwa kwa utamaduni huu ambao ni mzuri tutakuficha pahala na baadae utaitwa ili uingie na bila shaka Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wanakupokea kwa furaha zote. Hilo la kwanza.

La pili, ni kwamba baada ya shughuli yetu ya kuja kusomwa hotuba ya bajeti hapo jioni, basi tumejiwekea utamaduni na kwa sababu kazi hiyo ni kubwa na tuna wageni wengi basi kutakuwa na dhifa kidogo hapo nje, ili wajumbe pamoja na wale waalikwa mbali mbali waweze kutafuna tafuna na kubadilishana mawazo hapa na pale, hiyo itastawisha zaidi yale maelezo mazuri ya bajeti ambayo Mhe. Waziri wetu atatuwasilishia hapo jioni. Kwa hivyo, taarifa hii nitakuja kuirejea tena jioni, ili kuweza kuwakaribisha wote pamoja na wageni wetu ili kujumuika nje pahala ambapo pamepangwa tuweze kubadilishana maneno na vinywaji kidogo, vinywaji baridi *(Makofi).*

Suala jengine la tatu. Waheshimiwa Wajumbe, mliomba kwa muda mrefu kwamba sisi Waheshimiwa Wajumbe pamoja na watumishi wetu huwa tunapata shida ya kuhusu pahala pa kupata chochote, inabidi tuondoke na kwende mbali kidogo ambapo wakati mwengine inavuruga mtiririko mzuri wa shughuli zetu. Kwa hivyo, naomba nitowe taarifa rasmi kwamba mkahawa wetu ambao umejengwa nyuma hapa tayari umekamilika, vifaa vyake vimo tayari na utaanza kufanya kazi rasmi siku ya Jumatatu, ile siku ya kuanza mjadala mzito hapa basi mjumbe akijisikia kiu kidogo ya kupata soda, basi anaweza akaenda katika mkahawa huo kwa kulipa. Kwa hivyo, tarehe 20/06/2011 siku ya Jumatatu tutakuwa tunaufungua rasmi hapa nyuma. Una mazingira mazuri na nafikiri mambo yako mazuri.*(Vicheko).*

Waheshimiwa Wajumbe, nataka nihimize jambo moja muhimu sana, kwa kuwa ni kawaida katika kikao cha bajeti tunawaalika watu wengi na huwa wanaitikia. Kuna wananchi wengine nao hupata hamu ya kuja kusikiliza, hivyo maana yake ni kwamba katika eneo letu hapa juu patakuwa pamejaa na itakuwa sio jambo linalopendeza wageni wakafika wakaona shughuli zinaanza, lakini ukumbi haukutimia vizuri.

Niwaombe basi muda ambao tutaahirisha kikao hiki, Waheshimiwa Wajumbe tujitahidi kufika mapemba, ili isaidie pamoja na ile itifaki ya hapo nje ya utaratibu wa kuingia humu ndani. Kwa sababu wale watakaopita katika kilango kidogo kile cha upekuzi, basi watakuwa ni wengi na inaweza ikachukua muda mkubwa, hivyo tukifika mapema itasaidia kuruhusu na hao wageni waweze kupita kwenye kilango kidogo cha *screen* na kuweza kukaa katika maeneo ambayo wamepangiwa.

Kwa hivyo, naomba tujitahidi tufike pengine kwenye saa 9:30 hivi, tuwe tumefika hapa basi itakuwa ni jambo jema na itakuwa tunaanza kubadilishana maneno hapa na pale kabla ya waziri kuja kuingia na kabla ya kikao kuanza rasmi.

Baada ya taarifa hiyo sasa Waheshimiwa Wajumbe, naahirisha kikao hiki hadi saa 10:00 leo jioni, ahsante sana.

(Saa 5:09 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 10:00 jioni)

(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati Maalum lijadili na hatimae kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012.

Pamoja na hotuba hii, pia naomba kuwasilisha vitabu vinavyoelezea Mpango wa Serikali na Bajeti. Kitabu cha kwanza kinaelezea Mapitio ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2010/2011. Kitabu cha pili kinahusu Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2011/12 na Kitabu cha tatu ni Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya na kuweza kukamilisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ambao umetoa ushindi kwa Chama cha Mapinduzi na hatimae leo

hii kukutana katika kikao hiki ambacho hujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Tunamuomba Mwenyezi Mungu akijaalie kikao hiki kiendeshe shughuli zake kwa utulivu, maelewano na upendo ili tuweze kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu. Aidha, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hii ni uthibitisho tosha kwamba wananchi wa Zanzibar wana imani kutokana na uongozi wake. Vile vile, napenda kuwapongeza wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mhe. Spika, Mwaka huu wa fedha ni mwaka maalum kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii ni bajeti ya kwanza ya Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Halikadhalika, hii ni bajeti ya kwanza inayoanza kutekeleza nusu ya pili ya Dira ya Maendeleo ya 2020. Napenda kuchukua fursa hii kumpongezi kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Makamo wa kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa maamuzi ya busara ya kuukubali muundo wa Serikali ya pamoja ambao umeanza kufanya kazi rasmi kuanzia mwezi Novemba 2010.

Aidha, pongezi za pekee nazitoa kwa Mheshimiwa Rais wa awamu ya sita, Dk. Amani Abeid Karume kwa kusimamia na kufanikisha kura ya maoni juu ya uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, utaratibu ambao ulitoa fursa ya kidemokrasia kwa wananchi kuweza kuchagua mfumo wa Serikali wanayoitaka. Vile vile nawapongeza viongozi wetu wa kisiasa pamoja na wananchi kwa busara na nia zao njema za kujenga taifa lenye amani na utulivu. Ni matumaini yetu kwamba, Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi itafanya kazi kwa umakini mkubwa na hatimae kuleta maendeleo endelevu kwa maslahi ya nchi na wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Sina budi kutoa shukurani zangu za pekee, kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi wake uliojaa busara na hekima katika kuiongoza nchi. Kwa kipindi kifupi cha kuwepo kwake madarakani ameweza kuendesha gurudumu la maendeleo kwa umahiri mkubwa. Maelekezo, muongozo na uzoefu mkubwa alionao umeanza kuleta ufanisi katika maendeleo ya Zanzibar. Aidha, napenda pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa kuniteua nimsaidie katika masuala ya fedha, uchumi na mipango ya maendeleo. Ahsante sana Mheshimiwa Rais.

Mhe. Spika, Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein imeweka bayana dhamira yake katika kuwajengea Wazanzibari misingi imara ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini, utawala

bora pamoja na kuimarisha huduma mbali mbali za jamii. Utekelezaji wa makusudio hayo unakwenda sambamba na mipango ya kipindi cha kati cha miaka mitano ijayo (2011-2015) kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II) na malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020.

Mhe. Spika, Uchaguzi Mkuu umemalizika, wakati wa kampeni tumetoa ahadi nyingi kwa wananchi wetu. Kipindi kilichopo mbele yetu ni cha kutekeleza na kutimiza ahadi zetu kwa wananchi. Serikali ya Awamu ya Saba, ikiwa ni bajeti yake ya kwanza inakusudia kuweka misingi imara ya kutekeleza ahadi ilizozitoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2010.

Miongoni mwa ahadi hizo ni kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi, uimarishaji wa elimu katika ngazi zote, kufanya mapinduzi katika kilimo na uvuvi pamoja na usanifu wa mazao ya kilimo na uvuvi. Aidha, Serikali pia imekusudia kuweka mkazo zaidi katika uimarishaji wa utawala bora, uimarishaji wa huduma za kijamii kama vile afya na elimu, usambazaji na upatikanaji wa maji safi na salama, makaazi bora, kuongeza nafasi za ajira hususan kwa vijana, kujenga ustawi wa jamii kwa kuzingatia maslahi na mahitaji ya watu maalum kama vile walemavu, wazee na watoto pamoja na uhifadhi wa mazingira yetu. Vile vile, sekta ya viwanda itapewa msukumo wa kipekee pamoja na uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi ikiwemo nishati, barabara na ustawi wa utumishi wa umma.

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ninaouwasilisha leo unabeba hatua mahsusi za mwanzo wa utekelezaji, hususan katika maeneo ya kuimarisha maslahi ya watumishi wa Umma, kuimarisha huduma za afya, upatikanaji wa maji safi na salama, umeme, barabara, uimarishaji wa viwanja vya ndege kwa lengo la kukuza utalii, uimarishaji wa sekta ya elimu, uhakika wa chakula pamoja na kuwajengea wazee mazingira mazuri ya kuishi. Kama inavyoeleweka kuwa, Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazoendelea ambayo ina idadi ndogo ya wakaazi wanaoongezeka kwa kasi kubwa mwaka hadi mwaka. Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika sekta mbali mbali, bado tuko nyuma kiuchumi na maendeleo ya kijamii. Hivyo, jitihada za makusudi zinahitajika katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi inayolingana na kasi ya ukuaji wa idadi ya watu wa asilimia 3.1.

Mhe. Spika, Mwanzoni mwa miaka ya 2000, Serikali ilianza kutekeleza Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo ulioitwa DIRA ya Maendeleo ya 2020. Lengo la DIRA ni kuwa na mwongozo ambao utatusaidia katika utekelezaji wa sekta mbali mbali katika kujenga uchumi imara unaohimili ushindani wa kimataifa na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi ambayo yatasaidia kupunguza makali ya umasikini. Pamoja na utekelezaji wa Dira hiyo, Serikali

pia inatekeleza Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*MDGs*), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 ambayo inaendana na mnasaba wa malengo yote haya. Katika utekelezaji wa Dira 2020, Serikali iliandaa na kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA) kwa awamu ya kwanza ambao uliotekelezwa kuanzia mwaka 2007 na kumalizika mwaka 2010.

Aidha, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini kwa awamu ya pili *(MKUZA II)* umeshaandaliwa na utekelezaji wake unaendelea. Vile vile, kufuatia kukamilika nusu ya kwanza ya Dira 2020, Serikali imefanya mapitio ya utekelezaji wa Dira hiyo kwa kipindi cha miaka kumi ya awali. Kwa sasa Serikali inakamilisha kuipitia ripoti na mapendekezo ya mapitio hayo ambapo mambo yaliyojitokeza yataendelea kufanyiwa kazi, lengo ni kutafuta mbinu zaidi za kupunguza umasikini kwa wananchi wa Zanzibar.

UCHUMI WA DUNIA NA KIKANDA

Mhe. Spika, Pato halisi la Taifa *(Real GDP)* katika uchumi wa dunia limekua kwa asilimia 5.0 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 0.5 mwaka 2009. Hali hiyo imetokana na kukua kwa taasisi za fedha baada ya kuhamasisha wawekezaji kuchukua mikopo ikiwemo kupunguzwa kwa gharama za uwekezaji na kupelekea kukua kwa Pato halisi kwa nchi zilizoendelea kwa asilimia 1.8 mwaka 2010 baada ya uchumi wa dunia, ukuaji wake kuzorota mwaka 2009. Uchumi wa nchi zinazochipukia kiuchumi na zile zinazoendelea umekua kwa hali ya kuridhisha. Hii inatokana na kuongezeka kwa usafirishaji mkubwa wa bidhaa nje. Ukuaji halisi wa uchumi kwa nchi hizo ulifikia wastani wa asilimia 6.1 kwa mwaka 2008 na kushuka hadi kufikia wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2009. Katika mwaka 2010 uchumi wa nchi zinazoendelea umekuwa kwa hadi asilimia 7.3.

Mhe. Spika, Athari za msukosuko wa fedha na uchumi uliozikumba nchi za Magharibi na nchi zinazoendelea ikiwemo Zanzibar umeanza kupungua taratibu. Katika nchi ambazo zinaonekana uchumi wake kukua kwa haraka, kama vile; Brazil, Russia, India, China *(BRIC)* athari hizo zimeathiri zaidi sekta za usafirishaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi. Hali hii imepelekea nchi hizi kupanga mikakati mipya ya ukuzaji wa uchumi.

Mhe. Spika, Kwa upande wa uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, umeonekana kuongezeka kwa wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2010 kutoka ukuaji wa asilimia 2.8 mwaka 2009. Aidha, uchumi katika nchi za Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* haukuathirika sana na mtikisiko wa uchumi wa dunia. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi hizi imeongezeka kutoka

wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2009 hadi kufikia wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2010. Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, uchumi umekua kwa asilimia 5.2 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 5.6 mwaka 2010. Aidha, Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika, uchumi wake kwa mwaka 2009 haukuonyesha ukuaji lakini katika mwaka 2010 umekuwa kwa wastani asilimia 3.3.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

Pato la Taifa na Ukuaji Wake

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2010 uchumi wa Zanzibar umeendelea kukua ingawa kwa kasi ndogo ikilinganishwa na mwaka 2009. Kwa bei za kudumu za mwaka 2001, Pato halisi la Taifa la Zanzibar limekua kwa asilimia 6.5 na kufikia Shilingi za Kitanzania bilioni 385.4 mwaka 2010 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2009 ambapo Pato la Taifa lilikuwa TZS 361.9 bilioni. Kasi ya ukuaji imeonekana kuwa chini ya makadirio yaliyotarajiwa ya kufikia ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2010. Hali hii imetokana na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa sekta ndogo za umeme, viwanda, ujenzi na utalii. Aidha, ukuaji wa asilimia 6.5 umechangiwa zaidi na sekta ya huduma ambayo ukuaji wake umefikia asilimia 8.7 mwaka 2010 kutoka asilimia 8.8 mwaka 2009. Mwenendo huo wa ukuaji wa uchumi umepelekea kutofikiwa kwa kiwango cha ukuaji cha asilimia 8 hadi 10 baina ya mwaka 2005 na 2010 kama kilivyotarajiwa katika Dira ya Maendeleo ya 2020.

Mhe. Spika, Wastani wa Pato la Taifa kwa mtu binafsi limekua likiongezeka mwaka hadi mwaka. Wakati idadi ya watu ilikadiriwa kufikia milioni 1.21 kwa mwaka 2010 ikilinganishwa na milioni 1.18 ya waliokuwepo mwaka 2009, ongezeko hili ni ukuaji wa asilimia 3.1 kwa mwaka. Kwa wastani, Pato la mtu binafsi kwa mwaka 2010 liliongezeka kwa asilimia 7.6 kutoka TZS 728,000 mwaka 2009 hadi kufikia TZS 783,370 mwaka 2010 hii ni sawa na Dola za Kimarekani 561 kwa mwaka 2010 kutoka Dola za Kimarekani 558 kwa mwaka 2009. Ni dhahiri kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi maskini ambayo wastani wa kipato cha mtu binafsi kiko chini ya Dola za Kimarekani 950. Azma ya Dira ya Maendeleo ya 2020 ni kufikia katika kundi la nchi zenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2020.

MWENENDO WA SEKTA ZA KIUCHUMI

Mhe. Spika, Ukuaji wa Sekta ya huduma umeonekana kupungua kutoka asilimia 8.8 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 8.7 mwaka 2010. Hali hii imetokana na kupungua kwa shughuli mbali mbali za huduma zikiwemo hoteli na mikahawa ambazo zilikuwa kwa asilimia 3.0 mwaka 2010 ikilinganishwa na

asilimia 5.0 mwaka 2009. Sekta hii ina mchango mkubwa katika uchumi wa Zanzibar ingawaje mchango wake kwenye Pato la Taifa umeshuka hadi kufikia asilimia 42.5 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 44.1 ya mwaka 2009. Sekta hii inajumuisha pia Sekta ndogo za Huduma za Usafirishaji na Mawasiliano, Utawala wa Umma, Elimu, Biashara na Afya.

Mhe. Spika, Wananchi wa Zanzibar wengi bado wanategemea kilimo kwa maisha yao ya kila siku. Hali hii ndio iliyopelekea ukuaji wa Sekta ya kilimo uimarike mwaka 2010 na kufikia asilimia 4.6 ikilinganishwa na asilimia 4.4 katika mwaka 2009. Aidha kutokana na ukuaji huo na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa Sekta ya Huduma, mchango wa Sekta hiyo katika uchumi umeongezeka kutoka asilimia 30.8 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 32.8 mwaka 2010.

Ongezeko hilo limechangiwa zaidi na shughuli za mazao na ufugaji. Mwenendo mzuri wa Sekta ya Kilimo unamaanisha kwamba juhudi za Serikali katika kuimarisha Sekta hii zimeanza kuleta matunda. Juhudi hizo ni pamoja na utoaji wa taaluma kwa wakulima, matumizi ya vifaa vya kisasa kama vile matrekta, utumiaji wa mbegu bora zenye kustahamili ukame na maradhi, mbolea, na dawa ya kuulia wadudu na umwagiliaji.

Mhe. Spika, Sekta nyengine muhimu kwa maendeleo ya uchumi ni Viwanda. Kwa bahati mbaya kasi ya ukuaji wa sekta hiyo imeshuka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2009 hadi asilimia 1.9 mwaka 2010. Mchango wa sekta hii katika uchumi umefikia asilimia 12.6 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 13.1 kwa mwaka 2009. Sababu kubwa ya kudorora kwa ukuaji wa sekta hii ni kukosekana kwa umeme nchini kwa zaidi ya miezi miwili mnamo mwanzoni mwa mwaka (10 Disemba 2009 hadi 8 Machi 2010).

UKUZAJI RASILIMALI

Mhe. Spika, Uwekezaji katika raslimali nao ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi. Mwenendo wake unaonesha kuwa ukuaji wa rasilimali umeongezeka kutoka thamani ya TZS 175.88 bilioni mwaka 2009 na kufikia TZS 200.94 bilioni mwaka 2010 sawa na asilimia 14.2. Ongezeko hilo la thamani limetokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali pamoja na sekta binafsi katika maeneo ya ujenzi wa barabara na miundombinu mingine ya kiuchumi na kijamii na ujenzi wa nyumba za kuishi na za biashara. Uwekezaji wa Miradi ya Ujenzi wa barabara na madaraja, umekuwa kwa asilimia 12.7 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 14.7 mwaka 2009.

Mhe. Spika, Kwa upande wa sekta binafsi, kiwango cha uwekezaji kimeshuka kwa mwaka 2010 ikilinganishwa na kiwango cha miaka ya karibuni, idadi ya

miradi iliyothibitishwa kutekelezwa katika mwaka 2010 ina thamani ya Dola za Kimarekani 110.34 milioni ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 270.92 milioni ya

mwaka 2009 sawa na upungufu wa asilimia 59.2. Asilimia 95.2 ya uwekezaji kati ya miradi iliyothibitishwa mwaka 2010 ulikuwa katika hoteli na mikahawa. Upungufu huu wa uwekezaji umetokana zaidi katika maeneo ya usafiri na mawasiliano, huduma za fedha, ujenzi na ukodishwaji wa majumba ya kisasa.

MWENENDO WA BEI

Mhe. Spika, Uchumi endelevu unahitaji zaidi utulivu wa bei za bidhaa na huduma. Kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2010 ilionekana kushuka na kufikia asilimia 6.1 ikilinganishwa na asilimia 8.9 mwaka 2009. Katika mwaka 2010, kasi ya mfumko wa bei kwa bidhaa za chakula ilishuka hadi asilimia 6.2 kutoka asilimia 9.6 mwaka 2009, wakati bidhaa zisizo za chakula, kasi yake ya mfumko wa bei ilipanda kidogo hadi asilimia 6.2 mwaka 2010 kutoka asilimia 6.1 mwaka 2009. Mwenendo huo wa bei umetokana na mambo yafuatayo:

- Kuanza kushuka kwa bei za chakula hasa mchele, unga na sukari katika soko la dunia kwa mwaka 2010 ukilinganisha na mwaka 2009 na
- Kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani wa mazao ya kilimo na mifugo.

SEKTA YA NJE

Mhe. Spika, Kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa mwaka ulioishia Machi 2011, hesabu ya urari wa kawaida *(current account balance)* ilipanda na kufikia nakisi ya Dola za Kimarekani 9.1 milioni kutoka ziada ya Dola za Kimarekani 4.4 milioni iliyofikiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2010. Hali hii inatokana na kushuka kwa bidhaa zinazosafirishwa kwenda nje pamoja na kushuka kwa uhaulishaji wa fedha kutoka nje *(current transfers).* Jumla ya usafirishaji wa bidhaa na huduma nchi za nje ulipanda kutoka Dola za Kimarekani 130.9 milioni mwaka ulioishia Machi 2010 na kufikia Dola za Kimarekani 140.0 milioni mwaka ulioishia Machi 2011, hasa kutokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utoaji wa huduma.

Mhe. Spika, Nakisi ya Urari wa bidhaa za biashara *(trade balance-merchandize)* iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 65.7 milioni mwaka ulioishia Machi 2010 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 86.1 mwaka ulioshia Machi 2011. Hii ilichangiwa na kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi kutoka Dola za Kimarekani 23.9 milioni mwaka ulioishia Machi

2010 hadi kufikia Dola za Kimarekani 15.6 milioni mwaka ulioishia Machi 2011, pamoja na kuongezeka kwa uagiziaji wa bidhaa kutoka nje na kufikia Dola za Kimarekani 101.7 milioni mwaka ulioishia Machi 2011 kutoka Dola za Kimarekani 89.6 milioni mwaka ulioishia Machi 2010.

Mhe. Spika, Kwa upande wa usafirishaji wa bidhaa, thamani ya usafirishaji wa zao la karafuu, ilipungua kwa asilimia 29.1 kutoka Dola za Kimarekani 10.3 milioni kwa mwaka ulioshia Machi 2010 hadi kufikia Dola za Kimarekani 7.3 milioni mwaka ulioishia Machi 2011. Kiwango cha usafirishaji wa zao la karafuu kilishuka kutoka tani 2,900 mwaka ulioishia Machi 2010 hadi kufikia tani 2,000 kwa mwaka ulioishia Machi 2011, wakati bei ya karafuu iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 3,559.8 kwa tani na kufikia Dola za Kimarekani 3,591.4 kwa tani kwa kipindi hicho hicho.

Hata hivyo, takwimu za usafirishaji wa zao hili pia zinaathiriwa sana na magendo. Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012 imeandaa mipango madhubuti ya kupandisha mikarafuu mipya pamoja na kuwatafutia wakulima soko la uhakika ambalo litapelekea kuwapatia wakulima bei nzuri itakayo kuwa na tija. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi imeelekeza kuwa na mipango mizuri ya kuyaimarisha mazao ya biashara, ikiwa ni pamoja na karafuu; mipango ambayo itasimamiwa kwa pamoja na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Biashara na Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, Kwa upande wa zao la mwani, bei ilionekana kushuka kutoka Dola za Kimarekani 264.4 kwa tani mwaka ulioishia Machi 2010 hadi kufikia Dola za Kimarekani 255.7 mwaka ulioishia Machi 2011, wakati kiwango cha usafirishaji pia kilipungua kutoka tani 10,900 hadi tani 9,300 katika kipindi hicho.

Mhe. Spika, Thamani ya uagiziaji wa bidhaa *(c.i.f)* kwa mwaka ulioishia Machi 2010 iliongezeka na kufikia Dola za Kimarekani 111.7 milioni kutoka Dola za Kimarekani 98.4 milioni mwaka ulioishia Machi 2010. Uagiziaji wa bidhaa za kudumu *(capital goods)* uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 38.6 na kufikia Dola za Kimarekani 40.3 milioni, na uagiziaji wa bidhaa za kati *(intermediate goods)* uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 38.7 milioni na kufikia Dola za Kimarekani 52.2 milioni kwa kipindi hicho.

Kupanda kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati kulitokana hasa na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia. Kwa upande wa uagiziaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida *(consumer goods)*, thamani ya uagiziaji ilishuka kwa asilimia 9.0 kutoka Dola za Kimarekani 21.1 milioni mwaka ulioishia Machi 2010 na kufikia Dola za Kimarekani 19.2 milioni mwaka ulioishia Machi 2011. Hali hii inaonyesha kuwa Zanzibar inatumia fedha

nyingi katika kuagiza bidhaa kutoka nje ukilinganisha na usafirishaji. Hata hivyo, ipo haja kubwa ya kuangalia eneo hili kwa kushajihisha wananchi wazalishe zaidi pamoja na kuwa na viwanda vidogo vidogo na vya kati ambavyo vitatoa msukumo katika usafirishaji wa bidhaa zetu za ndani.

HUDUMA ZA FEDHA

Mhe. Spika**,** Sekta ya Fedha ni miongoni mwa sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi. Tathmini inaonesha kwamba ukuaji wa Sekta hii nchini unaongezeka mwaka hadi mwaka. Amana za benki za kibiashara ziliongezeka kutoka TZS 241.0 bilioni Disemba 2009 na kufikia TZS 300.9 bilioni Disemba 2010 ikiwa ni sawa ongezeko la asilimia 24.9. Hali hii ya ukuaji mzuri wa uwekaji wa amana inaashiria wananchi wengi kufahamu umuhimu wa kuhifadhi fedha zao benki, baada ya kuongezeka kwa benki za kibiashara.

Mhe. Spika, Baada ya kukusanya amana, jukumu la benki za biashara ni kutoa mikopo kwa Sekta Binafsi. Ukopeshaji wa fedha nao umeongezeka kwa asilimia 6.9 na kufikia TZS 82.5 bilioni Disemba 2010 kutoka TZS 77.2 bilioni mwishoni mwa Disemba 2009. Bado kiwango cha ukopeshaji ni kidogo na hali hii inatokana zaidi na ukubwa wa riba. Hata hivyo, Serikali itakaa na viongozi wa benki kuangalia uwezekano wa kupunguza riba ili kuwawezesha wananchi wengi kukopa.

Kadhalika uwiano baina ya ukopeshaji na Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 8.8 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 9.4 mwaka 2010. Uchambuzi unaonesha kuwa mikopo kwa matumizi binafsi *(Personal loans)* ndio inayoongoza na kufikia asilimia 55.8 ya mikopo yote. Aidha nafasi ya pili ya ukopeshaji ilikwenda kwenye sekta ya biashara ambayo ni asilimia 12.1, utalii asilimia 6.7 wakati usafirishaji ulifikia asilimia 5.8. Hali hii ya ukopaji haiwezi kutusaidia sana, nawaomba wananchi kubadili mitazamo yao, fedha wanazokopa wazitumie zaidi kwa kufanyia biashara badala ya shughuli binafsi. Vile vile, hadi kufikia Disemba mwaka 2010, maduka 25 ya ubadilishaji wa fedha za kigeni *(Bureau de Change*) yamesajiliwa Zanzibar na yanaendelea kufanyakazi.

AJIRA RASMI

Mhe. Spika, Kiwango cha ajira katika sekta iliyo rasmi imeongezeka kutoka watumishi 47,548 mwaka 2009 na kufikia 48,701 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Kati ya hao watumishi 31,433 ni wa Serikali ambapo 14,748 ni wanawake na 16,685 ni wanaume. Waajiriwa katika Sekta Binafsi ni 13,148 ambapo kati ya hao 9,083 ni wanaume na 4,065 ni wanawake.

Kadhalika, watumishi katika Mashirika ya Umma ni 4,120. Hali hii inaonesha kwamba sekta binafsi inaendelea kukua ikilinganishwa na Sekta ya Umma.

Mhe. Spika, Katika kukabiliana na tatizo la ajira, Serikali imeweka mikakati maalum na utaratibu wa upatikanaji wa taarifa za nafasi za ajira. Serikali imeshakamilisha ujenzi wa kituo cha kutoa taarifa za nafasi za ajira kwa wanaomba kazi na taarifa za biashara na masoko kwa wajasiriamali. Kituo hicho kimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa, vitendea kazi na watendaji wa kusimamia uendeshaji. Aidha, watendaji wanapatiwa mafunzo ili wafanye kazi kwa ufanisi zaidi. Kwa upande mwengine, Serikali inaziimarisha Sheria za Kazi kwa kuzifanyia marekebisho kasoro zilizomo ndani ya Sheria hizo. Hatua hii itasaidia sana kuelewa wapi pana nafasi ya ajira na upatikanaji wake utakuwa wa uwazi zaidi.

Mhe. Spika, Katika kilele cha maadhimisho ya kutimiza miaka 47 ya Mapinduzi Matukufu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alieleza nia ya kutekeleza mpango mkubwa wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kuimarisha utendaji Serikalini na huduma kwa wananchi. Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma inahusisha maeneo ya miundo ya utumishi, mifumo ya utoaji huduma, kusimamia na kuendeleza watumishi wa umma, utunzaji wa kumbukumbu na Mageuzi ya Serikali za Mitaa.

Kukamilika kwa Programu hii kutapelekea kuwa na muundo wa utumishi wa umma unaokidhi mahitaji na matakwa ya nchi, kupatikana kwa taarifa za mahitaji halisi ya watumishi na sifa zinazohitajika. Vile vile, kutakuwa na sheria na miongozo inayotoa ufafanuzi juu ya majukumu baina ya Sekta ya Umma na Sekta ya Binafsi, uwajibikaji kwa watumishi wa umma na utoaji huduma kwa jamii pamoja na mfumo unaoridhisha wa maslahi ya watumishi wa umma.

Mhe. Spika, Katika utekelezaji wa Programu hii; Sera na Sheria za Utumishi wa Umma zimetayarishwa. Aidha, utafiti unaofafanua majukumu ya Serikali umekamilika. Serikali inaendelea kufanya mapitio na ukaguzi wa Watumishi wa Sekta ya Umma na uimarishaji wa Mfumo wa Taarifa za Wafanyakazi na kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, Kupitia kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Serikali iliahidi kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kwa nia ya kuwapunguzia makali ya maisha pamoja na kuhakikisha kuwa wataalamu wanaofundishwa kwa gharama kubwa wanabakia nchini. Kuhusu suala la mishahara ya Watumishi wa Umma, Serikali tayari imefanya mapitio na kuandaa mapendekezo mapya ya mishahara ya Watumishi ambayo itaanza kutumika mwaka wa fedha

2011/2012. Viwango vipya na taratibu zake zitatolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mapendekezo hayo ya mishahara mipya yamezingatia vigezo mbali mbali ikiwa ni pamoja na elimu aliyonayo mtumishi, uzoefu na muda aliofanyia kazi. Miundo ya Utumishi *(scheme)* imewapanga watumishi na nyongeza zao za mishahara kwa kuzingatia muda wa uajiri na kiwango cha elimu. Mbali ya hatua zinazochukuliwa, Serikali itakuwa ikiongeza maslahi ya watumishi wa umma kila mwaka pale hali ya uchumi na mapato ya Serikali itakapokuwa nzuri.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2010/2011 umeanza kwa utekelezaji wa *MKUZA II* kwa kuzingatia maeneo yaliyopewa msisitizo ambayo ni maendeleo ya watu, ustawi wa uchumi na kuimarisha utawala bora na demokrasia. Aidha, Dira ya Maendeleo ya 2020 ya Zanzibar, Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Malengo ya Maendeleo ya Milenia yameendelea kuwa nguzo katika utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2010/2011 unatekeleza program 25 na miradi 94. Jumla ya TZS 251.20 bilioni zimepangwa kugharamia program/miradi hiyo. Kati ya fedha hizo TZS 39.49 bilioni sawa na asilimia 15.7 zimepangwa kutolewa na Serikali na TZS 211.71 bilioni sawa na asilimia 84.3 zilitarajiwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha zilizotarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo TZS 78. 92 bilioni ni ruzuku na TZS 132.79 bilioni ni mikopo.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, matumizi ya kazi za maendeleo kutokana na mchango wa Serikali yalifikia TZS 24.51 bilioni sawa na asilimia 62 ya makadirio ya mwaka. Kiwango hicho cha matumizi kimepungua kwa asilimia 13.36 ambapo zilitolewa TZS 28.29 bilioni ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita 2009/2010. Sababu kuu ya kushuka huko ni kutokana na kuwa na harakati za Uchaguzi Mkuu ambapo Wizara ya Fedha ilichukua hatua maalumu za kudhibiti matumizi ya Serikali.

Mhe. Spika, Mchango wa Kazi za Maendeleo kupitia fedha za Washirika wa Maendeleo ni ya kuridhisha ikilingalishwa na mwaka uliopita. Katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 fedha zilizokwisha kutolewa na Washirika wa Maendeleo zimefikia TZS 117.71 bilioni sawa na asilimia 56 ya fedha zilizokadiriwa. Ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana, kumekuwa na ongezeko la fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo jumla ya TZS 66.98 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 75.9. Sababu kubwa ya

ongezeko hilo inatokana na kuongezeka kwa ufanisi katika kupanga, kusimamia pamoja na kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha kumekuwa na ufanisi wa upatikanaji wa taarifa za matumizi ya fedha za Washirika wa Maendeleo kutokana na matumizi ya database inayotumia mfumo wa mtandao *(Aid Management Platform).*

Klasta ya I: Ukuzaji Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

Mhe. Spika, Ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, Serikali imeugawa katika Klasta tatu. Klasta ya kwanza ni Ukuzaji Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato kwa 2010/2011 ilipangiwa kutekeleza programu 14 na miradi 27 ya maendeleo kwa kutumia jumla ya TZS 114.43 bilioni sawa na asilimia 45.6 ya Bajeti ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo mchango wa Serikali ni TZS 16.74 bilioni sawa na asilimia 14.6, wakati Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia jumla ya TZS 97.69 bilioni ikiwa sawa na asilimia 85.4 ya bajeti ya klasta hii. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2010 mpaka Machi 2011) jumla ya TZS 104.78 bilioni zimetolewa sawa na asilimia 92.2 ya bajeti ya Klasta ya kwanza. Kati ya fedha hizo Serikali imetoa TZS 13.1 bilioni sawa na asilimia 78.4 na Washirika wa Maendeleo wamechangia TZS 91.6 bilioni sawa na asilimia 93.7 ya makadirio.

Mhe. Spika, Utekelezaji halisi katika klasta hii kwa baadhi ya sekta ni kama ifuatavyo:

Kilimo:

Mhe. Spika, Sekta hii kwa mwaka 2010/2011 ililenga katika kuongeza uzalishaji wa mazao yenye ubora na tija, kuongeza ufanisi katika udhibiti wa matumizi ya maliasili na kupunguza uharibifu wa mazingira. Sekta ilipata mafanikio katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Kwa upande wa mazao ya chakula uzalishaji umeongezeka kutoka jumla ya tani 400,905 mwaka 2009 hadi kufikia jumla ya tani 440,529. Mazao yaliyoongezeka uzalishaji wake ni mpunga ambao ulitoka tani 26,980 mwaka 2009 mpaka 31,000 mwaka 2010, muhogo tani 195,674 mwaka 2009 mpaka tani 229,284 mwaka 2010, ndizi tani 100,873 mwaka 2009 mpaka 102,258 mwaka 2010 na viazi vitamu kutoka tani 53,596 mwaka 2009 hadi 58,958 mwaka 2010.

Aidha, kwa upande wa mazao ya biashara uzalishaji nao pia umeongezeka kutoka jumla ya tani 14,657 mpaka jumla ya tani 15,526. Zao lililoongezeka katika uzalishaji ni mwani ambao umetoka tani 10,248 mwaka 2009 hadi tani 12,516 mwaka 2010. Mafanikio haya yametokana na matumizi bora ya pembejeo ikiwemo usambazaji wa tani 390 za mbolea, matumizi ya trekta, mashine za kuchimbia. Vile vile, Serikali ilisambaza tani 51 za aina mbali mbali za mbegu za mpunga kwa wakulima Unguja na Pemba. Aidha, Serikali

iliendelea na kuimarisha miundo mbinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Tunduni, Bumbwisudi, Kianga, Jendele, Machigini na Tungamaa.

Mhe. Spika, Serikali ilitilia mkazo utafiti katika sekta hii na kufanya tafiti mbali mbali zikiwemo zile za mazao ya mpunga na mahindi. Kwa upande wa zao la mpunga majaribio ya aina mbegu ya *NERICA* yalifanyika kwa lengo la kutoa aina mpya za mbegu baada ya aina nne za hapo awali kuzalishwa. Mbegu ya *NERICA* itasaidia sana wakulima wetu kwani inaota katika maeneo ya juu badala ya kutegemea mabonde. Tukijipanga vizuri katika eneo hili, tunaweza kujitosheleza kwa mpunga baada ya kipindi kifupi pamoja na kusafirisha mbegu za mpunga. Tafiti nyengine za aina 55 za mpunga kutoka China zilifanyika zikilinganishwa na mbegu za kiasili ambapo 12 kati ya mbegu hizo zimeonyesha matokeo ya kutoa mazao zaidi ikilinganishwa na mbegu 3 za kiasili. Kwa upande wa mahindi aina 15 za mbegu zilifanyiwa utafiti, awamu ya kwanza ya utafiti mbegu 5 zimechaguliwa ambazo zimeonyesha kuwa na uzazi mkubwa na sasa zinaendelezwa kwa awamu ya pili.

Mifugo:

Mhe. Spika, Huduma za kinga na tiba zimeendelea kutolewa kwa wafugaji wanaohitaji huduma hizo na jumla ya mifugo 94,131 ilitibiwa na 68,533 kupatiwa kinga dhidi ya maradhi mbali mbali. Aidha idadi ya ng'ombe wa maziwa imeongezeka kutoka ng'ombe 9,500 mwaka 2009 hadi ng'ombe 11,409. Vile vile huduma za kupandisha ng'ombe kwa sindano zimeimarika ambapo kwa sasa Serikali inazalisha *Liquid Nitrogen* ya kutosheleza mahitaji Unguja na Pemba ambapo ng'ombe 459 tayari wamefaidika na huduma hiyo. Serikali imekusudia kuendeleza mifugo ili tuweze kujitosheleza kwa kitoweo na hatimae kusafirisha nchi za nje kwani soko la mifugo ni kubwa sana.

Uvuvi

Mhe. Spika, Sekta hii imedhihirisha ongezeko la uzalishaji wa samaki na thamani yake. Jumla ya tani 25,693 zenye thamani ya TZS 61.78 bilioni mwaka 2010 zimezalishwa ikilinganishwa na tani 25,397 zenye thamani ya TZS 47.71 bilioni mwaka 2009. Mafanikio haya yamechangiwa kwa kushirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za baharini pamoja na kukabiliana na uvuvi haramu. Vile vile kuendelea kutoa mafunzo na vifaa kwa wavuvi na kushajiisha wavuvi juu ya ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini. Aidha, Serikali ilitoa leseni 16 kwa wavuvi wanaovua bahari kuu. Leseni tano zilitolewa kwa mashirika ya uvuvi kutoka Seychelles na 11 zimetolewa kwa mashirika ya uvuvi kutoka Spain. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa wavuvi wetu wanawezeshwa kwa kupatiwa mikopo ili waweze kuwa na boti za kisasa zaidi na hatimae kuwa na uwezo mkubwa wa kuvua na hasa bahari kuu ambayo ina samaki wengi zaidi.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi:
Mhe. Spika, Mfuko wa kuwawezesha wananchi kiuchumi ambao ulizinduliwa 2008 ulikuwa na lengo la kutoa fursa ya kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu wananchi wenye kipato cha chini ili waweze kujiajiri pamoja na kuwawezesha kiuchumi na hatimae kuwapunguzia wananchi umaskini wa kipato . Hadi kufikia Machi 2011, Serikali imetoa mikopo yenye jumla ya thamani ya TZS 1.4 bilioni kupitia Mfuko wa JK na AK. Mikopo hiyo imetolewa kwa watu binafsi 660, vikundi 58 na *SACCOS* 10 katika mikoa yote ya Unguja na Pemba. Vile vile, Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya TZS 25.8 milioni kupitia Mfuko wa Kujitegemea.

Mhe. Spika, Idadi ya waliopata mkopo na kima kilichotolewa ni kidogo ikilinganishwa na maombi yaliyopokelewa, ni asilimia 43 tu ya waombaji ndio waliopatiwa mikopo. Katika kipindi cha miezi sita ya awali, baada ya kuzinduliwa mikopo ulipaji ulikuwa ni mzuri. Kadiri siku zilivyokuwa zikienda ulipaji haukuwa wa kuridhisha. Hata hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika watashirikiana na Benki ya Watu wa Zanzibar na *CRDB* kuandaa utaratibu wa ukusanyaji wa mikopo iliyotolewa.

Mhe. Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* unatoa mchango mkubwa katika jitihada za Serikali za kuyafikia Malengo Milenia na utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar. Programu hii inatekelezwa kutokana na mkopo wa Benki ya Dunia ambayo inatoa fedha za kutekeleza miradi inayoibuliwa na wananchi. Shughuli za Mfuko wa *TASAF* Awamu ya Pili zinatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba 2011. Hadi kufikia mwezi March 2011, jumla ya miradi 104 ya wananchi imetekelezwa ambapo miradi 54 kwa Unguja na miradi 50 kwa Pemba. Miradi yote hiyo imetumia jumla ya TZS 1.49 bilioni kwa Unguja na Pemba. Miradi hiyo inajumuisha shughuli za Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Barabara, na Viwanda vidogo vidogo. Aidha, *TASAF* imetoa mafunzo ya ujasiri amali kwa vikundi 45 vya kuweka na kukopa.

Utalii:
Mhe. Spika, utalii ni sekta muhimu katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Vile vile ina mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Sekta hii inahusisha uingiaji wa wageni kutoka sehemu mbali mbali za dunia. Ukuaji wake unaangaliwa zaidi kutokana na shughuli za hoteli na mikahawa. Kwa mwaka 2010 uingiaji wa wageni umeshuka kutoka watalii 134,954 mwaka 2009 hadi watalii 132,836 mwaka 2010. Hivyo, kusababisha kasi ya ukuaji wa shughuli za hoteli na mikahawa kupungua kutoka asilimia 5 mwaka 2009 hadi asilimia 3 mwaka 2010. Hata hivyo, Serikali bado itaendelea na lengo lake la kukuza utalii ili uwe chachu katika kuendeleza kilimo na viwanda. Sambamba na kukuza utalii,

wananchi na hasa vijana watahamasishwa kushiriki katika kilimo chenye tija zaidi.

Nishati:
Mhe. Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani inaendelea na utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa njia ya pili ya umeme kutoka Ras Kiromoni hadi Fumba ambao unatarajia kuongeza kiwango cha umeme kufikia Megawati 100. Kampuni ya *Viscas Corporation* ya Japan inaendelea na utengenezaji wa waya wa kulaza baharini. Aidha, TZS 5.30 bilioni zimetumika kuwalipa fidia wananchi 843 waliopo katika eneo la mradi kutokana na fidia ya mali na mazao yao.

Kati ya fedha hizo TZS 3.20 bilioni zimelipwa na Serikali ya Marekani na TZS 2.1 bilioni zimelipwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia sana kuwa na umeme wa uhakika. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ina mpango wa kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia upepo na jua. Juhudi za kuzalisha umeme kwa kutumia upepo ziko mbioni na tayari maeneo kama Makunduchi, Matemwe na Nungwi yameonyesha kuwa na upepo ambao una uwezo wa kuzalisha umeme.

Mhe. Spika, Chanzo kikuu cha nishati ya kupikia kwa Zanzibar ni kuni; nyumba saba kati ya nyumba 10 zinatumia kuni ikifuatiwa na matumizi ya makaa hivyo kusababisha ukataji ovyo wa miti na kuharibu mazingira. Hata hivyo, Serikali inaendeleza juhudi za kutoa taaluma ya matumizi ya nishati mbadala ikiwemo matumizi ya gesi na mafuta ya taa hadi hapo uwezo wa uzalishaji utakapokuwa mzuri na wananchi kufaidika na nishati ya umeme.

Biashara

Mhe. Spika, Serikali ilipitisha Sera ya Biashara ya Zanzibar. Moja kati ya mikakati iliyomo ndani ya sera hiyo ni kuifanya Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la Uchumi (*SEZ*) ndani ya ushirikiano wa Afrika Mashariki, ili iweze kufaidika kiuchumi ndani ya Jumuia hiyo. Serikali tayari imepata Kampuni elekezi ya *"Crisil Risk and Infrastructure"* ya India ili kufanya utafiti juu ya suala hilo. Aidha, katika kuweka mazingira bora ya biashara, Serikali imekamilisha Sheria ya kusimamia viwango na ubora wa bidhaa itakayounda taasisi ya viwango ya Zanzibar ili kusimamia na kuweka viwango vya bidhaa zinazozalishwa, zinazosafirishwa na zinazoingizwa nchini.

Usafirishaji:
Mhe. Spika, Kwa mwaka 2010/2011 Serikali imejenga jumla ya kilomita 91 za barabara kati ya kilomita 125 zilizopangwa kwa Unguja na Pemba. Kati ya hizo kilomita 25 zimekamilika kwa kiwango cha lami, kilomita 40 zimefikia kiwango cha *sub-base* na kilomita 36 zimesafishwa na kuwekwa kifusi cha mwanzo. Kazi za kuzifanyia matengenezo barabara za mijini na vijijini

zimefanyika. Vile vile, kwa hatua za awali, Serikali imeanza ujenzi wa jengo jipya la abiria na huduma katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, ujenzi unaofanywa na Kampuni ya *Beijing Construction Engineering* kutoka China. Kukamilika kwa ujenzi huo kutaongeza zaidi idadi ya watalii na hatimae kukuza uchumi.

MKUMBITA (*BEST*)

Mhe. Spika, Katika kuimarisha mazingira bora ya biashara Zanzibar, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa (MKUMBITA) ambao lengo kuu ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mazingira ya kisheria yatakayorahisisha uendeshaji biashara nchini. Hadi kufikia Machi, 2011 kazi zifuatazo zimetekelezwa chini ya Mpango huu:

- Kusimamia mageuzi katika uingiaji na utokaji katika biashara, pamoja na usajili wa mikataba ya mali zinazohamishika.
- Kupitia mfumo wa leseni za biashara.
- Kufaya utafiti wa mahitaji ya Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.
- Kupitia viwango vya kodi kwa biashara ndogo ndogo na za kati.
- Kuwapatia mafunzo watendaji kutoka Taasisi mbali mbali ambao wanashughulikia Mpango huu.

Mhe. Spika, Kuendeleza mazingira ya kisheria na biashara nchini mwetu ni kigezo muhimu katika mkakati wetu wa kuvutia uwekezaji na kupunguza umaskini, mwezi Machi mwaka huu tulizindua ripoti ya urahisi wa utekelezaji wa biashara kwa Zanzibar. Ripoti hiyo ni matokeo ya utafiti uliofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IFC*), na *"Multilateral Investment Guarantee Agency" (MIGA)* na imeonesha kuwa kati ya nchi 183, Zanzibar tuko nafasi ya 155 kwa urahisi wa kuendesha biashara.

Hata hivyo, kwa upande wa kusimamia mikataba Zanzibar inashika nafasi ya 37 kati ya nchi 183 na nafasi ya pili tukilinganishwa na nchi 34 za visiwa zenye kuendelea kiuchumi. Hali yetu sio mbaya lakini kuna haja ya kufanya mapitio ya kisheria, Kanuni na taratibu zetu katika uanzishaji na ufungaji biashara, utoaji vibali vya ujenzi, usimamizi wa mikataba, kuwalinda wawekezaji, kusimamia biashara mipakani na kupata mikopo.

Mhe. Spika, baada ya kupata matokeo ya ripoti hiyo, Serikali imeandaa mpango kazi *"Road Map''* kwa ajili ya kuyafanyia miongozo mapendekezo ya

ripoti hiyo. Mpango kazi huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwanzoni mwa mwaka 2011/2012 baada ya kupitiwa, kujadiliwa na kukubaliwa na wadau husika.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali nchi yetu hivi sasa inaongozwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hali hii imeleta utulivu amani na mapenzi baina ya wananchi, hali ambayo imeletea wafanyabiashara, wawekezaji na wageni kutokuwa na hofu ya kuja kufanya shughuli zao hapa Zanzibar. Bila ya shaka utulivu na amani uliopo itatuongezea wawekezaji, watalii na wafanyabiashara na hatimae kuongezeka kwa Pato la Taifa na ubora wa maisha ya wananchi wetu. Hapa napenda kuchukua fursa hii kuendelea kuwaomba sana wananchi kuendeleza amani iliopo na mapenzi miongoni mwetu kwani sisi sote ni ndugu.

Klasta ya II: **Huduma na Ustawi wa Jamii:**
Mhe. Spika, Klasta ya Huduma na Ustawi wa Jamii kwa 2010/2011 ambayo ni ya pili, ilipangiwa kutekeleza programu sita na miradi 37 ya maendeleo na kukadiriwa kutumia jumla ya TZS 110.88 bilioni sawa na asilimia 44.1 ya Bajeti ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Serikali ilitenga TZS 9.48 bilioni sawa na asilimia 8.5 na Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia jumla ya TZS 101.404 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 91.5 ya bajeti ya klasta hii.

Mhe. Spika, kuanzia Julai, 2010 hadi Machi, 2011, jumla ya TZS 27.3 bilioni zimetolewa sawa na asilimia 24.6 ya Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa klasta ya pili. Kati ya fedha hizo Serikali imetoa TZS 4.8 bilioni sawa na asilimia 51.1 na Washirika wa Maendeleo wamechangia TZS 22.5 bilioni sawa na asilimia 22.2 ya makadirio ya kuchangia.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi katika klasta hii ya pili kwa baadhi ya sekta ni kama ifuatavyo:

Elimu:
Mhe. Spika, moja kati ya changamoto iliyobainika katika matayarisho ya MKUZA ni kiwango kidogo cha lugha ya Kiingereza pamoja na masomo ya sayansi na hisabati kwa wanafunzi wetu na walimu. Serikali imeendelea kutoa mafunzo ya lugha ya Kiingereza kwa walimu wapatao 700 wanaosomesha madarasa ya msingi ili kutumia lugha hii kwa kufundishia masomo mbali mbali kuanzia darasa la tano. Pia katika kuwashajiisha wanafunzi wa kike wa Sekondari hasa katika kupenda masomo ya sayansi na hisabati, wanafunzi hao wameendelezwa kupitia kambi za sayansi. Vitabu vya masomo ya Jiografia, Elimu ya Uraia, Dini, Biashara na Ufundi vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli mbali mbali.

Mhe. Spika, Mfuko wa Elimu ya Juu umeendelea kutoa mikopo kwa ajili ya masomo kwa vijana wanaokwenda kusoma ndani na nje ya nchi. Jumla ya wanafunzi 1,271 wamepatiwa mikopo wakiwemo 1,058 katika vyuo vya ndani na 213 katika vyuo vya nje. Sheria mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeshapitishwa na Baraza lako tukufu ili kuufanya mfuko ujitegemee zaidi na kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, Serikali inaendelea na azma yake ya kuendelea kutoa huduma na kuimarisha ubora wa elimu kwa ngazi zote, nina furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa ujenzi wa skuli mpya 15 za sekondari za vijijini unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwisho mwa mwaka 2011. Skuli hizo ni Paje Mtule, Matemwe, Mwanda, Chaani, Uzini, Dole, Tunguu na Dimani kwa upande wa Unguja na Wawi, Ngwachani, Kiwani, Mauwani, Utaani, Pandani, Konde na Tumbe kwa upande wa Pemba. Kukamilika kwa skuli hizi kutaimarisha huduma na kupunguza msongamano wa wanafunzi katika madarasa. Aidha, skuli hizi zitatoa nafasi zaidi kwa wanafunzi kusoma masomo ya sayansi na kompyuta kwani zimejengwa pamoja na maabara.

Afya:
Mhe. Spika, Sekta ya Afya inaendelea kuimarika ambapo kwa mwaka 2010/2011, jumla ya wafanyakazi 76 wakiwemo wanaume 44 na wanawake 32 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kuhusiana na masuala mbali mbali ya afya. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu kama vile ujenzi wa vituo vya afya ambavyo vinasaidia sana katika kutoa huduma. Jitihada kadhaa zimeendelea kuchukuliwa katika kuhakikisha kuwa dawa muhimu zinapatikana pamoja na vifaa vya matibabu vinavyokidhi haja. Vile vile ujenzi wa majengo matatu katika Chuo cha Afya Mbweni umeanza. Ujenzi wa nyumba 20 za wafanyakazi Pemba umekamilika na kukabidhiwa kwa wahusika.

Halikadhalika huduma za kujifungua katika vituo vya afya zimeongezeka na jamii imehamasishwa kutumia njia za uzazi wa mpango. Vile vile, Serikali imeendelea na juhudi zake za kuhakikisha kuwa maradhi ya malaria yanaondoka kabisa Zanzibar. Elimu ya afya imeendelea kutolewa kwa maradhi yakuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Utoaji huo wa elimu umesaidia sana kwa wananchi kufahamu sababu kuu zinazosababisha maradhi hayo na hivyo kuanza kuchukua tahadhari.

Maji:
Mhe. Spika, kutokana na matokeo ya Utafiti wa Matumizi na Mapato ya Kaya, usambazaji wa mabomba kwa ajili ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi umefikia asilimia 89.4 mwaka 2009/2010, ingawa upatikanaji wa maji bado unaendelea kuwa ni changamoto kubwa kwa

Zanzibar na zaidi katika maeneo ya mjini ikilinganishwa na vijijini ambapo viwango vya matumizi ya maji vimeongezeka kutoka asilimia 80.6 mwaka 2004/2005 hadi 85.9 mwaka 2009/2010 katika maeneo ya vijijini.

Mhe. Spika, utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa uhuishaji na upanuzi wa shughuli za maji Mkoa Mjini Magharibi umekamilika kwa kujenga matangi makubwa mawili, Dole na Kinuni na kuchimba visima vitano pamoja na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 21.

Mafanikio ya mradi huu hayajaonekana sana kwa baadhi ya maeneo ya mjini kutokana na uchakavu uliopo wa mabomba na kusababisha maji mengi kupotea ardhini kabla ya kuwafikia watumiaji. Serikali inaendelea na jitihada za kurekebisha hali hiyo. Hata hivyo, tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama ni kubwa. Jumla ya dola za Kimarekani 123 milioni zinahitajika ili kuondokana na tatizo lililopo kwa ajili ya kuchimba visima zaidi, kununulia mabomba na pampu pamoja na kujenga matangi ya ziada. Serikali kwa kuona uzito wa tatizo hilo, upatikanaji wa maji safi na salama umepewa kipaumbele.

Vijana, Wanawake na Watoto:
Mhe. Spika, Serikali imezindua Mfuko wa Vijana unaoendeshwa na Shirika la *UN-Habitat* unaogharimiwa na Serikali ya Norway ambao una lengo la kuwaendeleza vijana kiuchumi. Mfuko huo umetengewa jumla ya TZS 149 milioni. Aidha, mikutano ya kuwaelimisha vijana wa Zanzibar juu ya utaratibu na masharti ya kupata fedha kwenye mfumo huo tayari imeshafanyika Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, mafunzo ya haki za watoto yametolewa kwa Baraza la Watoto yakiwa na lengo la kutoa fursa kwa watoto kujua haki zao na kuweza kutoa taaluma ya haki hizo kwa watoto wenzao ndani ya jamii. Vile vile, Sheria ya Mtoto imeshapitishwa na Baraza lako tukufu na uratibu wa mafunzo ya kuwasilisha ujumbe wa haki za watoto kwa watendaji wa shughuli za watoto umeshaandaliwa. Aidha, kituo cha *One Stop Centre* kimeanzishwa kikiwa na lengo la kuratibu shughuli zote za udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Kituo hicho kipo Hospitali ya Mnazi Mmoja (Unguja) na vile vile Chake Chake (Pemba).

Vituo hivyo vitajumuisha watendaji kutoka Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Jeshi la Polisi, Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Madaktari. Lengo la kuanzishwa vituo hivyo ni kurahisisha ufuatiliaji wa kesi na matukio ya udhalilishaji wa kijinsia. Kadhalika, kumejitokeza vitendo vya ubakaji ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar na hali hii imefikia kutisha. Serikali itafanya kila

liwezalo katika kuhakikisha kuwa vitendo vya ubakaji vinakomeshwa na kufikiwa mwisho.

Klasta ya III: **Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa:**
Mhe. Spika, Klasta ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa ni klasta ya tatu, kwa 2010/2011 ilipangiwa kutekeleza programu tano na miradi 30 ya maendeleo na ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 25.89 bilioni sawa na asilimia 10.3 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Serikali ilitenga TZS 13.27 bilioni sawa na asilimia 51.2 ya bajeti na Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia jumla ya TZS 12.26 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 48.8 ya bajeti ya klasta hii.

Mhe. Spika, kuanzia Julai, 2010 hadi Machi, 2011, TZS 10.1 bilioni sawa na asilimia 39 ya Bajeti ya Maendeleo kwa klasta ya tatu zimetolewa. Kati ya fedha hizo, Serikali imetoa TZS 6.5 bilioni sawa na asilimia 49.2 na Washirika wa Maendeleo wamechangia TZS 3.6 bilioni sawa na asilimia 28.6.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi katika klasta hii kwa baadhi ya sekta ni kama ifuatavyo:

Utawala:
Mhe. Spika, Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi ili kuongeza ufanisi na tija katika maendeleo ya nchi. Kwa mwaka 2010/2011, Serikali imeendelea na ujenzi wa baadhi ya ofisi na sasa zimo katika hatua za kukamilika. Ofisi zenyewe ni Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini (Unguja), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini (Unguja), Ofisi ya Makao Makuu ya Valantia, ujenzi wa Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria kinachojengwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka n.k. Aidha, ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umekamilika.

Utawala Bora:
Mhe. Spika, Serikali imeendelea na kuwashajihisha watendaji wa Serikali kuongeza uelewa wa Sheria ya Fedha za Umma, Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali na Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, mafunzo ya msingi ya *"Risk Based Audit"* yametolewa kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuweza kuhakiki maeneo ya upotevu wa mapato ya Serikali na kutambua maeneo hatarishi ya matumizi ya fedha yanayofanywa kinyume na utaratibu. Pia watendaji hao wanapatiwa mafunzo ya ukaguzi wa mbinu za kisasa unaofanywa duniani yakiwemo ukaguzi wa thamani, ukaguzi wa kutumia kompyuta na ukaguzi wa mazingira. Serikali itaendelea kuwapatia mafunzo watumishi wake kwa lengo la kubadilika katika utekelezaji wa majukumu yao.

Maafa:
Mhe. Spika, Serikali imeendelea pia kujenga uwezo wa Zanzibar katika kujiandaa na kukabiliana na maafa. Rasimu ya Sera ya kukabiliana na maafa imeanza kujadiliwa na wadau ikiwemo Kamati za Kukabiliana na Maafa za Mikoani na Wilaya ili kupata maoni ya kuimarisha sera hiyo. Pia vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya wakati wa hali ya dharura vimepatikana yakiwemo mahema, vifaa vya huduma ya kwanza, maturubali na mablanketi. Ni muhimu kwa Serikali na jamii kwa ujumla wake kujitayarisha katika kukabiliana na maafa. Serikali imejipanga kutoa kila msukumo katika eneo hili.

Sheria:
Mhe. Spika, Sekta ya Sheria ni muhimu sana katika kusimamia haki, usawa, kuleta ustawi na ufanisi katika jamii. Serikali kupitia Sekta hii imezichapisha Sheria za Zanzibar kuanzia mwaka 1980 hadi 2010 ambapo jumla ya juzuu (*volumes*) 15 zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau, sambamba na uchapishaji wa nakala zisizopungua elfu tatu (3,000) za Katiba ya Zanzibar na kusambazwa kwa taasisi mbali mbali za Serikali, Mashirika na Taasisi Binafsi. Aidha, katika kuendelea na mageuzi ya kuingia na kutoka katika biashara, Serikali imepitisha Sheria ya Usajili wa Mikataba ya Mali isiyohamishika. Kwa hatua hizi zinazochukuliwa na Serikali, wananchi nao hawana budi kuzifahamu sheria zinazosimamia maslahi yao na nchi yao. Imebainika wananchi wengi hufanya makosa kwa kisingizio cha kutokuijua sheria.

Habari:
Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali ilikusudia kubadilisha Sekta ya Utangazaji na kuwa na mfumo wa mitambo ya kisasa ya *digital* na kuondokana na mfumo wa zamani wa urushaji wa matangazo wa *analog*. Baadhi ya mitambo ya mfumo mpya wa *digital* imeshawasili hapa nchini na Serikali imo mbioni kuunganisha mitambo hiyo. Zanzibar tukiwa ni sehemu ya dunia, hatuwezi kuwa nyuma katika matumizi ya mfumo mpya wa *digital*.

MASUALA YA MTAMBUKA

Mhe. Spika, masuala ya MTAMBUKA ni miongoni mwa masuala yanayostahiki kupewa umuhimu katika utayarishaji wa Sera na Mipango. Masuala hayo yanajumuisha mazingira, jinsia, idadi ya watu, maafa, utawala bora na ukimwi. Ili kuyapa msukumo unaostahiki, masuala ya usimamizi wa mazingira, ukimwi na ulemavu yamewekwa chini ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Ni dhahiri kuwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii yanategemea kuwepo kwa Mpango madhubuti wa kusimamia matumizi bora ya ardhi na mazingira. Kukua kwa kasi kwa idadi ya watu kunachangia sana uharibifu wa mazingira yanayowazunguka, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Katika kukabiliana na athari hizo utayarishaji wa Kanuni za Tathmini za Athari ya Mazingira na Maliasili zisizorejesheka uko katika hatua za mwisho kukamilika. Kukua kwa idadi ya watu ni changamoto kubwa Zanzibar ambapo juhudi za makusudi zinahitajika kwa ajili ya kutunza afya ya mzazi. Aidha, elimu inahitajika kwa vijana hususan watoto wa kike. Vile vile, kuongezeka kwa harakati za maendeleo katika ukanda wa pwani, changamoto mbali mbali zimejitokeza zikiwemo kuharibiwa kwa mazalio ya kasa na samaki, ukataji wa miti kwa matumizi ya kupikia na kujengea, njia duni za uvuvi, uchimbaji wa mawe na mchanga.

Mhe. Spika, Katika mikakati ya utunzaji wa mazingira, Serikali katika mwaka 2010/2011 iliweza kutoa elimu kwa jamii na wawekezaji nchini kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na mwenendo mzima wa mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Jumla ya miradi 36 ya uwekezaji ilifanyiwa mapitio na kutolewa ushauri wa kimazingira. Aidha, miradi 14 imefanyiwa tathmini za athari za kimazingira katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Vile vile Serikali inaendelea kusimamia amri ya upigaji marufuku uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plastiki ikiwemo kutoa elimu kwa wadau mbali mbali kuhusu athari za matumizi ya mifuko hiyo. Kwa upande mwengine, hatua maalum zinaendelea kuchukuliwa kwa kuangamiza kunguru weusi ambao wamebainika kuwa na athari kubwa kwa mazingira na jamii. Kadhalika, Serikali itahakikisha kuwa inawatafutia vijana na wananchi kwa ujumla njia mbadala za kuendesha maisha yao, badala ya uharibifu wa mazingira kama ndio njia ya kuendesha maisha.

Mhe. Spika, Masuala ya Kijinsia yanachukua nafasi yake katika mipango ya maendeleo nchini. Kamati imeundwa ya kushughulikia vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar na inasimamiwa na Kamishna wa Polisi Zanzibar akishirikiana na Wizara ya Ustawi wa jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Aidha, Mpango Mkakati wa kupiga vita udhalilishaji wa kijinsia na Sera ya Uadilifu wa kijinsia zipo katika hatua za mwisho kukamilika.

Mhe. Spika, Kuhusu mapambano dhidi ya ukimwi, Serikali inaendelea na utayarishaji wa Mkakati wa Pili wa Kupambana na UKIMWI ambao unajumuisha mashauriano ya kina kwa makundi mbalimbali katika jamii. Mkakati huo umejikita zaidi kutoa kipaumbele kwa makundi hatarishi kama vile wanawake wanaojihusisha na biashara ya ngono, watumiaji wa dawa za kulevya na watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja..

Mhe. Spika, Mwaka 2010/2011 katika juhudi za kutoa elimu ya UKIMWI kwa jamii, Serikali kwa kutumia vyombo vya habari, vipindi mbali mbali vipatavyo 720 vya kuwaelimisha wananchi vimerushwa hewani. Lengo nikuwaelimisha

wananchi katika kujikinga na UKIMWI. Vyombo vya habari vilivyotumika kwa kurushia vipindi hivyo ni Sauti ya Tanzania Zanzibar, Micheweni *Community Redio, Annur Zenj FM* pamoja na *Hits FM*. Hata hivyo, licha ya juhudi hizo baadhi ya maeneo maambukizi ya UKIMWI yameonekana kuongezeka ukilinganisha na miaka ya nyuma. Hali hii ni hatari na iko haja ya kufanya uchunguzi zaidi ili kuelewa sababu za msingi.

KUIMARISHA MUUNGANO

Mhe. Spika, katika juhudi za kuimarisha Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia vikao mbali mbali vya Watendaji, Mawaziri, Vikao vya Waziri Mkuu, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar (zamani Waziri Kiongozi) vinavyoongozwa na Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, juhudi mbali mbali zimechukuliwa za kuzipatia ufumbuzi baadhi ya kero za Muungano.

Mhe. Spika, tokea kuanza kwa vikao hivyo mwaka 2006 jumla ya vikao 6 vya Mhe. Waziri Mkuu na Mhe. Waziri Kiongozi/Makamu wa Pili wa Rais vimefanyika na jumla ya masuala (Kero) 7 yamepatiwa ufumbuzi. Hata hivyo, mazungumzo ya kutafuta ufumbuzi wa masuala (Kero) nyengine yanaendelea. Kwa upande wa Tume ya Pamoja ya Fedha, Serikali itaendelea na juhudi za kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa mapendekezo ya juu ya Taarifa ya Tume hiyo yaliyowasilishwa katika Serikali zetu mbili.

Mhe. Spika, katika suala la kuimarisha na kuibua vyanzo vipya vya mapato, Serikali inaendelea na juhudi za maandalizi ya uchimbaji wa mafuta na gesi kwa upande wa Zanzibar. Kufuatia maamuzi yaliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimae kupitishwa na Baraza lako tukufu juu ya kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia katika orodha ya Mambo ya Muungano, Serikali ya awamu ya saba itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kulipatia ufumbuzi wa pamoja wa kulitoa suala la mafuta katika orodha ya mambo ya Muungano.

UTEKELEZAJI WA BAJETI 2010/11

Mapato ya Ndani:
Mhe. Spika, kufuatia kuimarika kwa uwekezaji nchini, mapato ya Serikali yamekuwa yakiongezeka kutoka TZS 62.4 bilioni mwaka 2005/2006 hadi TZS 149.5 bilioni mwaka 2009/2010. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 139.6 katika kipindi hicho.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa ya awali ya mwaka wa fedha 2010/11, jumla ya mapato yaliokusanywa yalifikia TZS 132.96 bilioni sawa na asilimia 100.9 ya makadirio ya kipindi hicho. Ikilinganishwa na mwaka uliopita (2009/2010) katika kipindi kama hicho, kunajitokeza ukuaji wa mapato kwa asilimia 16.7. Kati ya makusanyo hayo jumla ya TZS 126.10 bilioni zilitokana na mapato ya kodi ambazo ni sawa na asilimia 89.1 ya makadirio (sawa na ukuaji wa asilimia 16.8 kulinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2009/2010). Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 6.86 bilioni sawa na asilimia 87 ya makusanyo ya kipindi hicho.

Mhe. Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato kitaasisi, katika miezi tisa ya kwanza ya mwaka 2010/11, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya jumla ya TZS 55.73 bilioni sawa na asilimia 108 ya makadirio ya kipindi hicho. Ukuaji huo ni asilimia 27.2 ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita. Bodi ya Mapato ya Zanzibar kwa kipindi cha Julai – Machi 2010/2011 nayo imekusanya jumla ya TZS 77.23 bilioni sawa na asilimia 96.3 ya makadirio ya miezi tisa, sawa na ukuaji wa asilimia 10.14 kwa mwaka uliopita katika kipindi kama hicho.

Mhe. Spika, mapato yasiyokuwa ya kodi kutoka katika Wizara za Serikali yameendelea kuwa madogo, jumla ya TZS 6.88 bilioni zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 87 ya makadirio ya miezi tisa ya awali. Hali hii imetokana zaidi na viwango vya kutozea ada kuwa vidogo pamoja na baadhi ya sheria zetu kutoa mwanya kwa Waziri wa sekta kusamehe kodi. Serikali katika juhudi zake za kuongeza mapato hasa yale ya mawizara yakiwemo ya ardhí inaandaa utaratibu wa kurekebisha kasoro hizo.

Mapato ya Nje:
Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepokea Misaada ya Kibajeti (4.5%) yenye thamani ya TZS 33.89 bilioni hadi Machi, 2011 ambazo ni sawa na asilimia 60 ya makadirio ya mwaka wa fedha 2010/2011, ya TZS 55.24 bilioni. Aidha, Ruzuku na Mikopo iliyopokelewa kwa ajili ya Miradi na Programu za Maendeleo imefikia TZS 117.72 bilioni sawa na asilimia 56 ya matarajio ya mwaka ya TZS 211.71 bilioni. Hali hii inatufanya tuongeze nguvu zaidi katika kujitegemea kimapato hasa kwa kuangalia fursa zilizopo.

MATUMIZI

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya Serikali ni dhahiri yatakuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha tathmini (Julai, 2010 hadi Machi, 2011), matumizi halisi ya Serikali yalifikia TZS 256.48 bilioni sawa na asilimia 76.9 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi kwa ajili ya

kazi za kawaida yalifikia TZS 138.76 bilioni sawa na asilimia 95.7 ya makadirio, wakati yale ya kazi za maendeleo yalifikia TZS 142.23 bilioni sawa na asilimia 75.5 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya matumizi hayo ya kazi za maendeleo, TZS 24.51 bilioni zilikuwa ni fedha za ndani na TZS 117.72 bilioni ni fedha za kigeni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, muundo mpya wa kiwizara ulioanza mwezi wa Januari 2011 baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2010, hakukubadilisha kiwango cha bajeti ya Serikali iliyokadiriwa kwa mwaka 2010/2012. Wizara pamoja na Idara mpya zilizojichomoza ziligawiwa sehemu ya bajeti kutoka katika bajeti iliyopitishwa na Baraza lako tukufu.

Matumizi ya Kazi za Kawaida 2010/2011:
Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa cha mwaka 2010/2011, matumizi ya kazi za kawaida yalifikia TZS 138.76 bilioni. Matumizi hayo ni sawa na asilimia 95.7 ya makadirio. Ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita, matumizi ya kazi za kawaida yameongezeka kwa TZS 23.9 bilioni sawa na asilimia 20.8 ambapo jumla ya TZS 114.83 bilioni zilitumika. Kati ya matumizi hayo ya kazi za kawaida, TZS 62.86 bilioni zilitumika kwa ajili ya mishahara, TZS 56.79 bilioni ni matumizi mengineyo na TZS 19.11 bilioni ni ruzuku kwa taasisi mbali mbali za Serikali.

Mishahara:
Mhe. Spika, TZS 62.86 bilioni zilitumika kwa ajili ya kulipia mishahara kwa watumishi wa Serikali katika kipindi cha miezi tisa, sawa na asilimia 101.6 ya makadirio ya kipindi hicho na ni asilimia 45.3 ya matumizi yote ya kazi za kawaida. Aidha, matumizi hayo ya mshahara ni sawa na asilimia 47.3 ya makusanyo ya ndani.

Ruzuku:
Mhe. Spika, uchambuzi wa matumizi unaonesha kwamba katika miezi tisa ya mwaka 2010/11 Serikali imetumia TZS 19.11 bilioni ikiwa ni ruzuku kwa Taasisi mbali mbali za Serikali. Matumizi hayo ni sawa na asilimia 94.9 ya makadirio ya kipindi hicho. Kwa kulinganisha na matumizi halisi katika kipindi kama hicho mwaka 2009/10, kiasi hicho cha ruzuku kinaonesha ukuaji wa asilimia 23.1. Kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha ruzuku, Serikali inajipanga kuzifanyia mapitio taasisi zote zinazopata ruzuku, lengo ni kuzijengea uwezo, ili baadae ziweze kujitegemea zaidi na hatimae kupunguwa kwa kiwango cha ruzuku kinachokwenda katika taasisi hizo.

Mfuko Mkuu wa Serikali na Mengineyo:
Mhe. Spika, matumizi katika Mfuko Mkuu wa Serikali katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2010/11 yalifikia TZS 26.97 bilioni ambazo ni sawa na

asilimia 79.9 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi mengineyo yaliyotumika kuendesha shughuli mbali mbali za Serikali yalifikia TZS 29.82 bilioni katika kipindi cha tathmini ambayo ni sawa na asilimia 48.1 ya makadirio katika kipindi hicho. Ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2009/2010 matumizi yameongezeka kwa TZS 4.23 bilioni sawa na asilimia 14 ambapo TZS 25.59 bilioni zilitumika katika kipindi kama hicho.

DENI LA TAIFA

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi ya mwaka wa fedha 2010/2011 malipo ya marejesho ya mikopo ya ndani yalifikia TZS 1.76 bilioni sawa na asilimia 29.3 ya makadirio katika kipindi hicho. Ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2009/2010 marejesho hayo yalifikia TZS 1.99 bilioni sawa na asilimia 55.5 ya makadirio. Kupungua kwa malipo hayo kwa mwaka 2010/2011 kumesababishwa na kuwa marejesho mengi yalitarajiwa kufanyika katika robo ya mwisho ya mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, malipo ya riba ya madeni ya ndani kwa mwaka wa fedha 2010/2011 hadi kufikia Machi, 2011 yalikuwa TZS 1.18 bilioni sawa na asilimia 84.4 ya makadirio kwa kipindi hicho ikilinganishwa na mwaka 2009/2010, hadi kufikia Machi, 2010 malipo yalikuwa TZS 1.27 bilioni sawa na asilimia 95.5 ya makadirio ya kipindi hicho.

Mhe. Spika, malipo hayo ya riba kwa mwaka 2010/2011 yamepungua kwa TZS 0.09 bilioni au asilimia 7.6 ikilinganishwa na mwaka 2009/2010.

MALIPO YA KIINUA MGONGO

Mhe. Spika, Serikali imekuwa ikichukua juhudi za kuhakikisha kuwa wastaafu wanalipwa haki zao kwa wakati. Katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011, jumla ya wastaafu 748 kati ya wastaafu 1,045 Unguja na Pemba waliripotiwa kulipwa haki zao. Jumla ya TZS 5.18 bilioni zimetumika kwa kuwalipa wastaafu hao kiinua mgongo.

Utekelezaji wa Hatua za Kuimarisha Mapato:
Mhe. Spika, katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2010/2011, Serikali ilichukua hatua maalum ya kupunguza misamaha ya kodi, ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kuangalia mianya iliyopo na kufuatilia kwa karibu na kufanya uchambuzi wa kina juu ya maombi ya misamaha. Hatua hizo zimeonesha matunda mazuri, kwani misamaha ya kodi imepungua kutoka TZS 21.02 bilioni mwaka 2009/2010 na kufikia TZS 14.76 bilioni mwaka 2010/2011 sawa na ushukaji wa asilimia 29.8. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbali mbali kwa nia ya kuimarisha mapato ya Serikali.

UTAYARISHAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASIKINI ZANZIBAR (MKUZA II) NA MAPITIO YA DIRA 2020

Mhe. Spika, kufuatia kukamilika utekelezaji wa MKUZA awamu ya kwanza, Serikali imekamilisha utayarishaji wa awamu ya pili ya MKUZA. Mwelekeo wa MKUZA awamu ya pili ni kama ifuatavyo:

i) Kuendelea kuwa na Klasta tatu; Klasta ya Kwanza ni Ukuzaji Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato yenye malengo manne; Klasta ya pili ni Huduma za Jamii na Ustawi yenye malengo saba; na Klasta ya tatu ni Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa yenye malengo matatu.

ii) Katika kuendeleza Sekta Binafsi nchini, lengo maalum limewekwa katika Klasta ya kwanza.

iii) Klasta ya pili kuendelea kubeba malengo mengi zaidi.

iv) Utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi Zanzibar unaendelea kuwa na umuhimu katika MKUZA II.

v) Mashirikiano ya Sekta za Umma na za Binafsi yamepewa msisitizo zaidi kwa dhamira ya kuleta ufanisi.

vi) Mageuzi ya Msingi *(Core Reform)* yanahitaji kuendelezwa kwa kasi zaidi. Ufuatiliaji na tathmini utaimarishwa zaidi kutokana na uzoefu uliopatikana baada ya mapitio ya MKUZA I.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo kabla, kufuatia kufikia nusu ya kipindi cha utekelezaji, Serikali imefanya mapitio ya Dira 2020 na sasa iko katika hatua za kukamilisha taarifa ya mapitio hayo. Mategemeo ni kuwa mapendekezo ya taarifa hiyo yatasaidia kuimarisha mikakati yetu ya kujiletea maendeleo nchini kwa kipindi kilichobakia ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI, MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI MWAKA 2011/12

Mwelekeo wa Hali ya Uchumi:

Mhe. Spika, uchumi wa dunia unaendelea kukua lakini kwa kasi ndogo, hali hii imetokana na msukosuko wa uchumi na fedha ulioikumba dunia katika miaka miwili ya 2008 na 2009 iliyopita. Uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.4 kwa mwaka 2011. Ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea unatarajiwa kufikia asilimia 2.5 wakati nchi zinazoendelea na zilizo chini kiuchumi zinatarajiwa kukua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 6.5 kwa mwaka 2011. Vile vile, nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara zinaendelea kurejea katika hali ya kawaida kutoka katika msukosuko wa kiuchumi na fedha, huku kukiwa na matarajio ya ukuaji wa uchumi wa asilimia

5.5 kwa mwaka 2011. Taarifa hizi ni kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Uchumi wa Dunia ya Shirika la Fedha Duniani.

Mhe. Spika, athari ya kushuka kwa biashara katika soko la dunia na kupanda kwa kiwango cha ukosefu wa ajira ni changamoto kubwa kwa nchi mbali mbali duniani. Ukuaji wa biashara kati ya nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara na nchi za Asia umechukua nafasi kubwa ya kurudisha hali ya uzalishaji na ukuaji wa uchumi katika nchi hizi, ingawa tatizo la ajira litaendelea kudumu kwa kipindi kifupi kijacho.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011 mfumko wa bei duniani unatarajiwa kupanda hadi kufikia wastani wa asilimia 2.0. Bei za bidhaa mbali mbali zikiwemo za chakula na mafuta zimeonekana kuongezeka kuanzia mwishoni mwa mwaka 2010. Hali hii inatarajiwa kuendelea kwa mwaka 2011 kutokana na kasi ya ukuaji wa mahitaji na kupungua kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa kuliko mahitaji ya soko. Matatizo ya kijamii na kisiasa yanayoendelea katika nchi kadhaa za Afrika ya Kaskazini na Mashariki ya Kati, ambazo ndio wazalishaji wakubwa wa mafuta nayo yanachangia katika utete wa bei ya mafuta duniani.

Mhe. Spika, robo ya mwanzo ya mwaka 2011, bei za mafuta zimepanda kufikia wastani wa Dola 90 za Kimarekani kwa pipa ikilinganishwa na Dola 79 kwa pipa iliofikiwa mwezi wa Oktoba mwaka 2010. Bei hizo zinaonekana pia kusababisha kuongezeka kwa bei ya bidhaa mbali mbali duniani kwa asilimia 12 kwa mwaka 2011. Bei za mafuta zinatarajiwa kuongezeka zaidi hadi kufikia Dola 100 kwa pipa kwa mwaka 2012. Aidha, dalili za kuongezeka kwa madeni na kupanda kwa bei za rasilimali zimeanza kujitokeza katika nchi mbali mbali duniani.

Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar, mwaka 2011/12, mwelekeo wa hali ya uchumi unategemea zaidi utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II), Malengo ya Milenia ya mwaka 2015, Mageuzi ya Msingi pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/12, Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa kasi zaidi kutoka ukuaji wa asilimia 6.5 hadi kufikia asilimia 7.9. Kutokana na athari za mabadiliko ya bei za chakula na mafuta ya nishati duniani, kasi ya Mfumko wa bei inatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 6.1 mwaka 2010 hadi asilimia 7. Serikali inaendelea kuchukua juhudi za makusudi za kuongeza uzalishaji wa chakula na hasa zao la mpunga wa kumwagilia maji, ili kupunguza kiwango cha uagiziaji wa bidhaa hiyo kutoka nje.

Aidha, matarajio ya kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa yanatokana na mategemeo ya matokeo ya kuimarika kwa miundombinu ya kiuchumi kama vile uwanja wa ndege, barabara, umeme na mfumo wa umwagiliaji maji pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji. Juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani zinatarajiwa kuongeza kigavi cha mapato ya ndani kwa Pato la Taifa na kufikia asilimia 20.2 kutoka asilimia 18 ya mwaka 2010/11.

Mhe. Spika, Serikali imeazimia kujenga mazingira ya kiuchumi ambayo yatawezesha maeneo yafuatayo:

- Kuimarika kwa rasilimali watu, kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi na kuinua kiwango cha sayansi, teknolojia na mafunzo ya vitendo.
- Kuimarisha kwa sekta ya fedha kwa lengo la kuchangia na kujenga ukuaji uchumi ambao utategemea utekelezaji wa awamu ya pili ya Mageuzi ya Sekta ya Fedha.
- Kutekeleza Mkakati wa Usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.
- Kuimarika kwa miundombinu ya kiuchumi na
- Sera za kodi na fedha ambazo zitatekeleza mageuzi ya mfumo wa kodi katika sekta mbali mbali.

MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI KWA MWAKA 2011/12

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/12, Serikali inataraji kutekeleza jumla ya programu 27 (kati ya hizo saba ni mpya) na miradi ya maendeleo 77 (kati yake 11 ni mipya) yenye gharama ya jumla ya TZS 378.90 bilioni. Kati ya fedha hizi, Serikali itatoa TZS 37.95 bilioni sawa na asilimia 10 na Washirika wa Maendeleo watachangia TZS 340.96 bilioni sawa na asilimia 90. Kati ya fedha hizo za washirika wa maendeleo ruzuku ni TZS 124.96 bilioni na mikopo ni TZS 216 bilioni.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi kwa kila klasta ni kama ifuatavyo: Klasta ya Ukuzaji wa Uchumi na Upunguzaji wa Umasikini inatarajiwa kutekeleza jumla ya programu 17 (kati yake tano ni mpya) na miradi 17 (mmoja ni mpya) katika mwaka 2011/2012 kwa gharama ya TZS 183.23 bilioni. Kati ya hizo Serikali itatoa TZS 15.76 bilioni sawa na asilimia 8.6 na Washirika wa Maendeleo watachangia TZS 167.48 bilioni sawa na asilimia 91.4.

Mhe. Spika, Klasta ya Uimarishaji wa Huduma za Jamii, inatarajiwa kutekeleza jumla ya programu sita (kati yake moja ni mpya) na miradi 33 (kati yake mitano ni mipya) katika mwaka 2011/2012 kwa gharama ya TZS 151.52

bilioni. Kati ya hizo Serikali itatoa TZS 12.89 bilioni sawa na asilimia 8.5 na Washirika wa Maendeleo TZS 138.63 bilioni sawa na asilimia 91.5.

Mhe. Spika, Klasta ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa inatarajiwa kutekeleza jumla ya programu 4 (moja mpya) na miradi 27 (kati yake mitano mipya) katika mwaka 2011/2012, kwa gharama ya TZS 44.15 bilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali itatoa TZS 9.30 bilioni sawa na asilimia 21.0 na Washirika wa Maendeleo watachangia TZS 34.85 bilioni sawa na asilimia 79.0.

Mhe. Spika, Maeneo makubwa ambayo programu na miradi hiyo itashughulikiwa ni kama ifuatavyo**:**

KUIMARISHA SEKTA YA UMMA

Mhe. Spika, Serikali imedhamiria kuimarisha utendaji wa sekta ya umma ili kuongeza ufanisi wa kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi. Ili kutimiza dhamira hiyo, Serikali itatekeleza Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Umma itayohusisha maeneo ya kuimarisha miundo ya taasisi, watumishi, uwekaji wa kumbumbu na Mageuzi ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, kuhusu marekebisho ya mfumo wa Serikali za Mitaa, dhamira ya Serikali ni kupeleka madaraka na huduma karibu zaidi na wananchi. Lengo ni kuharakisha ustawi wa maisha kwa kuzingatia masuala muhimu kwenye maeneo. Juhudi hizi zinakwenda sambamba na misingi ya kuimarisha Demokrasia na kujali vipaumbele na rasilimali zilizomo ndani ya maeneo ya wananchi.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2011/12, Sheria ya Mamlaka ya Utawala wa Mikoa itapitiwa na kufanyiwa marekebisho. Maeneo mengine yatakayofanyiwa kazi ni pamoja na haya yafuatayo:-

a) Kufanya mapitio katika muundo wa kitaasisi;
b) Kufanya mapitio ya Sheria Nam. 3 na 4 ya mwaka 1995 za Serikali za Mitaa;
c) Muundo wa Utumishi na;
d) Kujenga uwezo wa rasilimaliwatu pamoja na fedha.

Mhe. Spika, sambamba na marekebisho hayo ya kisheria na kitaasisi, Serikali pia inatarajia kuchukua hatua maalum za kujenga uwezo wa Baraza la Manispaa na Halmashauri za Mji wa Mkoani, Chake Chake na Wete Pemba ili kuiwezesha kutoa huduma bora zaidi na kuimarisha usafi wa mazingira ya makaazi katika miji hiyo. Kazi hii itafanyika kupitia utekelezaji wa Mpango wa Kuimarisha Huduma za Mijini (*Zanzibar Urban Service Programme - ZUSP*) utakaogharimu jumla ya Dola za Kimarekani 38 milioni sawa na TZS

58.0 bilioni. Kati ya fedha hizo, jumla ya Dola za Kimarekani 31.2 milioni zitatumika kwa ajili ya Manispaa ya Unguja, Dola za Kimarekani 3.8 milioni kwa miji mitatu ya Pemba na Dola za Kimarekani 3.0 milioni kwa kazi za kiutawala. Aidha, mradi huo unalenga kutekeleza mambo makubwa yafuatayo:

i) Ukarabati na Ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua katika maeneo ya Manispaa ya Unguja yenye jumla ya urefu wa Kilomita 19.6. Maeneo yatakayonufaika na mradi huu ni ziwa la Sebleni, ziwa la kwa Mtumwa Jeni, ziwa la Binti Amrani, ziwa la Mwantenga, Kwamtipura, Kilima hewa, Karakana, Sogea, Mpendae, Jang'ombe (*Botanical garden*), Uwanja wa demokrasia na Shauri moyo.

ii) Uimarishaji wa huduma za ukusanyaji wa taka mjini kwa kupatiwa magari tisa, vikapu vya taka (*skip*) 193 na ndoo za taka (*dust bin*).

iii) Ukarabati na uwekaji wa taa za barabarani katika njia kuu za mjini kama ya Ikulu hadi Uwanja wa Ndege, Kiembesamaki hadi Amani, Amani hadi Mwembeladu, Magomeni hadi Kariakoo, Kinazini hadi Magereza, *Creek road* Kinazini hadi Bububu, katika maeneo ya Mji Mkongwe ikiwemo Kiponda, Vuga, Malindi na Shangani n.k.

iv) Kulipa uwezo Baraza la Manispaa katika mbinu za kukuza mapato, mafunzo ya wafanyakazi na utoaji wa huduma bora (*ZMC Institutional Strengthening)*

v) Ujenzi na utanuzi wa ukuta wa Forodhani ili kuweza kutumika kwa waendao kwa miguu kutoka Msikiti wa Ijumaa Malindi hadi Bustani ya Forodhani wenye urefu wa mita 340.

vi) Kuinua uwezo wa Mabaraza ya Miji mitatu ya Pemba (*Institutional Strengthening*) yaani Mkoani, Wete na Chake Chake.

vii) Kutekeleza miradi midogo midogo ya ujenzi ikiwemo ununuzi wa magari kwa ajili ya huduma.

Mhe. Spika, Kwa dhamira hiyo hiyo ya kuimarisha ufanisi Serikalini, Serikali inakusudia kutekeleza Mradi wa Mfumo wa kompyuta Serikalini (e-*government*) unaotarajiwa kugharimu TZS 30 bilioni kupitia mkopo nafuu kutoka Serikali ya Watu wa China. Utakapokamilika, Mradi huu utarahisisha sana mawasiliano Serikalini na kupunguza gharama za mawasiliano.

Aidha, inatazamiwa kwamba Mradi utakuwa chanzo kipya cha mapato ya Serikali kutokana na mauzo ya uwezo wa ziada kwa makampuni ya simu nchini.

UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

Mhe. Spika, Serikali ya awamu ya saba imetoa msisitizo maalumu katika kuwawezesha wananchi kiuchumi. Haya yamedhihirishwa na kauli mbali mbali za Mheshimiwa Rais, Dr Ali Mohamed Shein, kama vile katika uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi na katika kilele cha maadhimisho ya Sherehe za miaka 47 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Nia hii ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inaendana na Dira ya Maendeleo ya 2020 na MKUZA II. Programu mpya ya kuimarisha Miundombinu ya Soko, Kuongeza Thamani na Misaada Vijijini itatekelezwa katika mwaka 2011/12. Programu nyengine zitakazotekelezwa ni utafiti wa kilimo na mali asili, Programu ya umwagiliaji maji na Programu ya kuendeleza miundombinu ya ufugaji. Programu hizi zitatekelezwa kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, Utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi utaendelezwa. mifuko mbali mbali iliyopo itafanyiwa mapitio kwa nia ya kuiimarisha ili lengo la kuanzishwa kwake liweze kufikiwa kwa ufanisi zaidi. Aidha, maeneo mapya ya ukopaji yataanzishwa na kuhakikisha kuwepo kwa taratibu za mikopo zinazokuwa bora zaidi, mikopo inatolewa kwa wakati na kuimarisha huduma kwa wakopaji.

UJENZI WA RASLIMALI WATU

Mhe. Spika, maendeleo ya nchi yoyote yanategemea sana uwezo wa watu wake kielimu hususan wanaofanya kazi. Serikali inakusudia kuendelea kuimarisha utaalamu nchini kwa lengo la kuimarisha tija katika shughuli za kiuchumi na za uzalishaji. Programu na miradi mbali mbali ya elimu itatekelezwa ikiwemo Mradi wa Upanuzi na Uimarishaji wa Huduma za Maktaba, Mradi wa Uimarishaji wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), na Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi. Miradi mingine ni pamoja na wa Chuo cha Kiislamu Micheweni Pemba, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Mali, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi na Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi.

Mhe. Spika, Ili kufanikisha suala la ubunifu kwa vijana, serikali inakusudia kukamilisha ujenzi wa madarasa manne mapya katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi Kengeja pamoja na kuipatia vifaa mbali mbali, kuendelea na ukarabati wa Taasisi ya Sayansi na Teklonojia ya Karume na kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala huko Wingwi Mtemani Pemba ikiwa ni pamoja na kukipatia samani na vifaa vya kufundishia. Vile vile, serikali itatoa mikopo kwa vikundi vya ushirika vya wanawake na kwa wahitimu kutoka vituo vya Mafunzo ya Amali ili waweze kujiajiri na kuendeleza fani walizosomea. Hii itasaidia sana kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Mhe. Spika, mkazo pia utaendelea kuwekwa katika kuimarisha elimu ya juu ili nchi iwe na wataalamu wa kutosha na kupunguza kutegemea utaalamu kutoka nje ya nchi. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Tunguu, unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2011/2012.

KUIMARISHA AFYA ZA WATU

Mhe. Spika, nia ya serikali ni kuona kuwa Zanzibar inakuwa na watu wenye afya nzuri muda wote. Serikali inachukua jitihada maalum kuhakikisha uhakika wa chakula na lishe nchini. Uzalishaji wa mazao ya kilimo na pato la mkulima ni eneo linalopewa mkazo maalumu kwa kuongezwa huduma za ugani na utafiti, kuimarisha usimamizi wa uzalishaji endelevu wa mazao ya kilimo, kuimarisha matumizi ya mbegu bora na mbolea na pembejeo nyengine za kilimo. Uzalishaji wa mpunga unaotoa chakula kikuu kwa wananchi wetu unatarajiwa kupata msukumo mpya kufuatia kupatikana mafanikio makubwa katika mbegu mpya ya NERICA ambayo imetoa matumaini mapya kwa wakulima. Serikali itaendeleza juhudi za kuimarisha uzalishaji huo wa mpunga ili hatimae usaidie uanzishwaji wa akiba maalum ya chakula ambayo inatarajiwa kuwa chachu ya kusaidia kupungua kwa mfumko wa bei nchini. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeshaanza kuzalisha kwa wingi mbegu ya *NERICA* ambayo kuota kwake haihitaji bonde. Vile vile, inaandaa utaratibu wa kulishirikisha Jeshi la Kujenga Uchumi ili nao waweze kuzalisha mbegu ya *NERICA*. Lengo ni kuisambaza kwa wakulima.

Mhe. Spika, Serikali itaendelea na juhudi zake za kukiendeleza Kituo cha Usarifu wa Mazao ya Kilimo kwa madhumuni ya kutoa mafunzo ya usarifu kwa wananchi wanaojishughulisha na uuzaji wa mazao mbali mbali, ili waweza kuongeza kipato chao na hatimae kuwapunguzia makali ya umasikini, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya usarifu wa mazao ya kilimo Zanzibar.

Mhe. Spika, moja ya eneo lililoonesha changamoto kubwa katika kuhakikisha afya za wananchi ni upatikanaji endelevu wa maji safi na salama. Serikali imeshachukua juhudi mbali mbali za kuimarisha upatikanaji wa huduma hii ya lazima kwa maisha ya mwanaadamu, lakini bado mafanikio yake yamekuwa chini ya matarajio. Sababu zinazojitokeza ni pamoja na kupungua kwa kina cha maji kutokana na ujenzi wa karibu ya vyanzo vya maji unaofanywa na wananchi, kuchakaa kwa mitandao ya mabomba ya maji, na uharibifu wa mara kwa mara wa mitambo ya kusukumia maji kutokana na matatizo ya kukatika kwa umeme.

Serikali itaendeleza juhudi zake za kuhakikisha kuwa huduma ya maji ambayo ni muhimu inapatikana kwa uhakika. Tayari serikali imeshafanya mazungumzo na nchi na wahisani mbali mbali ili waweze kusaidiana na serikali katika kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo la maji. Lengo la serikali ni kuwa ifikapo mwaka 2015, asilimia 75 ya wananchi wa vijijini na asilimia 85 wa mijini wawe wamepata maji safi na salama.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada zote zinazoweza kuchukuliwa kuepusha maradhi, licha ya malaria kupungua kwa kiwango kikubwa lakini bado wananchi wataendelea kusumbuliwa na maradhi mbali, mbali na hivyo kuna haja ya kuimarisha huduma za afya. Serikali itaendelea kutilia mkazo huduma za kinga na tiba. Serikali pia inakusudia kutekeleza Mkakati wa Afya ya Jamii. Aidha, mpango mzima wa kuifanya hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa hospitali ya rufaa, na kuanzisha mchakato wa kuzipandisha daraja hospitali za Kivunge, Makunduchi, Micheweni na Vitongoji, kuwa za Wilaya na hospitali za Wete na Abdalla Mzee kuwa za mikoa katika mwaka wa fedha 2011/2012 utapewa msukumo mkubwa.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, takwimu zinaonesha kuwa bado vifo vya mama na mtoto vimeendelea kuwa changamoto hapa nchini. Ili kurekebisha hali hii, Serikali inakusudia kuimarisha huduma za chanjo kwa mama na watoto katika vituo vyote vya huduma za mama na watoto nchini. Juhudi zinazoendelezwa za kusogeza huduma za uzazi salama karibu na wananchi nazo kwa kiwango kikubwa zinatarajiwa kupunguza vifo vya mama na watoto. Pamoja na hali ngumu ya maisha nia ya serikali ni kuhakikisha kuwa dawa muhimu zinapatikana katika hospitali na vituo vya afya wakati wote.

KUUNGANISHA WATU KIJAMII NA KIUCHUMI

Mhe. Spika, maendeleo yanahitaji kuunganishwa kwa sehemu za uzalishaji na masoko na huduma nyengine za jamii. Serikali kwa mwaka 2011/12 itaendeleza uimarishaji wa miundombinu ya mawasiliano kwa njia ya barabara, bandari na viwanja vya ndege. Kwa upande wa barabara, madaraja manne ya barabara ya Mahonda-Donge-Mkokotoni yanatarajiwa kujengwa. Aidha, barabara za Mgagadu-Kiwani, Pale-Kiongele, Amani-Mtoni, Wete-Konde, Wete-Chake, Wete-Gando, Mzambarautakao-Finya, Mzambarauzikaribu-Mapofu, Bahanasa-Daya-Mtambwe, Chwale-Kojani, Kipangani-Kangagani zinatarajiwa kukamilishwa kwa kiwango cha lami. Pia tunataraji kuanza matayarisho ya ujenzi wa barabara Ole-Kengeja. Serikali pia inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bandari mpya ya Mpigaduri.

Mhe. Spika, Kwa upande wa usafiri wa anga, ujenzi wa jengo jipya la abiria unaendelea vizuri katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani

Karume. Mazungumzo ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa maegesho (*apron*) na njia ya kupitia ndege (*taxiway*) yanaendelea. Inatarajiwa pia kuwa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba utapatiwa ufumbuzi hivi karibuni na kazi za ujenzi kuanza mapema iwezekanavyo. Uimarishaji wa njia za mawasiliano una faida kubwa kiuchumi na kijamii, hivyo serikali itahakikisha kuwa juhudi mbali mbali zinachukuliwa kufanikisha suala la mawasiliano.

UTAFITI NA MAENDELEO

Mhe. Spika, serikali kwa kuelewa umuhimu wa utafiti katika maendeleo imeamua kwa kila Wizara kuanzisha Kitengo cha Utafiti ndani ya Idara za Mipango, Sera na Utafiti. Vitengo hivi vina jukumu la kubainisha na kuratibu masuala ya utafiti pamoja na kuandaa na kusimamia mipango ya utafiti kwa pamoja na kutumia matokeo ya tafiti hizo katika mipango ya maendeleo ya sekta.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imepewa jukumu maalumu la kuratibu masuala yote ya utafiti nchini. Katika kutimiza azma hiyo, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imeshafanya mazungumzo na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTEC*) kwa ajili ya *COSTEC* kufungua ofisi yake Zanzibar na hatua za kuanzisha ofisi hiyo zinaendelea kuchukuliwa.

Mhe. Spika, Kwa sasa *COSTEC* inajitayarisha kufanya warsha maalumu kwa Watendaji Wakuu wa Serikali kuwaelewesha juu ya Sera na Sheria zinazohusiana na mambo ya tafiti za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kamati zote za *COSTEC* zitafanyiwa mapitio ili kuwaingiza wataalamu wa Zanzibar katika kamati hizo. Uelewa huu utasaidia serikali kuanzisha Baraza la Utafiti la Zanzibar ambalo litakuwa na wajumbe kutoka sekta mbali mbali.

MWELEKEO WA BAJETI

Mapato ya Serikali:
Mhe. Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012 inatarajia kukusanya TZS 613.08 bilioni ikilinganishwa TZS 444.64 bilioni mwaka 2010/2011 ikiwa ni ziada ya TZS 168.44 bilioni sawa na asilimia 38. Hali hii inatokana na kuimarika kwa makusanyo ya ndani na kuongezeka kwa misaada ya Washirika wa Maendeleo.

Mapato ya Ndani:
Mhe. Spika, Jumla ya TZS 221.24 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kutokana na vyanzo vya ndani. TZS 210.22 bilioni zitatokana na makusanyo ya vyanzo

vya kodi na TZS 11.02 bilioni kutokana na vyanzo visivyokuwa vya kodi. Mapato ya ndani yanatarajiwa kuongezeka kwa TZS 49.55 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 28.86. Kati ya TZS 210.22 bilioni zitakazotokana na kodi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatarajiwa kukusanya TZS 100.58 bilioni wakati Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) inatarajiwa kukusanya TZS 120.66 bilioni. Makusanyo hayo ya ndani yanatarijiwa kuwa sawa na asilimia 20.2 ya Pato la Taifa. Ongezeko kubwa la mapato ya TRA linategemea kutekelezwa kwa makubaliano ya kukusanya Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar kulipwa Zanzibar. Aidha, Serikali inatarajia kukopa ndani kupitia Hati Fungani yenye thamani ya TZS 15.0 bilioni na mikopo ya kibenki ya TZS 1.6 bilioni. Vile vile, kutakuwa na bakaa ya bajeti kwa mwaka unaomalizika inayokadiriwa kufikia TZS 4.0 bilioni.

HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/12, serikali haikusudii kupandisha kodi yoyote. Serikali imekusudia kuimarisha zaidi usimamizi na ukusanyaji wa mapato kwa vianzio vilivyopo na kuziba mianya inayotumika katika kuepuka, kupunguza au kukwepa kulipa kodi pamoja na kuendelea kufuatilia matumizi mabaya ya misamaha ya kodi nchini. Lengo ni kuona kuwa kabla ya kuongeza kodi, juhudi zinachukuliwa kwanza katika kuongeza ufanisi wa ukusanyaji na uwajibikaji wa ulipaji kwenye vianzio vilivyopo na kuhakikisha kuwa misamaha inayotolewa inatumika kwa dhamira iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, katika juhudi nyengine za kuongeza na kuimarisha mapato, Serikali katika mwaka ujao itaanza kupokea marejesho ya kodi ya mapato ya mtu binafsi kwa wafanyakazi wa taasisi za Muungano wanaofanyakazi Zanzibar. Hatua hii imekuja kufuatia makubaliano yaliofikiwa kati ya SMZ na SMT katika juhudi za kushughulikia Kero za Muungano.

Mapato ya Nje:
Mhe. Spika, serikali inatarajia kupata Misaada ya Kibajeti (*GBS*) yenye jumla ya TZS 30.28 bilioni ikiwa ni asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Ruzuku na Mikopo kwa ajili ya Miradi na Programu mbali mbali inatarajiwa kufikia TZS 340.96 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 124.95 bilioni ni ruzuku na TZS 216.0 bilioni ni mikopo.

Misaada ya Kibajeti ambayo ni ruzuku kupitia *GBS* na programu/miradi inawakilisha utegemezi wa bajeti kwa asilimia 24 kwa mwaka 2011/12 ikilinganishwa na asilimia 26 kwa mwaka 2010/11. Hali hii inatokana zaidi na juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyetu vya mapato ya ndani.

Maeneo ya Kipaumbele:
Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/12, maeneo ya kipaumbele yatajikita katika kutekeleza Mkakati wa muda wa kati (MKUZA) unaolenga ukuaji wa haraka ambao utahakikisha maendeleo ya wananchi na ukuaji wa uchumi ulio endelevu pamoja na huduma bora kwa ustawi wa jamii. Kulingana na malengo ya mkakati huo maeneo yafuatayo yatapewa kipaumbele:

i) Kuimarisha huduma za afya, msisitizo zaidi ukilenga katika ununuzi wa vifaa vya hospitali, dawa muhimu pamoja na kuimarisha huduma zinazotolewa na vituo vya afya vya wilaya/mikoa.
ii) Kuimarisha ubora wa elimu kwa kupunguza tatizo la uhaba wa madawati vifaa vya maabara, vifaa vya kufundishia na kumaliza ujenzi wa madarasa yaliyoanzishwa na wananchi katika maeneo yao.
iii) Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama.
iv) Kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuendeleza shughuli za umwagiliaji, mbegu bora, mbolea na matumizi ya matrekta pamoja na kuimarisha miundombinu ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuendeleza miradi ya barabara na umeme katika maeneo ya kilimo.
v) Kuanza kuweka mazingira bora ya uwezeshaji wananchi kiuchumi
vi) Kuendeleza tafiti mbali mbali kwa lengo la kuimarisha uzalishaji na utoaji wa huduma za kijamii na maendeleo.

MATUMIZI

Mhe. Spika, serikali inatarajia kutumia TZS 613.08 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Matumizi ya Kazi za Kawaida:
Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, matumizi ya kazi za kawaida yanatazamiwa kuwa ni TZS 234.18 bilioni. Kwa kuwa Serikali imepanga kuongeza mishahara kwa watumishi wake, hivyo mishahara na posho kwa Wizara na Idara za Serikali pamoja na taasisi zinazopokea ruzuku itakuwa ni TZS 126.34 bilioni sawa na asilimia 53.9 ya matumizi yote ya kazi za kawaida ambayo ni asilimia 57.1 ya matarajio ya makusanyo ya mapato ya ndani. Aidha, kiwango hicho cha mishahara ni sawa na asilimia 11.5 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 9.9 kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Serikali pia imepanga kutumia TZS 47.75 bilioni sawa na asilimia 20.3 ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya Mfuko Mkuu. Matumizi mengineyo kwa Wizara na Idara za Serikali ni TZS 48.17 bilioni sawa na asilimia 20.1. Aidha, matumizi kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi mbali mbali zinazojitegemea ni TZS 13.05 bilioni

sawa na asilimia 5.6 ya matumizi yote ya kazi za kawaida. Serikali imechukua juhudi za kuongeza mishahara kwa watumishi wake, ili na wao waongeze tija katika utekelezaji wa majukumu yao.

Matumizi ya Kazi za Maendeleo:
Mhe. Spika, fedha kutoka nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012 zinatarajiwa kufikia TZS 340.96 bilioni. Fedha za ndani zilizotengwa na serikali kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo zinatarajiwa kufikia jumla ya TZS 37.95 bilioni. Fedha hizo zinatarajiwa kutumika kwa miradi ambayo Washirika wa Maendeleo wanaiunga mkono na ile ambayo inategemea fedha za ndani pekee. Aidha, kipaumbele kitawekwa kwa miradi yenye kuhitaji fedha za serikali kutokana na kuchangiwa na Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, matumizi kutokana na mikopo na ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo ni TZS 340.96 bilioni. Mgawanyo huu unategemea kiwango cha upatikanaji halisi wa ruzuku na mikopo katika mwaka ujao wa fedha. Jitihada zaidi za ufuatiliaji zitachukuliwa ili fedha zilizopangwa zipatikane kwa ukamilifu kwa faida ya wananchi na nchi yetu.

DENI LA TAIFA

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2011, deni la Taifa lilifikia TZS 144.79 bilioni sawa na asilimia 19 ya Pato la Taifa. Deni hilo ni sawa asilimia 84.3 ya mapato ya ndani na asilimia 74.8 ya matumizi ya kazi za kawaida kwa 2011/12. Kati ya deni hilo, jumla ya TZS 41.49 bilioni ni deni la ndani wakati deni la nje lilifikia TZS 103.30 bilioni. Kati ya deni lote, jumla ya TZS 93.50 bilioni sawa na asilimia 64.6 linadhaminiwa na Serikali ya Muungano na deni lililobakia linalipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar moja kwa moja.

Mhe. Spika, ulipaji wa riba kutokana na deni la Taifa unatarajiwa kuwa TZS 2.93 bilioni kwa 2011/12. Kiwango hicho ni pungufu kwa TZS 0.07 bilioni ikilinganishwa na makadirio ya TZS 3.0 bilioni kwa mwaka 2010/11. Uwiano wa malipo ya riba za ndani na pato la ndani ni asilimia 1.3. Ukuaji wa malipo ya madeni katika mpango wa kati unatokana na kupevuka kwa hati fungani za muda mfupi na mrefu. Hata hivyo, uwiano wa deni na Pato la Taifa unaonyesha dhahiri kuwa Zanzibar inakopesheka.

Hatua za Kuimarisha Usimamizi wa Matumizi:
Mhe. Spika, serikali inakusudia kuchukua hatua za kisera katika kusimamia matumizi ya Serikali kama ifuatavyo:

i) Kufuatilia kwa karibu Misaada ya Kibajeti (GBS) inayotarajiwa kwa mwaka ujao wa fedha ili kuepusha athari ya Kibajeti;
ii) Kusisitiza usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato ya ndani pamoja na matumizi yake;
iii) Kuimarisha usimamizi wa mikataba baina ya Serikali na sekta binafsi;
iv) Kuimarisha utaratibu wa upatikanaji wa bajeti zenye uhalisia zaidi kutoka katika sekta;
v) Kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kulipa mafao ya likizo kwa watumishi wa Serikali.

SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya mapato yote ya ndani na ya nje yanakadiriwa kufikia TZS 613.08 bilioni. Kati ya fedha hizo, mapato ya ndani yanakadiriwa kufikia TZS 221.24 bilioni, wakati mapato kutokana na misaada (ruzuku na mikopo) ya Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya Miradi na Programu za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/12 ni TZS 340.96 bilioni. Aidha, misaada ya kibajeti (4.5%) inakadiriwa kufikia TZS 30.28 bilioni. Jumla ya TZS 20.6 bilioni zinatarajiwa kupatikana kupitia mikopo na bakaa iliyoletwa kutoka bajeti itakayomalizika.

Mhe. Spika, Kwa kuzingatia masuala mbali mbali na changamoto nilizozieleza hapo juu, mapato hayo yanatarajiwa kugawanywa kama ifuatavyo: TZS 234.18 bilioni kutumiwa kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 378.90 bilioni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Kati ya matumizi ya kawaida, mishahara na posho kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinazopokea ruzuku ni TZS 126.34 bilioni sawa na asilimia 53.9 ya matumizi yote ya kazi za kawaida na asilimia 57.1 ya makusanyo ya mapato ya ndani. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS 47.62 bilioni sawa na asilimia 20.3 ya matumizi ya kazi za kawaida. Matumizi mengineyo kwa Wizara na Idara za Serikali ni TZS 47.17 bilioni sawa na asilimia 20.8 na matumizi mengineyo kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi mbali mbali zinazojitegemea ni TZS 13.05 bilioni sawa na asilimia 5.6 ya matumizi yote ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, Kwa upande wa matumizi ya kazi za maendeleo mchango wa Serikali unatarajiwa kufikia jumla ya TZS 37.95 bilioni. Kipaumbele kitawekwa kwa miradi yenye kuhitaji mchango wa Serikali kutokana na kufadhiliwa na Washirika wa Maendeleo. Matumizi ya fedha zinazotegemewa kutoka nje kwa ajili ya Miradi na Programu za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/12 ni TZS 340.96 bilioni. Hivyo jumla ya fedha zote kwa ajili ya kazi za maendeleo zitafikia TZS 378.90 bilioni kutoka TZS 251.20 bilioni

mwaka 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la TZS 127.70 bilioni sawa na asilimia 50.8. Makadirio hayo ya kazi za maendeleo ni sawa na asilimia 61.8 ya matumizi yote kwa 2011/2012.

Mhe. Spika, Baada ya kuwasilisha mwelekeo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/12, ufuatao ni muhtasari wa mapendekezo hayo:

Mfumo wa Bajeti ya mwaka 2011/2012

Maelezo	**Makisio** 2010/11 (TZS Bil.)	**Makisio** 2011/12 (TZS Bil.)	**Ongezeko (%)**
Mapato			
A. Mapato ya ndani	**171.69**	**221.24**	**28.9**
B. 4.5% Msaada wa kibajeti (GBS)	**55.24**	**30.28**	**(45.2)**
C. Hati fungate ya muda mrefu	**3.00**	**15.00**	**400.0**
D. Mikopo ya Kibenki	**3.00**	**1.60**	**(46.7)**
E. Bakaa iliyoletwa	**0**	**4.00**	**100.0**
F. Mikopo na Ruzuku	**211.71**	**340.96**	**61.1**
Jumla ya Mapato	**444.64**	**613.08**	**37.9**
MATUMIZI			
G. **Matumizi ya Kawaida**	193.43	234.18	21.1
i) Mishahara (Mawizara)	82.46	105.78	28.3
ii) Mishahara (ruzuku)	12.31	20.56	67.0
iii) Matumizi mengineyo (Mawizara)	39.78	47.17	18.6
iv) Matumizi mengineyo (ruzuku)	13.86	13.05	(5.8)
v) Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS)	45.00	47.62	5.8
H. MAENDELEO	**251.20**	**378.90**	**50.8**
i) Mchango wa Serikali	39.49	37.95	(3.9)
ii) Washirika wa Maendeleo	211.71	340.96	61.1
Jumla ya Matumizi	**444.64**	**613.08**	**37.9**

Chanzo*: Ofisi ya Rais - Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo*

SHUKRANI

Mhe. Spika, kwa kumalizia, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza kwa kurudi tena katika nafasi ya kuliongoza Baraza hili tukufu katika awamu hii ya saba ya Serikali ya Mfumo wa Kitaifa. Ni matumaini yangu kwamba busara na hekima zako zitaongoza vyema katika majadiliano ya vikao vya Baraza hili tukufu. Aidha, kwa kupitia kwako napenda kumshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Baraza hili tukufu, Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza lako, Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashauriano, maoni na miongozo katika mchakato mzima wa maandalizi ya bajeti ninayoiwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu. Ni imani yangu kuwa tutaendelea kushirikiana kwa nia ya kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, maandalizi ya bajeti hii yamehusisha wadau wengi wa ndani na nje ya Serikali. Napenda kuwashukuru wote waliochangia kwa kutoa maoni ambao ni pamoja na Watendaji Wakuu na wafanyakazi wa Wizara Mbali mbali, Idara zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Asasi zote za Serikali na sekta binafsi. Michango yao ilisaidia kufanikisha utayarishaji wa bajeti hii. Aidha, napenda kuwashukuru watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha miswada na nyaraka mbali mbali za sheria ambazo ni sehemu ya bajeti hii. Kwa upande wa Ofisi ya Rais – Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, napenda kutoa shukurani za pekee kwa Katibu Mkuu ndugu Khamis Mussa Omar, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Bi Amina Khamis Shaaban na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Abdi Khamis Faki. Aidha, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais - Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha na hatimae leo hii kuiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru wananchi kwa kuendelea kudumisha amani na utulivu hapa nchini kwetu hali inayopelekea kutekeleza vyema mipango yetu ya maendeleo. Sasa umefika wakati kwa Wazanzibari kujituma. Amani na utulivu upo hakuna sababu ya kuwa nyuma kimaendeleo, kila mmoja wetu atekeleza wajibu wake na hili linawezeka.

Mhe. Spika, napenda kutumia fursa hii adhimu kuwashukuru kwa dhati kabisa Washirika wetu wa Maendeleo katika kuchangia maendeleo ya nchi na wananchi wetu. Kwa hakika misaada yao imekuwa ni kichocheo kikubwa cha harakati za maendeleo nchini kwetu. Washirika wa Maendeleo waliochangia bajeti ya mwaka 2011/2012 ni Canada, Cuba, Denmark, Finland, India, Ireland, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Watu wa Korea, Japani, Marekani, Misri, Norway, Oman, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uturuki, *ACBF, ACCRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL*,

CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank of China, EXIM Bank of Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OPEC, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UN AIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO, WSPA .

HITIMISHO

Mhe. Spika, Bajeti ya 2011/2012 ni mwendelezo wa jitihada za Serikali katika kufikia maendeleo ya MKUZA, malengo ya maendeleo ya Milenia, na hatimaye Dira ya Maendeleo 2020. Hata hivyo, ili kufikia malengo yetu mapema zaidi, kila mwananchi anapaswa kuwajibika na kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zinazojitokeza kwa kuzalisha mali na kujiongezea kipato.

Mhe. Spika, ushiriki katika uzalishaji kwa wananchi mmoja mmoja au vikundi ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu. Aidha, sekta za kilimo, mifugo na viwanda zikiboreshwa na kutiliwa mkazo, usindikaji wa mazao ya kilimo una nafasi kubwa ya kuchangia Pato la Taifa na kukuza ajira. Bajeti hii pia inalenga kuongeza jitihada za serikali za kuimarisha matumizi bora ya ardhi, miundombinu na mawasiliano.

Mhe. Spika, Ili kuimarisha ukuzaji wa uchumi wetu, hatuna budi kufikiria mipango ya muda mrefu ambayo itachochea ari na ushindani katika uzalishaji kwa kutumia rasilimali zetu za ndani ambazo zitapelekea uchumi wa kisasa na tija kwa nchi. Mafanikio katika kukuza na kuendeleza mipango yetu ya kiuchumi hayawezi kupimwa kwa kuangalia upande mmoja, ni lazima miundombinu ya kiuchumi katika sekta mbali mbali iungane. Vile vile, kujituma pamoja na kuwa na maadili mema katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ni muhimu; maadili yanaweza kutokomeza umasikini uliokithiri.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumalizia kwa kusisitiza kuwa Bajeti hii inalenga zaidi katika kuimarisha na kuleta maendeleo ya kiuchumi pamoja na maslahi ya wafanyakazi na wananchi kwa jumla. Tumeeleza changamoto zinazotukabili katika vyanzo vyetu vya ukuaji wa uchumi na ukusanyaji wa mapato. Hatuna budi kuwa na mikakati maaalum ya kukabiliana na changamoto hizo. Dhamira ya serikali ni kujenga uwezo kwa watoto, vijana na wafanyakazi hatimae waweze kujenga uchumi wenye kuendana na ushindani katika dunia. Serikali inalengo la kufikia maendeleo ya kiuchumi ambayo yatazaa tija ya maisha tulivu na maslahi bora kwa wananchi wake. Mpango wetu wa muda mrefu ni dira ya maendeleo ya kiuchumi ambao unatoa muongozo wa kuondosha umasikini uliokithiri, makazi bora na usalama wa chakula kwa nia ya kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Bajeti yetu hii imeeleza

kwa uwazi kuhusu malengo yetu. Mwisho namalizia kwa kusema “Kipimo cha ufanisi wa mtu si wapi amesimama wakati wa faraja, bali wapi amesimama wakati wa changamoto”.

Mhe. Spika, kwa heshima, taadhima na unyenyekevu, naomba sasa Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimae lipitishe mapendekezo juu ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2011/2012, ili yawe muongozo wa utekelezaji wa shughuli za serikali kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, serikali inapendekeza mbele ya Baraza lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kukusanya jumla ya **shilingi Mia Sita na Kumi na Tatu bilioni, na Sabiini na Sita milioni** (TZS 613,076 millioni) pamoja na matumizi ya **shilingi bilioni Mia Mbili na Thelathini na Nne, milioni Mia Moja na Sabiini na Tano** (234.175 bilioni) kwa kazi za kawaida na **shilingi bilioni Mia Tatu Sabiini na Nane, milioni Mia Tisa na Moja** (378.901 bilioni) kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Spika: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa makofi ya kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuisoma Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuisoma Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kiasi cha muda wa saa 2 na dakika kama ishirini hivi. Kwa niaba yenu nataka nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba hii ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa utulivu na ufanisi mkubwa.

Vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wageni wetu, kwamba kwa muda wote ambao Mhe. Waziri alikuwa anawasilisha hotuba ya bajeti, tumekuwa watulivu na kumsikiliza kwa makini sana wakati anawasilisha hotuba hiyo.

Kwa mujibu wa taratibu za kanuni chini ya ibara ya 92(5) na (6) inahitaji Mhe. Waziri atowe hoja ya kuahirisha mjadala wa hotuba hii kwa kiasi ya muda wa siku mbili, zisizozidi siku mbili za kazi ili Waheshimiwa Wajumbe wapate nafasi ya kujichimbia na kuisoma kwa makini hotuba hii ili kuja kuanza mjadala wiki ijayo. Kwa maana hiyo basi nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kutoa hoja hiyo chini ya ibara ya 92(5) na (6) ili kuweza kuahirisha mjadala huu, Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Waziri wa Nchi anayeshughulikia Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na kwa kuwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wanahitaji muda wa kuipitia bajeti hii. Kwa hivyo, tunapendekeza kwako Mhe. Spika, kuliahirisha Baraza letu hili tukufu mpaka Jumatatu tarehe 20/06/2011 saa 3:00 asubuhi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuahirisha shughuli zetu za jioni hii, naomba nitowe matangazo mawili. Tangazo la kwanza mara baada ya kuahirishwa shughuli zetu hizi, hapo nje pameandaliwa vitafunio na vinywaji, ili baada ya kazi kubwa hii aliyoifanya Mhe. Waziri, pamoja na kwamba wakati umekuwa mkubwa kidogo, lakini tuweze kutafuna tafuna na kubadilishana mawazo juu ya hotuba ya bajeti iliyotolewa hivi punde nzuri na Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, naomba niwaalike Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na wageni wetu, tukusanyike hapo nje ili kuifanya kazi hiyo kuweza kukamilisha kikao chetu hiki cha jioni.

Pili, Waheshimiwa Wajumbe, mtakumbuka kwamba tuliomba tufanye semina mahususi kuhusiana na suala la shughuli zetu. Naomba kutoa taarifa kwamba semina hiyo itakuwepo siku ya Jumamosi, tarehe 18/06/2011 mnamo saa 3:00 asubuhi na tutatoka hapa tutakwenda pale *Ocean View*. Semina hiyo ni ya siku moja na tunategemea Waheshimiwa Wajumbe tutapata taaluma ya kutosha juu ya masuala ya bajeti.

Waheshimiwa Wajumbe, hayo ndio matangazo mawili yaliopo na sasa niko tayari ili kuweza kuahirisha kikao chetu cha jioni hii.

Waheshimiwa Wajumbe, naahirisha kikao hiki mpaka tarehe 20/06/2011 saa 3:00 barabara za asubuhi ambapo tutaanza mjadala wa hotuba hii ya bajeti. Nakushukuruni sana.

(Saa 12:40 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 20/06/2011 Saa 3:00 za asubuhi)